JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA

MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KATIKA MUDA WA KATI (2026/27 - 2028/29)

February, 2026

YALIYOMO

YALIYOMO 1

VIFUPISHO I

MUHTASARI 2

1. MUHTASARI WA MWENENDO NA MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI NA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI 4

1.1 Utangulizi 4

1.2 Mwenendo na Mwelekeo wa Uchumi 4

1.3 Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2024/25 8

1.4 Mwenendo wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Kipindi cha Robo ya Kwanza ya Mwaka 2025/26 8

2. VIPAUMBELE VYA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2026/27 HADI 2028/29 9

2.1 Utangulizi 9

2.2 Maeneo Mahsusi ya Vipaumbele kwa Mwaka 2026/27 10

2.3 Shabaha na Misingi ya Uchumi Jumla 11

2.4 Makadirio ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka katika kipindi cha Muda wa Kati 12

3. USIMAMIZI WA VIHATARISHI VYA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI 19

3.1. Utangulizi 19

3.2. Vihatarishi vya Uchumi Jumla 19

3.3. Vihatarishi Mahsusi 21

4. MAELEKEZO YA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KATIKA MUDA WA KATI 24

4.1 Maandalizi ya Mpango na Bajeti 24

4.2 Maelekezo ya Jumla ya Uandaaji wa Mpango na Bajeti 28

4.3 Maelekezo Mahsusi kwa Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma 33

4.4 Maelekezo kwa Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa 34

4.5 Masuala Mengine Muhimu ya Kuzingatiwa Wakati wa Uandaaji wa Mpango na Bajeti 37

4.6 Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji Taarifa za Utekelezaji wa Mpango na Bajeti 45

VIFUPISHO

CBR	Central Bank Rate
COSTECH	Tanzania Commission for Science and Technology
DCF	Development Co-operation Framework
EAC	East African Community
EFD	Electronic Fiscal Device
EPZs	Export Processing Zone
FDI	Foreign Direct Investment
FYDP	Five Years Development Plan
GFS	Government Finance Statistics
GNI	Gross National Income
IMF	International Monetary Fund
MKUMBI	Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji
MTEF	Medium Term Expenditure Framework
MTAKUWWA	Mpangokazi wa Pili wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto
PPP	Public Private Partnership
SADC	Southern African Development Community
SEZs	Special Economic Zone
TARURA	Tanzania Rural and Urban Road Agency
TEHAMA	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
UKIMWI	Upungufu wa Kinga Mwilini
WEO	World Economic Outlook

MUHTASARI

Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali umeandaliwa kwa mujibu wa Kifungu cha 21 cha Sheria ya Bajeti, Sura 439. Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali katika Muda wa Kati (2026/27 - 2028/29) ni wa kwanza katika utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/27 – 2030/31). Maandalizi ya Mwongozo huu yamezingatia: Dira 2050; Ilani ya CCM ya Uchaguzi wa Mwaka 2025, Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/27 – 2030/31); Makubaliano ya Paris kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi; Agenda 2063 ya Maendeleo ya Afrika; Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030; Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki 2050; Dira ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika 2050; na maelekezo mbalimbali ya Serikali.

Mwongozo unatoa mwenendo na mwelekeo wa viashiria vya uchumi, sera za fedha na bajeti, vipaumbele vya bajeti na maelekezo kwa Maafisa Masuuli wote kuhusu masuala ya kuzingatia wakati wa maandalizi na utekelezaji wa mpango na bajeti katika muda wa kati. Uchumi wa Tanzania unatarajiwa kuendelea kuimarika ambapo katika muda wa kati; Pato halisi la Taifa linatarajiwa kukua kwa asilimia 6.9, mapato ya kodi kufikia wastani wa asilimia 13.7 ya Pato la Taifa, mfumuko wa bei kuwa kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya 3.0 - 5.0 na nakisi ya bajeti kuwa chini ya asilimia 3.0 ya Pato la Taifa. Deni la Serikali linatarajiwa kuwa himilivu kwa kipindi cha muda wa kati na mrefu kwa mujibu wa tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Novemba 2025. Aidha, utekelezaji wa bajeti katika kipindi cha muda wa kati utazingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/27 – 2030/31) wenye dhima “Mageuzi kwa ajili ya Ukuaji Jumuishi wa Uchumi na Uzalishaji wa Fursa za Ajira”.

Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali 2026/27 - 2028/2 katika Muda wa Kati (2026/27 - 2028/29) umetoa **Maelekezo ya Kimkakati** ya kuzingatiwa na Maafisa Masuuli ambayo yanaakisi dhana ya mageuzi muhimu iliyobainishwa katika FYDP IV. **Maelekezo ya Kimkakati** yaliyobainishwa ni hatua ambazo zinatarajiwa kuwa na matokeo chanya katika kuchochea ukuaji wa uchumi, kuimarisha uwekezaji, kuibua na kuongeza fursa za ajira kwa wazawa na kudhibiti nakisi ya bajeti (fiscal consolidation) kwa kuimarisha ukusanyaji wa mapato na udhibiti wa matumizi ya fedha za umma. Pia hatua hizi zinatarajiwa kuboresha usimamizi wa mipango na bajeti ili kuleta tija katika matumizi ya fedha za umma. Vilevile, Mwongozo umetoa maelekezo mengine ya masuala muhimu ya kuzingatiwa katika uandaaji na utekelezaji wa mpango na bajeti ya Serikali ikiwemo: kuimarisha ukusanyaji wa mapato; kuimarisha utendaji wa Kamati za Bajeti; kudhibiti uzalishaji wa madeni; uandaaji wa bajeti ya mlengo wa kijinsia, masuala ya muungano, uchumi wa kidigitali na uandaaji wa makadirio ya bajeti kwa kuzingatia miongozo, nyaraka na mifumo iliyopo.

Mwongozo umegawanyika katika sura nne ambazo ni: Muhtasari wa Mwenendo na Mwelekeo wa Uchumi na Utekelezaji wa Mpango na Bajeti; Vipaumbele vya Mpango na Bajeti ya Mwaka 2026/27 hadi 2028/29; Usimamizi wa Vihatarishi vya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti; na Maelekezo ya Maandalizi ya Mpango na Bajeti katika Muda wa Kati. Aidha, Mwongozo utasomwa sambamba na Viambatisho vyake (1A – 1G).

SURA YA KWANZA

MUHTASARI WA MWENENDO NA MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI NA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI

1.1 Utangulizi

1. Sura hii inaelezea tathmini ya mwenendo na mwelekeo wa viashiria vya hali ya uchumi ikiwemo ukuaji wa uchumi, mfumuko wa bei, mikopo kwa sekta binafsi, viwango vya riba, mikopo chechefu, deni la Serikali pamoja na utekelezaji wa mpango na bajeti.

1.2 Mwenendo na Mwelekeo wa Uchumi

1.2.1 Ukuaji wa Uchumi wa Dunia na Kikanda

2. Uchumi wa dunia umeendelea kuimarika licha ya kukabiliana na changamoto mbalimbali ikiwemo zilizotokana na migogoro ya kikanda na kutokutabirika kwa sera za biashara. Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa - IMF World Economic Outlook (WEO), toleo la Oktoba 2025, uchumi wa dunia ulikua kwa wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 3.5 mwaka 2023. Kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia inatarajia kuendelea kupungua kufikia wastani wa asilimia 3.2 mwaka 2025 na asilimia 3.1 mwaka 2026. Maoteo hayo yanatokana na matarajio ya utekelezaji wa sera za bajeti zinazolenga kuongeza fedha katika uchumi na kupungua kwa athari zitokanazo na utekelezaji wa sera za bajeti zinazolenga kuongeza ushuru kwa mataifa yaliyoendelea hususan nchi ya Marekani.

3. Kwa mujibu wa taarifa ya IMF ya Oktoba 2025, uchumi wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki - EAC ulikua kwa wastani wa asilimia 1.7 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 5.3 mwaka 2023. Kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi wa ukanda wa EAC ilichangiwa na kuporomoka kwa uchumi wa nchi ya Sudani Kusini ambao ulikuwa na ukuaji hasi wa asilimia 26.1 mwaka 2024. Uchumi wa nchi za EAC unakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 7.7 mwaka 2025 na mwaka 2026.

1.2.2 Ukuaji wa uchumi wa Tanzania

4. Kwa mujibu wa taarifa za Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Pato halisi la Taifa kwa kuzingatia mwaka wa kizio 2019 lilikua kwa asilimia 5.6 mwaka 2024 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.2 mwaka 2023. Ukuaji huo ulichangiwa na: uwekezaji wa Serikali kwenye miradi ya kimkakati na ya kielelezo inayohusisha miundombinu ya nishati na usafirishaji; kuanza kwa uzalishaji wa umeme katika Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Julius Nyerere; kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi; usimamizi madhubuti wa sera za fedha; kuimarika kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo; kuimarika kwa huduma za fedha na bima; pamoja na uwekezaji wa Serikali katika huduma za jamii ikiwemo elimu, afya, maji na hifadhi ya jamii.

5. Shughuli za kilimo zimeendelea kuwa na mchango mkubwa katika Pato la Taifa kwa kuchangia asilimia 24.9, ikifuatiwa na shughuli za ujenzi (asilimia 12.5), biashara na matengenezo (asilimia 8.6) na usafiri na usafirishaji (asilimia 8.1). Aidha,

sekta zilizochangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa Pato la Taifa ni sekta ya kilimo iliyochangia asilimia 20.8 ikifuatiwa na usafiri na usafirishaji (asilimia 10.4) na fedha na bima (asilimia 9.3). Kwa mujibu wa taarifa ya Benki ya Dunia iliyotolewa tarehe 01 Julai 2025, wastani wa pato kwa kila mtu (Per Capita GNI) umeongezeka na kufikia dola za Marekani 1,200 (sawa na takribani shilingi 3,116,825) mwaka 2024 ikilinganishwa na dola za Marekani 1,136 ambao ni wigo wa chini kwa nchi zenye uchumi wa kipato cha chini ngazi ya kati (lower middle income).

6. Pato halisi la Taifa kwa kipindi cha Januari hadi Juni 2025 lilikua kwa wastani wa asilimia 5.8 ikilinganishwa na asilimia 5.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2024.Ukuaji huo ulichangiwa zaidi na shughuli za madini, kilimo, ujenzi na fedha na bima. Mfumuko wa bei ulikuwa wastani wa asilimia 3.1 kama ilivyokuwa katika mwaka 2023/24. Mwenendo huo ulichangiwa na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti na utulivu wa bei za mafuta katika soko la dunia. Hata hivyo, uchambuzi wa awali iliofanywa kuhusiana na athari za matukio ya wakati na baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 unaonesha uwezekano wa kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi hususan katika robo ya nne ya mwaka 2025. Hivyo, lengo la ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2025 la asilimia 6.0 linakadiriwa kupungua hadi asilimia 5.9.

1.2.3 Mfumuko wa Bei

7. Katika kipindi cha Julai hadi Novemba 2025, wastani wa mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 3.4 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Aidha, mfumuko wa bei kwa mwezi Novemba, 2025 ulikuwa asilimia 3.4 ikilinganishwa na asilimia 3.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Hii ilitokana na kupungua kwa ugavi wa bidhaa za vyakula katika soko la ndani kufuatia ongezeko la mauzo kwenda nchi jirani. Kiwango hicho kipo ndani ya lengo la nchi la asilimia 3.0 hadi 5.0. Vilevile, kiwango hicho kipo ndani ya lengo la Jumuiya ya Afrika Mashariki la kutozidi asilimia 8.0 na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika la kati ya asilimia 3.0 hadi asilimia 7.0. Hii ilitokana na utekelezaji wa sera madhubuti za fedha, kuimarika kwa bei ya mafuta na bidhaa katika soko la dunia, na utulivu wa thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani iliyochangia kupunguza kasi ya ongezeko la bei ya bidhaa na huduma.

1.2.4 Ujazi wa Fedha

8. Utekelezaji wa sera ya fedha uliwezesha ujazi wa fedha (M3) kukua na kufikia wastani wa asilimia 21.0 kwa kipindi cha miezi mitano ya kwanza ya mwaka 2025/26, kutoka asilimia 12.1 katika kipindi kama hicho cha mwaka 2024/25, kufuatia uwepo wa ukwasi wa kutosha kwenye uchumi. Aidha, M3 ilikua kwa asilimia 23.0 Novemba 2025 ikilinganishwa na asilimia 13.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2024.

1.2.5 Mikopo kwa Sekta Binafsi

9. Katika kipindi cha Julai hadi Novemba 2025, mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa wastani wa asilimia 16.5, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 16.8 katika

kipindi kama hicho mwaka 2024. Hadi Novemba 2025, ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ulifikia asilimia 18.1 kwa mwaka, ikilinganishwa na asilimia 15.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Hii ilitokana na utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi kwenye uchumi.

1.2.6 Viwango vya Riba

10. Riba za mikopo zilipungua na kufikia wastani wa asilimia 15.27 mwezi Novemba 2025 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 15.67 Novemba 2024. Aidha, katika kipindi cha miezi mitano ya kwanza ya mwaka 2025/26 riba za mikopo zilipungua na kufikia wastani wa asilimia 15.18 ikilinganishwa na asilimia 15.49 katika kipindi kama hicho mwaka 2024/25. Mwenendo huu unaakisi utekelezaji madhubuti wa sera ya fedha pamoja na hatua za kisera zilizochukuliwa na Benki Kuu katika kuhakisha kunakuwa na ukwasi wa kutosheleza shughuli za kiuchumi na kuchochea ongezeko la ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi.

11. Wastani wa riba za amana uliongezeka na kufikia asilimia 8.54 Novemba 2025, ikilinganishwa na asilimia 8.18 Novemba 2024. Ongezeko hilo lilitokana na jitihada za mabenki kuvutia amana kwa kutoa riba shindani. Aidha, katika kipindi cha miezi mitano ya kwanza ya mwaka 2025/26 wastani wa riba za amana ulikuwa asilimia 8.57 ikilinganishwa na asilimia 8.15 katika kipindi kama hicho mwaka 2024/25. Kwa kuzingatia mwenendo huo, wigo kati ya riba za mikopo na amana za mwaka mmoja (*interest rate spread*) ulipungua hadi asilimia 5.51 Novemba 2025 kutoka asilimia 5.93 mwaka 2024.

1.2.7 Mikopo Chechefu

12. Mikopo chechefu ilipungua na kufikia asilimia 3.1 mwezi Novemba, 2025, ikilinganishwa na asilimia 3.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Kupungua kwa mikopo chechefu kulitokana na hatua mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali kwa kushirikiana na Benki Kuu zikiwemo: Kutoa maelekezo kwa benki kuendelea kutumia kanzidata ya taarifa za wakopaji (credit reference system) katika utoaji wa mikopo; kuimarisha mifumo ya udhibiti wa benki; benki kuendelea kuimarisha viwango vya uchambuzi wa maombi ya mikopo; kusimamia maadili ya wafanyakazi wa benki; na kufanya ukaguzi maalum wa wafanyakazi (staff audit) wa benki mara kwa mara. Lengo la hatua hizi ni kuhakikisha kiwango cha mikopo chechefu kinaendelea kuwa chini ya wastani wa asilimia 5.0.

1.2.8 Viwango vya Ubadilishaji Fedha

13. Mwenendo wa thamani ya shilingi dhidi ya sarafu nyingine duniani ulibadilika kuendana na hali ya ukwasi wa fedha za kigeni nchini sambamba na mwenendo wa uchumi wa Dunia, misimu ya mauzo ya mazao ya biashara na dhahabu nje ya nchi pamoja na shughuli za utalii. Katika kipindi cha miezi mitano ya kwanza ya mwaka 2025/26 thamani ya shilingi dhidi ya sarafu za nchi washirika wakuu wa kibiashara iliendelea kuwa imara. Mwenendo huo ulitokana na kuimarika kwa uchumi wa dunia na kuongezeka kwa mapato ya fedha za kigeni kutokana na shughuli za utalii na mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi. Vilevile, mabadiliko ya Kifungu cha 26 cha

Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania kinachozuia matumizi ya fedha za kigeni katika miamala ya ndani, ulichangia kupunguza mahitaji ya fedha za kigeni nchini. Kutokana na hali hii, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,444.81 mwezi Novemba 2025, ikilinganishwa na shilingi 2,659.03 katika kipindi kama hicho mwaka 2024, sawa na ongezeko la thamani ya shilingi kwa asilimia 8.1, kwa mwaka.

1.2.9 Sekta ya Nje

14. Sekta ya nje imeendelea kuimarika licha ya kuwepo kwa migogoro ya kisiasa na mivutano ya kibiashara duniani. Katika kipindi cha Julai hadi Novemba 2025, nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamishaji mali nje ya nchi ilipungua na kufikia dola za Marekani milioni 433.1 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 632.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Mwenendo huu ulitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi, hususan mapato yatokanayo na utalii na mauzo ya bidhaa zisizo asilia sambamba na kasi ndogo ya uagizaji wa bidhaa nje ya nchi. Aidha, thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma iliongezeka hadi dola za Marekani milioni 8,316.9 kutoka dola za Marekani milioni 7,728.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 7.6. Vilevile, thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje iliongezeka kwa kasi ndogo ya asilimia 2.4 na kufikia dola za Marekani milioni 7,929.9 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 7,742.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Mwaka 2025/26 na katika kipindi cha muda wa kati, urari wa malipo ya kawaida unatarajiwa kupungua kutoka asilimia 2.5 ya pato la Taifa mwaka 2024/25 hadi wastani wa asilimia 2.0 katika kipindi cha muda wa kati. Hii ni kutokana na matarajio ya kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa na huduma nje na kupungua kwa uagizaji wa bidhaa na huduma. Maelezo ya kina kuhusu mwenendo na mwelekeo wa hali ya uchumi yanapatikana katika **Kiambatisho Na. 1A**.

1.2.10 Uwekezaji wa Moja kwa Moja Kutoka Nje (FDI)

15. Uwekezaji wa Moja kwa Moja Kutoka Nje (*Foreign Direct Investment*) umeendelea kuimarika, ambapo mwaka 2023 uliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 1,648.2 kutoka dola za Marekani milioni 1,437.0 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 14.7. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mikopo baina ya makampuni (*intercompany loans*), ambapo mchango wake katika jumla FDI ulikuwa asilimia 43.1 mwaka 2023 kutoka asilimia 8.7 mwaka 2022. Mwenendo huu unaakisi juhudi za Serikali katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini.

1.2.11 Deni la Serikali

16. Deni la Serikali limeendelea kuwa himilivu ambapo hadi Novemba 2025 lilikuwa shilingi bilioni 109,012.72 ikilinganishwa na shilingi bilioni 100,352.49 katika kipindi kama hicho mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 8.63. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani lilikuwa shilingi bilioni 38,181.30 (sawa na asilimia 35 ya deni lote) na deni la nje lilikuwa shilingi bilioni 70,831.42. Ongezeko la deni limetokana na Serikali kuendelea kupokea fedha za mikopo kutoka vyanzo mbalimbali kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli,

viwanja vya ndege, umeme na maji. Tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Oktoba 2025 imebainisha kuwa deni la Serikali bado ni himilivu, ambapo viashiria vyote vikiwa ndani ya viwango vinavyokubalika kimataifa kwa kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu. Aidha, tathmini hiyo inaonesha kuwa katika mwaka 2024/25 uwiano wa deni la Serikali kwa Pato la Taifa umeendelea kubaki chini ya ukomo wa asilimia 55 wa Pato la Taifa na pia chini ya ukomo wa asilimia 50 unaotumika kama kigezo cha muunganiko wa viashiria vya uchumi jumla kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

1.3 Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2024/25

17. Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania liliidhinisha bajeti ya Serikali ya shilingi bilioni 50,291.4 kwa mwaka 2024/25. Hadi Juni 2025, Serikali ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 49,821.2 kutoka vyanzo vya ndani na nje, sawa na asilimia 99.1 ya lengo la mwaka. Kati ya kiasi hicho, mapato ya ndani yalikuwa shilingi bilioni 34,845.9, sawa na asilimia 100.7 ya lengo la mwaka na misaada shilingi bilioni 880.1 sawa asilimia 110.8. Aidha, mikopo ya ndani na nje ilikuwa shilingi bilioni 14,095.2 sawa na asilimia 94.7.

18. Katika mwaka 2024/25, Serikali ilitoa ridhaa ya matumizi ya jumla ya shilingi bilioni 49,821.2, sawa na asilimia 99.1 ya bajeti. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 34,418.4 zilitolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikiwemo mishahara ya watumishi wa umma, ugharamiaji wa deni la Serikali na uendeshaji wa shughuli za Serikali. Aidha, shilingi bilioni 15,402.7 zilitolewa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Nakisi ya bajeti iliendelea kuimarika na kufikia asilimia 3.1 ya Pato la Taifa mwaka 2024/25 kutoka asilimia 3.2 mwaka 2023/24 kutokana na utekelezaji madhubuti wa sera za bajeti. Maelezo ya kina yanapatikana katika **Kiambatisho Na. 1B**.

1.4 Mwenendo wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2025/26

19. Bajeti ya Serikali iliyoidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mwaka 2025/26 ni shilingi bilioni 56,490.3. Bajeti inagharamiwa na mapato ya ndani shilingi bilioni 40,466.1 na misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo shilingi bilioni 1,069.9. Aidha, nakisi ya bajeti inagharamiwa na mikopo ya ndani shilingi bilioni 6,278.2 na mikopo ya nje shilingi bilioni 8,676.1.

20. Katika kipindi cha julai hadi Novemba 2025, Serikali ilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 22,881.0 kutoka vyanzo vya ndani na nje sawa na asilimia 98.6 ya lengo la kipindi hicho. Matumizi ya Serikali yalikuwa shilingi bilioni 22,937.6, sawa na asilimia 98.8. Matumizi ya shilingi bilioni 56.5 yaliyozidi mapato yaligharamiwa na mkopo wa muda mfupi kutoka Benki Kuu. Maelezo ya kina yanapatikana katika **Kiambatisho Na. 1C**.

SURA YA PILI

VIPAUMBELE VYA MPANGO NA BAJETI

2.1 Utangulizi

21. Serikali imekuwa ikiandaa makadirio ya mapato na matumizi katika kipindi cha muda wa kati ambayo yamekuwa yakiainishwa katika Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti. Katika jitihada za kuimarisha: usimamizi wa utekelezaji wa bajeti; uandaaji wa mpango na bajeti katika mafungu; na mwelekeo wa Serikali katika utekelezaji wa vipaumbele, programu na miradi mbalimbali ya maendeleo, Mwongozo huu unapendekezwa kutumika katika kipindi cha muda wa kati (2026/27 – 2028/29).

22. Utekelezaji wa bajeti katika kipindi cha muda wa kati unatarajiwa kuwa mwanzo wa Serikali kuwa na sera za kibajeti zinazotabirika, hivyo kuongeza uaminifu wa bajeti (credibility). Aidha, kila mwaka Serikali itakuwa inawasilisha bungeni mapendekezo ya makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali ambayo hayatarajiwi kuwa na utofauti mkubwa na makadirio yaliyoidhinishwa katika mwongozo wa muda wa kati. Mapendekezo hayo yatategemea tathmini ya mapitio ya utekelezaji wa Mwongozo na kwa kuzingatia mwenendo wa viashiria mbalimbali vya uchumi jumla.

23. Mwongozo wa Mpango na Bajeti katika muda wa kati ni wa kwanza katika utekelezaji wa Dira 2050. Dira 2050 inaainisha ajenda ya maendeleo ya nchi kwa kipindi cha miaka 25 ijayo (2026 - 2050) ikiwa na lengo kuu la kuifanya Tanzania kuwa Taifa Jumuishi, Lenye Ustawi, Haki na Linalojitegemea. Malengo na shabaha mahsusi za Dira 2050 ni pamoja na: Kuiwezesha Tanzania kuwa nchi ya kipato cha kati ngazi ya juu yenye Pato la Taifa lenye thamani ya dola za Marekani trilioni moja (1) na Wastani wa Pato la Taifa kwa Kila Mtu (GNI Per Capita) lenye thamani ya angalau dola za Marekani 7,000; Maisha bora na ustawi kwa wote; Taifa linalohifadhi mazingira na kustahimili mabadiliko ya tabianchi; na Jamii yenye umahiri, ujuzi na inayotumia teknolojia za kidijitali.

24. Malengo ya Dira 2050 yatafikiwa kupitia utekelezaji wa Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu (Long Term Perspective Plan - LTPP 2050), ambao utazingatia kuanza na maeneo ya msingi yenye uwezo mkubwa wa kufungua na kuchochea fursa za maendeleo katika sekta mbalimbali. Mpango huo utatekelezwa kupitia awamu tano (5) mfululizo za Mipango ya Taifa ya Maendeleo ya Miaka Mitano (Five Years Development Plans – FYDPs) ambazo ni: FYDP IV, FYDP V, FYDP VI, FYDP VII na FYDP VIII. Vilevile, kupitia Mwelekeo na Ilani ya Chama Tawala. Utekelezaji wa mipango hii utaanza na Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/27 – 2030/31) ambao ni wa kwanza katika utekelezaji wa LTPP 2050. Kwa muktadha huo, Mwongozo wa Mpango na Bajeti ya Serikali umezingatia vipaumbele vilivyoanishwa katika FYDP IV ya utekelezaji wa Dira 2050.

2.2 Maeneo Mahsusi ya Vipaumbele

25. Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/27 – 2030/31) una dhima ya "Mageuzi kwa ajili ya Ukuaji Jumuishi wa Uchumi na Uzalishaji wa Fursa za Ajira". Mwongozo wa muda wa kati umejielekeza katika maeneo ya vipaumbele vya FYDP IV ambavyo ni: Uchumi imara, jumuishi na shindani; kujenga uwezo wa rasilimali watu na maendeleo ya jamii; uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi; kuimarisha msingi wa uendelevu wa Taifa pamoja na programu za kielelezo. Aidha, msisitizo umewekwa katika kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi na kuwezesha taasisi za Serikali kuwekeza katika miradi ya kimkakati ambayo itachochea ukuaji wa uchumi.

(i) Uchumi Imara, Jumuishi na Shindani

26. Mpango unatoa kipaumbele katika mageuzi yanayoimarisha utulivu wa uchumi jumla, mifumo endelevu ya kibajeti, uwezo wa nchi kuhimili misukosuko kutoka nje na kuchochea kasi ya mabadiliko katika sekta za uzalishaji. Mageuzi haya yatachochea kasi ya uongezaji thamani, kupunguza gharama za miamala, kuimarisha ushindani wa mauzo ya nje, na kuwezesha bidhaa na kampuni za ndani kuingia katika masoko ya kikanda na kimataifa. Uboreshaji wa sera za fedha na usimamizi wa mifumo ya kifedha utawezesha kutumia mfumo wa kisasa unaoongozwa na riba, kuboresha usimamizi wa ukwasi na kuongeza ufanisi wa kusimamia sera. Hatua za kimkakati zinalenga kupanua wigo wa masoko ya mitaji ya ndani ikiwemo hati fungani za kijani, hati fungani za buluu, na hati fungani za miundombinu. Vilevile, hatua hizo zitaboresha uwazi katika usimamizi wa deni la Serikali, kuimarisha ustahimilivu na uwezo wa nchi kuhimili misukosuko kutoka nje kupitia utofauti wa rasilimali na mitiririko ya fedha, na kuimarisha mifumo ya ushuru ya kidijitali ili kuongeza mapato. Mageuzi haya yataongeza fursa za upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya kuendeleza viwanda, miundombinu ya usafirishaji, na ubunifu hivyo kuongeza nafasi ya Tanzania kushindana kimataifa.

(ii) Kujenga Uwezo wa Rasilimali Watu na Maendeleo ya Jamii

27. Mpango unaweka kipaumbele katika kujenga uwezo wa rasilimali watu na maendeleo ya jamii kama misingi wa kufikia lengo la kuwa taifa jumuishi lenye ustawi, haki na linalojitegemea. Mpango unalenga kuzalisha nguvukazi iliyoelimika, yenye ujuzi, motisha na uwezo wa kushindana, kunufaika na ongezeko la idadi ya watu, na kushughulikia pengo la ujuzi na mahitaji ya soko ili kuongeza wigo wa fursa za ajira na uchumi. Mpango unaimarisha hifadhi ya jamii na kuboresha huduma za afya, makazi, upatikanaji wa maji safi na huduma za usafi na kuboresha hali ya maisha ya wananchi. Aidha, Mpango unajenga jamii zenye mshikamano, uwajibikaji na ushiriki mahiri katika shughuli za maendeleo vijijini na mageuzi ya vyama vya ushirika. Lengo kuu ni kupanua wigo wa tabaka la kati ambalo ni muhimu kwa kuimarika kwa uchumi, jamii kuwa na maendeleo, na ustawi endelevu wa taifa.

(iii) Uhifadhi wa Mazingira na Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi

28. Uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi ni msingi muhimu wa maendeleo endelevu ya Tanzania. Eneo hili linachochea uendelezaji wa

viwanda, ukuaji wa miji, ustawi wa maisha ya watu na mifumo thabiti ya ikolojia. Licha ya FYDP III kufanikiwa kurejesha misitu, kuhifadhi bioanuwai, nishati jadidifu na kuboresha mifumo ya utoaji tahadhari mapema, changamoto za kimazingira na athari za mabadiliko ya tabianchi zinaendelea kuongezeka. Kwa kuzingatia changamoto hiyo, FYDP IV inatoa kipaumbele katika utekelezaji wa hatua jumuishi zinazolenga kuimarisha uhifadhi wa mazingira, mifumo endelevu ya matumizi ya ardhi, ukuaji wa miji, shughuli za maendeleo zinazochangia hewa ukaa kwa kiasi kidogo, pamoja na kuboresha mifumo ya kisasa ya utoaji tahadhari mapema. Hatua hizi zinachangiwa na utekelezaji wa programu za kimkakati, mifumo ya ufuatiliaji na tathmini ya kidijitali, na ubunifu katika upatikanaji wa fedha zinazogharamia ajenda ya mabadiliko ya tabianchi ikiwemo masoko ya kaboni. Jitihada hizo zinalenga kulinda mtaji asilia wa taifa, kuongeza ustahimilivu, na kuweka msingi wa mageuzi nchini kuelekea uchumi wa kijani unaostahimili athari za mabadiliko ya tabianchi.

(iv) **Kuimarisha Msingi wa Uendelevu wa Taifa**

29. Mafanikio ya utekelezaji wa Mpango unategemea misingi imara ya ustawi uendelevu inayotokana na utawala bora, demokrasia, umoja, usalama na mabadiliko chanya ya fikra za wananchi. Misingi hii inawezesha kuwepo kwa uwazi, uwajibikaji, usimamizi madhubuti wa rasilimali za umma, na mazingira tulivu kwa ajili ya ukuaji jumuishi na endelevu wa uchumi. Mageuzi ya kitaasisi ni muhimu ili kuboresha utendaji na mifumo ya kisheria na kuchochea ubunifu, tija pamoja na kuleta usawa katika mgawanyo wa rasilimali. Ili matarajio hayo yaweze kufikiwa, ni muhimu kuwepo kwa Katiba madhubuti na jumuishi kwa lengo la kuhakikisha ulinganifu wa sera, ufanisi wa taasisi, ushiriki wa wananchi, mifumo thabiti ya udhibiti na usimamizi na Serikali za Mitaa zinazojisimamia. Kwa msingi huo, Mpango huu utajielekeza katika: kuimarisha mifumo ya taasisi na utawala wa kidemokrasia; kuboresha mifumo ya Serikali za Mitaa; kuendeleza utawala wa kidijitali na usimamizi mahiri wa takwimu; na kueneza mabadiliko ya fikra ili kuchochea mageuzi na kwa ajili ya maendeleo endelevu ya taifa.

30. Utekelezaji wa bajeti na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27 unajenga msingi wa utekelezaji wa FYDP IV ili kufikia malengo ya Dira 2050 ikiwemo utekelezaji wa programu na miradi ya kimkakati ambayo haikukamilika wakati wa utekelezaji wa FYDP III ili kuandaa mazingira endelevu ya utekelezaji wa mipango inayofuata katika mfululizo wa mipango mitano ya mwaka mmoja inayotekeleza FYDP IV. Aidha, programu na miradi itakayotekelezwa katika muda wa kati ni ile yenye matokeo ya haraka na inayojenga msingi wa mageuzi ya kiuchumi na kuboresha mifumo ya usimamizi na uendeshaji wa uchumi.

2.3 Shabaha na Misingi ya Uchumi Jumla

2.3.1 Shabaha za Uchumi Jumla katika Muda wa Kati

31. Shabaha na malengo ya uchumi jumla ni kama ifuatavyo:

(i) Pato halisi la Taifa linakadiriwa kukua kwa asilimia 5.9 mwaka 2025 na kuongezeka hadi asilimia 6.3 mwaka 2026 na asilimia 6.9 katika kipindi cha muda wa kati;

(ii) Mfumuko wa bei kuwa kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya 3.0 - 5.0 katika muda wa kati;
(iii) Mapato ya ndani kufikia asilimia 17.1 ya Pato la Taifa mwaka 2026/27 na wastani wa asilimia 17.2 katika kipindi cha muda wa kati;
(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 13.7 ya Pato la Taifa mwaka 2026/27 na wastani wa asilimia 13.7 katika kipindi cha muda wa kati;
(v) Kuhakikisha misamaha ya kodi haizidi asilimia moja (1) ya Pato la Taifa;
(vi) Kuwa na nakisi ya bajeti isiyozidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa; na
(vii) Akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

2.3.2 Misingi ya Uchumi Jumla

32. Shabaha za uchumi jumla katika kipindi cha muda wa kati zimezingatia misingi (*assumptions*) ifuatayo:

(i) Sera, sheria, kanuni na taratibu za usimamizi na uendeshaji wa uchumi kuboreshwa na kuzingatiwa;
(ii) Mkakati wa Ukusanyaji Mapato wa Muda wa Kati (Medium Term Revenue Mobilization Strategy), 2025/26 - 2027/28 kutekelezwa kwa ufanisi;
(iii) Kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za uwekezaji na biashara;
(iv) Kuendelea kuhimili athari za majanga ya asili na yasiyo ya asili ikiwemo ukame, tetemeko la ardhi, magonjwa ya mlipuko na mafuriko;
(v) Kuendelea kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya fedha na bidhaa;
(vi) Kuendelea kuimarika kwa ushirikiano wa kikanda na kimataifa;
(vii) Kuendelea kuimarika kwa upatikanaji na usalama wa chakula nchini; na
(viii) Uwepo wa amani, usalama, umoja na utulivu wa ndani na nchi jirani.

2.4 Makadirio ya Bajeti ya Serikali katika Muda wa Kati

33. Katika kipindi cha muda wa kati, Serikali inatarajia kukusanya na kutumia shilingi bilioni 204,087.7, sawa na wastani wa shilingi bilioni 68,029.2 kwa mwaka ili kugharamia utekelezaji wa mpango na bajeti. Aidha, mwaka 2026/27, bajeti ya Serikali inakadiriwa kuwa shilingi bilioni 61,934.2.

2.4.1 Mapato

34. Katika kipindi cha muda wa kati, mapato ikijumuisha misaada yanakadiriwa kuwa wastani wa shilingi bilioni 52,480.8, sawa na ukuaji wa wastani wa asilimia 12.1. Mwaka 2026/27, mapato yanakadiriwa kuwa shilingi bilioni 46,691.3 ambapo mapato ya kodi ni shilingi bilioni 36,889.3, mapato mengine ni shilingi bilioni 9,238.8 (ikiwemo mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya shilingi bilioni 1,966.2) na misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo shilingi bilioni 563.1. Aidha, makadirio ya mapato ya ndani (kodi na mengine) ni sawa na asilimia 74.5 ya bajeti ya mwaka 2026/27.

35. Misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo inatarajiwa kuwa shilingi bilioni 563.1 mwaka 2026/27, sawa na asilimia 0.9 ya bajeti na kufikia shilingi bilioni 486.0 mwaka 2028/29, sawa na asilimia 0.7 ya bajeti. Mchanganuo wa mapato kwa muda wa kati ni kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 2.1**.

Kielelezo Na 2.1: Mchanganuo wa Mapato katika Kipindi cha Muda wa Kati

(Shilingi bilioni)



2.4.1.1 Mikakati ya Ukusanyaji wa Mapato

36. Katika kipindi cha muda wa kati, Serikali itaendelea kutekeleza mikakati inayolenga kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kupunguza utegemezi wa kibajeti na kuongeza uwezo wa Serikali kugharamia programu na miradi ya maendeleo pamoja na kuboresha huduma za jamii. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali itaendelea kutekeleza mikakati ifuatayo:

(i) Kuimarisha urasimishaji wa sekta isiyo rasmi kupitia huduma za elimu na uwezeshaji zitolewazo katika *"Dawati la Kuwezesha Biashara"* nchini;

(ii) Kuhamasisha ulipaji kodi wa hiari nchini kwa kuimarisha mahusiano baina ya Serikali na walipakodi kupitia majadiliano kwenye majukwaa mbalimbali ikiwemo Baraza la Taifa la Biashara na *CEOs Round Table*;

(iii) Kuendelea kusimamia na kuhimiza matumizi sahihi ya mashine za kutolea risiti za kielektroniki (EFD) kupitia utoaji wa elimu na uendeshaji wa programu mbalimbali za hamasa;

(iv) Kuendelea kujenga na kuboresha mifumo ya TEHAMA ya usimamizi na ukusanyaji wa mapato ili kuhakikisha mifumo hiyo inaunganishwa na mifumo ya taasisi nyingine za umma kwa lengo la kupata taarifa za wafanyabiashara ambao hawajasajiliwa katika mifumo na wale waliosajiliwa wanalipa mapato yao stahiki;

(v) Kuendelea kuhamasisha matumizi ya njia za kibenki/kielektroniki kwenye kufanya malipo mbalimbali kupitia utoaji wa vivutio mbalimbali na ukusanyaji wa mapato;

(vi) Kuongeza kasi ya kupanga, kupima, kumilikisha na kurasimisha ardhi kwa

kuweka msisitizo katika kutambua vipande vya ardhi nchini ili kuongeza wigo wa mapato; na

(vii) Kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi ikiwemo ufuatiliaji wa karibu wa mashirika ya umma ili kuhakikisha yanaongeza tija, gawio na michango stahiki inawasilishwa kwa wakati katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

2.4.2 Matumizi

37. Katika kipindi cha muda wa kati, matumizi (bila kujumuisha malipo ya mtaji wa deni la Serikali) yanakadiriwa kuwa wastani wa shilingi bilioni 59,250.1, sawa na ukuaji wa wastani wa asilimia 9.7. Mwaka 2026/27, matumizi yanakadiriwa kuwa shilingi bilioni 54,098.6 bila kujumuisha malipo ya mtaji wa deni la Serikali ikilinganishwa na shilingi bilioni 48,775.0 ya mwaka 2025/26, sawa na ongezeko la asilimia 10.9. Kati ya matumizi hayo, stahiki za watumishi ikijumuisha michango ya pensheni shilingi bilioni 9,685.7; malipo ya riba shilingi bilioni 7,257.9; na ruzuku kwa baadhi ya taasisi za Serikali, mashirika ya umma na Mamlaka za Serikali za Mitaa shilingi bilioni 22,909.2. Aidha, ununuzi wa mali zisizo za kifedha (Net Acquisition of Nonfinancial Assets) ikiwemo vifaa vya ofisi, mashine, magari, samani, ujenzi wa majengo na miundombinu shilingi bilioni 3,030.4. Kwa kuzingatia mgawanyo wa matumizi ya kawaida na maendeleo, matumizi ya kawaida ni shilingi bilioni 41,217.1, sawa na asilimia 66.5 na matumizi ya maendeleo ni shilingi bilioni 20,717.1, sawa na asilimia 33.5 ya bajeti ya mwaka 2026/27. Mchanganuo wa makadirio ya matumizi ya Serikali umeanishwa katika **Jedwali Na. 2.1 hadi 2.3**.

2.4.2.1 Mikakati ya Usimamizi wa Matumizi

38. Mikakati ya usimamizi wa matumizi katika kipindi cha muda wa kati itajumuisha yafuatayo:

(i) Kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na matumizi ya mifumo ya TEHAMA ikiwa ni pamoja na kuiunganisha ili iweze kubadilishana taarifa;

(ii) Kutekeleza programu na miradi inayoendelea yenye matokeo ya haraka na inayojenga msingi wa mageuzi ya kiuchumi;

(iii) Kuendelea kuimarisha mifumo ya usimamizi na utendaji kazi katika Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma kwa kuboresha mikataba ya utendaji kazi, miundo ya taasisi na usimamizi wa bodi;

(iv) Kufungamanisha utekelezaji wa miradi na mipango ya maendeleo zenye malengo yanayofanana baina ya sekta ili kuongeza tija ya rasilimali za umma; na

(v) Kuendelea kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini unaozingatia matokeo na uwajibikaji katika utendaji kazi wa Serikali na utekelezaji wa miradi.

2.4.3 Kugharamia Nakisi ya Bajeti

39. Serikali itaendelea kugharamia nakisi ya bajeti kwa kutumia mikopo kutoka vyanzo vya ndani na nje kwa kuzingatia Mkakati wa Muda wa Kati wa Kusimamia Deni la Serikali (2025/26 – 2027/28). Katika kipindi cha muda wa kati, Serikali

inakadiria kukopa wastani wa shilingi bilioni 15,548.5. Aidha, Serikali inatarajia kukopa shilingi bilioni 15,242.9 kwa mwaka 2026/27. Kati ya kiasi hicho, mikopo ya ndani ni shilingi bilioni 6,257.7, mikopo ya nje yenye masharti nafuu shilingi bilioni 6,554.8 na mikopo ya nje yenye masharti ya kibiashara shilingi bilioni 2,430.4. Vilevile, Serikali inakadiria kulipa shilingi bilioni 7,835.6 kwa ajii ya malipo ya mtaji kwa mikopo iliyoiva.

40. Uchambuzi wa awali uliofanywa unaonesha kuwa utekelezaji wa mpango na bajeti ya Serikali unaweza kuathiriwa na mabadiliko ya sera za Washirika wa Maendeleo. Bunge la Umoja wa Ulaya liliazimia kuahirisha utoaji wa fedha za msaada kwa mikataba mipya ambayo Serikali ilitarajia kuingia yenye thamani ya takribani EUR milioni 156, sawa na shilingi bilioni 445.75. Kwa mikataba inayoendelea, Serikali inaweza kukosa misaada ya kibajeti kutoka Umoja wa Ulaya yenye thamani ya takriban EUR milioni 39.20, sawa na shilingi bilioni 113.8 kwa mwaka 2025/26 na shilingi bilioni 27.2 kwa mwaka 2026/27. Nchi nyingine iliyotoa tamko la kusitisha misaada ni Sweden ambapo imesitisha kutoa SEK 119,552,997, sawa na shilingi bilioni 31 kwa ajili ya programu ya elimu ya EpforR kwa mwaka wa fedha 2025/26. Hivyo, Serikali itaendelea kuwianisha mapato na matumizi huku ikihakikisha mahitaji ya msingi yanagharamiwa ikiwepo mishahara, deni la Serikali na huduma za jamii.

Jedwali Na 2.1: Makadirio ya Bajeti katika Muda wa Kati (2026/27 -2028/29)

	2025/26	2026/27	2027/28	2028/29
	Bajeti Iliyoidhinishwa	**Bajeti Inayopendekezwa**	**Maoteo**	**Maoteo**
A: Mapato	**41,536,016**	**46,691,299**	**52,360,781**	**58,390,269**
Mapato ya kodi	**32,306,123**	**36,889,320**	**41,393,268**	**46,260,777**
Misaada/Michango	**1,069,884**	**563,139**	**516,459**	**486,219**
Mapato mengine	**8,160,009**	**9,238,839**	**10,451,054**	**11,643,273**
o/w Mamlaka za Serikali za Mitaa	1,680,507	1,966,193	2,300,446	2,691,522
B: Matumizi	**45,994,829**	**51,068,233**	**56,087,146**	**60,965,872**
Mishahara na stahiki za watumishi	**7,711,867**	**9,685,742**	**11,530,985**	**13,293,402**
o/w Mishahara kwa watumishi wa Serikali Kuu	4,754,850	5,124,212	5,380,423	5,660,205
Michango ya hifadhi za jamii	2,240,141	2,569,421	2,619,818	2,824,843
Gharama za bidhaa na huduma	**7,812,245**	**8,202,857**	**8,613,000**	**9,043,650**
o/w Malipo ya madeni ya watumishi, wazabuni	700,000	550,000	500,000	500,000
Malipo ya riba	**6,493,715**	**7,257,876**	**8,019,853**	**8,208,854**
Malipo ya riba nje	2,796,427	3,000,302	3,402,605	3,501,541
Malipo ya riba ndani kwa taasisi zisizo Serikali Kuu	3,697,288	4,257,574	4,617,247	4,707,312
Ruzuku kwenye taasisi za uwekezaji	**1,936,023**	**1,923,246**	**1,888,215**	**1,854,057**
Kwa mashirikia ya umma	1,889,293	1,874,179	1,836,695	1,799,961
Kwa sekta nyingine	46,730	49,067	51,520	54,096
Ruzuku na michango	**21,107,935**	**23,018,817**	**25,006,413**	**27,485,795**
Kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa	9,703,349	10,412,288	11,356,726	12,419,809
o/w Mishahara ya watumishi	6,162,616	6,470,747	6,794,284	7,133,998
Ununuzi wa samani na uwekezaji	1,793,891	1,883,585	1,977,764	2,076,653
Kwa taasisi za umma	11,404,586	12,496,950	13,303,436	14,463,854
o/w Mishahara ya watumishi	2,183,984	2,293,183	2,407,842	2,528,234
Ununuzi wa samani na uwekezaji	6,819,691	7,160,676	7,518,710	7,894,645
Mafao na misaada ya kijamii	**752,516**	**790,141**	**829,649**	**871,131**
Misaada ya huduma za jamii	10,473	10,997	11,547	12,124
Mafao na viinua mgongo	742,042	779,144	818,102	859,007
Gharama nyingine	**180,528**	**189,554**	**199,032**	**208,984**
C: Uwekezaji katika mali zisizo za kifedha	**2,780,160**	**3,030,375**	**3,203,774**	**3,394,826**
Gharama za majengo, miundombinu, mashine n.k	2,666,037	2,905,980	3,073,160	3,257,681
Mali zisizozalishwa/mali za asili	114,123	124,394	130,614	137,145
Nakisi ya Bajeti bila Misaada	**(8,308,858)**	**(7,970,449)**	**(7,446,598)**	**(6,456,648)**
Nakisi ya bajeti ikijumuisha misaada	**(7,238,973)**	**(7,407,309)**	**(6,930,140)**	**(5,970,429)**
Ugharamiaji wa nakisi ya bajeti	7,238,973	7,407,309	6,930,140	5,970,429
Mikopo halisi	**7,238,973**	**7,407,309**	**6,930,140**	**5,970,429**
D: Mikopo ya ndani	**2,952,630**	**2,972,349**	**3,657,039**	**3,074,928**
D1 - Mikopo ya ndani	6,278,186	6,257,744	7,681,816	6,723,935
D2 - Malipo ya mikopo ya ndani	(3,325,557)	(3,285,395)	(4,024,778)	(3,649,007)
E: Mikopo ya nje	**4,286,343**	**4,434,960**	**3,273,101**	**2,895,501**
E1 - Mikopo ya nje	8,676,050	8,985,150	9,118,969	7,877,782
o/w Mikopo ya Kibiashara	2,629,012	2,430,372	3,126,936	2,923,829
E2 - Malipo ya mikopo ya nje	(4,389,707)	(4,550,190)	(5,845,868)	(4,982,281)
Jumla ya Bajeti (A + D1 + E1) AU (B-D2-E2)	**56,490,252**	**61,934,193**	**69,161,566**	**72,991,986**
Nakisi ya bajeti/Pato la Taifa	**-3.0%**	**-2.7%**	**-2.3%**	**-1.8%**
Memo Items				
Pato la Taifa	244,541,773	270,105,797	301,844,771	336,385,606

Chanzo: Wizara ya Fedha

Jedwali Na 2.2: Uwiano wa Makadirio ya Bajeti kwa Pato la Taifa (2025/26 - 2028/29)

	2025/26	2026/27	2027/28	2028/29
	Bajeti Iliyoidhinishwa	Bajeti Inayopendekezwa	Maoteo	Maoteo
A: Mapato	17.0%	17.3%	17.3%	17.4%
Mapato ya kodi	13.2%	13.7%	13.7%	13.8%
Misaada/Michango	0.4%	0.2%	0.2%	0.1%
Mapato mengine	3.3%	3.4%	3.5%	3.5%
o/w Mamlaka za Serikali za Mitaa	0.7%	0.7%	0.8%	0.8%
B: Matumizi	18.8%	18.9%	18.6%	18.1%
Mishahara na stahiki za watumishi	3.2%	3.6%	3.8%	4.0%
o/w Mishahara kwa watumishi wa Serikali Kuu	1.9%	1.9%	1.8%	1.7%
Michango ya hifadhi za jamii	0.9%	1.0%	0.9%	0.8%
Gharama za bidhaa na huduma	3.2%	3.0%	2.9%	2.7%
o/w Malipo ya madeni ya watumishi, wazabuni	0.3%	0.2%	0.2%	0.1%
Malipo ya riba	2.7%	2.7%	2.7%	2.4%
Malipo ya riba nje	1.1%	1.1%	1.1%	1.0%
Malipo ya riba ndani kwa taasisi zisizo Serikali Kuu	1.5%	1.6%	1.5%	1.4%
Ruzuku kwenye taasisi za uwekezaji	0.8%	0.7%	0.6%	0.6%
Kwa mashirikia ya umma	0.8%	0.7%	0.6%	0.5%
Kwa sekta nyingine	0.0%	0.0%	0.0%	0.0%
Ruzuku na michango	8.6%	8.5%	8.3%	8.2%
Kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa	4.0%	3.9%	3.8%	3.7%
o/w Mishahara ya watumishi	2.5%	2.4%	2.3%	2.1%
Ununuzi wa samani na uwekezaji	0.7%	0.7%	0.7%	0.6%
Kwa taasisi za umma	4.7%	4.6%	4.4%	4.3%
o/w Mishahara ya watumishi	0.9%	0.8%	0.8%	0.8%
Ununuzi wa samani na uwekezaji	2.8%	2.7%	2.5%	2.3%
Mafao na misaada ya kijamii	0.3%	0.3%	0.3%	0.3%
Misaada ya huduma za jamii	0.0%	0.0%	0.0%	0.0%
Mafao na viinua mgongo	0.3%	0.3%	0.3%	0.3%
Gharama nyingine	0.1%	0.1%	0.1%	0.1%
C: Uwekezaji katika mali zisizo za kifedha	1.1%	1.1%	1.1%	1.0%
najengo, miundombinu, mashine n.k	1.1%	1.1%	1.0%	1.0%
Mali zisizozalishwa/mali za asili	0.0%	0.0%	0.0%	0.0%
Nakisi ya Bajeti bila Misaada	-3.4%	-3.0%	-2.5%	-1.9%
Nakisi ya bajeti ikijumuisha misaada	-3.0%	-2.7%	-2.3%	-1.8%
Ugharamiaji wa nakisi ya bajeti	3.0%	2.7%	2.3%	1.8%
Mikopo halisi	3.0%	2.7%	2.3%	1.8%
D: Mikopo ya ndani	1.2%	1.1%	1.2%	0.9%
D1 - Mikopo ya ndani	2.6%	2.3%	2.5%	2.0%
D2 - Malipo ya mikopo ya ndani	-1.4%	-1.2%	-1.3%	-1.1%
E: Mikopo ya nje	1.8%	1.6%	1.1%	0.9%
E1 - Mikopo ya nje	3.5%	3.3%	3.0%	2.3%
E2 - Malipo ya mikopo ya nje	-1.8%	-1.7%	-1.9%	-1.5%
Jumla ya Bajeti (A + D1 + E1) AU (B-D2-E2)	23.1%	22.9%	22.9%	21.7%
Nakisi ya bajeti/Pato la Taifa	-3.0%	-2.7%	-2.3%	-1.8%

Chanzo: Wizara ya Fedha

Jedwali Na 2.3: Mgawanyo wa Bajeti Kisekta Katika Muda wa Kati (2025/26 - 2028/29)

Shilingi Bilioni

SEKTA	NAMBA YA SEKTA	2025/26 BAJETI ILIYOIDHINISHWA	2026/27 MAKADIRIO YA BAJETI	2027/28 MAKADIRIO YA BAJETI	2028/29 MAKADIRIO YA BAJETI
1 - Elimu	**709**	**7,394.4**	**8,191.8**	**8,935.2**	**9,720.5**
1.1 - Elimu Msingi	7091,7092	5,218.8	5,781.6	6,306.2	6,860.5
1.2 - Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi	7,093	354.4	392.7	428.3	465.9
1.3 - Elimu ya Juu	7,094	1,569.4	1,738.6	1,896.4	2,063.1
1.4 - Sayansi, Teknolojia na Ubunifu	7,098	83.1	92.1	100.5	109.3
1.5 - Huduma za Utawala	7,098	168.6	186.8	203.8	221.7
2 - Afya	**707**	**3,009.2**	**3,333.6**	**3,636.1**	**3,955.7**
2.1 - Huduma za Tiba	71,7072,7073,7074,7075,7076	1,426.9	1,580.7	1,724.1	1,875.6
2.2 - Huduma za Kinga	7071,7073,7074,7076	369.0	408.8	445.9	485.1
2.3 - Zahanati	7071,7072,7073,7074,7075	50.8	56.3	61.4	66.8
2.4 - Vituo vya Afya	7071,7072,7073,7074,7075	69.5	76.9	83.9	91.3
2.5- Hospitali za Wilaya	7071,7072,7073,7074,7075	980.4	1,086.2	1,184.8	1,288.9
2.6 - Huduma za Utawala	7,076	112.6	124.7	136.0	148.0
3 - Huduma za Utawala na Deni la Serikali	**701**	**16,802.0**	**18,677.8**	**20,476.0**	**21,759.8**
3.1 - Utawala na Bunge	7,011	6,239.5	6,912.3	7,539.5	8,202.2
3.2 - Usimamizi wa mapato na Matumizi	7,011	3,728.6	4,130.7	4,505.5	4,901.5
3.3 - Mambo ya Nje na Ushirikano wa Kimataifa	7,011	340.2	376.9	411.1	447.2
3.4 - Deni la Serikali (Malipo ya Riba)	7,018	6,493.7	7,257.9	8,019.9	8,208.9
4 - Ulinzi, Utawala wa Sheria na Usalama	**703**	**6,398.1**	**7,088.0**	**7,731.1**	**8,410.7**
4.1 - Ulinzi	702	3,642.7	4,035.5	4,401.7	4,788.6
4.2 - Usalama wa Umma	7,036	2,066.6	2,289.4	2,497.1	2,716.6
4.3 - Mahakama	7,033	688.8	763.1	832.3	905.5
5 - Maendeleo ya Uchumi	**704**	**10,235.9**	**11,339.7**	**12,478.8**	**14,026.0**
5.1 - Kilimo	7,042	1,925.8	2,133.5	2,327.1	2,531.6
5.2 - Madini	7,044	225.0	249.2	271.8	295.7
5.3 - Nishati	7,043	1,965.7	2,177.6	2,375.2	2,584.0
5.4 - Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano	7045, 7046	5,524.2	6,119.9	6,785.3	7,832.0
5.5 - Maliasili, Utalii na Mazingira	7,049	317.4	351.6	383.5	417.2
5.6 - Viwanda	7,047	132.4	146.7	160.0	174.1
5.7 - Biashara	7,047	107.0	118.6	129.4	140.8
5.8 - Kazi, Maendeleo ya Vijana na Kukuza Ujuzi	7,041	38.4	42.6	46.5	50.6
6 - Hifadhi ya Jamii	**710**	**3,154.1**	**3,494.2**	**3,811.3**	**4,146.3**
6.1 - Wazee, Watoto na Watu wenye Ulemavu	7101,7102	73.5	81.4	88.8	96.6
6.2 - Mifuko ya Hifadhi ya Jamii	7,109	2,629.0	2,912.5	3,176.8	3,456.0
6.3 - Mfuko wa Bima wa Afya	7,109	451.6	500.3	545.7	593.7
7 - Maji, Makazi na Maendeleo ya Jamii	**706**	**1,781.2**	**1,973.4**	**2,152.5**	**2,341.7**
7.1 - Maji	7,063	898.1	995.0	1,085.3	1,180.7
7.2 - Ardhi, Nyumba na Makazi ya Watu	7,065	166.9	185.0	201.8	219.5
7.3 - Maendeleo ya Jamii	7,062	196.5	217.7	237.5	258.4
7.4 - Habari, Michezo na Utamaduni	7,081	519.6	575.7	627.9	683.1
Jumla ya Sekta		**48,775.0**	**54,098.5**	**59,220.9**	**64,360.7**
Deni la Serikali (Ulipaji wa Mtaji)		7,715.3	7,835.6	9,940.6	8,631.3
Jumla Kuu		**56,490.3**	**61,934.1**	**69,161.6**	**72,992.0**

Chanzo: Wizara ya Fedha

SURA YA TATU

USIMAMIZI WA VIHATARISHI VYA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI

3.1. Utangulizi

41. Sura hii inaelezea vihatarishi vinavyoweza kujitokeza katika utekelezaji wa mpango na bajeti katika muda wa kati na kuathiri malengo ya mpango ikiwemo ukusanyaji wa mapato na matumizi. Vihatarishi hivyo vimegawanyika katika makundi mawili ambayo ni vihatarishi vya uchumi jumla na vihatarishi mahsusi.

3.2. Vihatarishi vya Uchumi Jumla

42. Vihatarishi vya uchumi jumla vinaweza kutokea kutokana na sababu za asili na zisizo za asili za ndani na nje ya nchi. Baadhi ya vihatarishi vinavyoweza kuathiri viashiria vya uchumi jumla ni pamoja na mabadiliko ya viwango vya riba za mikopo, mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma, kushuka kwa thamani ya shilingi pamoja na mabadiliko ya sera za nje.

(i) **Mabadiliko ya Viwango vya Riba za Mikopo**

43. Viwango vya riba katika soko la fedha hupangwa kulingana na nguvu ya uhitaji na ugavi wa huduma za fedha, hususan mikopo. Kuongezeka kwa uhitaji wa mikopo ikilinganishwa na ugavi husababisha ongezeko la viwango vya riba katika sekta ya fedha. Ongezeko la viwango vya riba huongeza gharama za mikopo kwa sekta ya umma na sekta binafsi, kupungua kwa uwezo wa taasisi katika utekelezaji wa miradi na huduma kwa jamii, kuongezeka kwa gharama za uzalishaji na ugavi wa bidhaa na huduma, kuongezeka kwa gharama za urejeshaji wa mikopo iliyoiva, kupungua kwa kasi ya uwekezaji katika sekta ya umma na binafsi, kuchochea mfumuko wa bei ya bidhaa na huduma, kupungua kwa mapato binafsi, mashirika, kampuni na serikali, na kupungua kwa bei ya hisa katika soko la hisa. Athari hizi kwa pamoja zinaweza kusababisha mtikisiko wa hali ya kiuchumi, hususan kupungua kwa kasi ya ukuaji wa Pato la Taifa.

44. Hatua za kukabiliana na kihatarishi hiki ni pamoja na: Kuendelea kutekeleza na kusimamia kwa uthabiti sera ya fedha na bajeti ili kufikia malengo na shabaha za uchumi jumla; kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara ili kuvutia mitaji kutoka nje; kuendeleza soko la ndani la fedha; kuongeza ufanisi katika uzalishaji wa bidhaa na huduma za ndani; na kuimarisha usimamizi wa Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, SURA 134 na Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo wa mwaka 2017/18-2029/30.

(ii) **Mabadiliko ya Bei za Bidhaa**

45. Kushuka kwa bei za bidhaa kwenye soko la dunia, hususan madini na mazao ya kilimo ni matokeo ya tofauti ya nguvu ya uhitaji na ugavi wa bidhaa. Hali hii inaweza kutokea kutokana na matukio ya kivita, ukame, mafuriko, milipuko ya

magonjwa, na migogoro wa kibiashara na kisiasa. Kushuka kwa bei ya bidhaa kunaweza kupunguza mapato yatokanayo na mauzo nje ya nchi na kuathiri uzalishaji wa mazao husika hapa nchini. Aidha, kupanda kwa bei za bidhaa muhimu katika soko la dunia, hususan bidhaa za petroli na mbolea kunaweza kuongeza matumizi ya fedha za kigeni katika kugharamia bidhaa hizo, kuongeza gharama za uzalishaji na ugavi wa bidhaa mbalimbali na uendeshaji wa shughuli za serikali. Vilevile, hali hii itapunguza kasi ya uzalishaji wa mazao, kuongeza nakisi ya bajeti, upungufu wa fedha za kigeni, na kuongeza mfumuko wa bei nchini.

Hatua za kukabaliana na vihatarishi vya mabadiliko ya bei za bidhaa ni pamoja na kuimarisha Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo, kuendelea kuwekeza kwenye uzalishaji wa nishati mbadala wa petroli kama vile gesi na umeme ili kupunguza athari za kupanda kwa bei ya bidhaa za petroli katika soko la dunia na kuwekeza kwenye miradi ya umwagiliaji na uhifadhi wa vyanzo vya maji na mazingira ili kuhakikisha shughuli za kilimo zinafanyika vipindi vyote vya mwaka. Pia, kuwekeza kwenye kilimo cha kisasa, mbegu bora zinazohimili mabadiliko ya tabianchi na teknolojia za kuhifadhi chakula, na kuongezea thamani za bidhaa.

(iii) **Kushuka kwa Thamani ya Shilingi ya Tanzania**

46. Thamani ya shilingi dhidi ya fedha za kigeni inategemea mzunguko wa fedha za kigeni, mizania ya biashara, sera za fedha na matarajio ya wawekezaji. Kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania kunaweza kuathiri utekelezaji wa bajeti kwa kuongeza matumizi hususan ugharamiaji wa deni la serikali la nje na ununuzi na usafirishaji wa bidhaa na huduma kutoka nje.

Hatua za kukabiliana na kihatarishi hiki ni kuendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kuimarisha Upatikanaji wa fedha za Kigeni, kuimarisha mifumo ya usimamizi wa sekta zinazochangia upatikanaji wa fedha za kigeni ikiwemo utalii, madini na kilimo, kuimarisha mifumo rasmi ya mauzo ya bidhaa na huduma nje, na kupunguza vikwazo vya kibiashara mipakani.

(iv) **Mabadiliko ya Sera za Nchi Wahisani**

47. Mabadiliko ya sera za nchi wahisani hutokea kutokana na mdororo wa shughuli za kiuchumi pamoja na mabadiliko ya uongozi wa kisiasa na mifumo ya uzalishaji wa bidhaa na huduma. Aidha, mabadiliko ya sera za nchi wahisani yanaweza kuathiri upatikanaji wa fedha za kigeni, misaada na mikopo inayotegemewa katika utekelezaji wa mpango na bajeti. Hali hii inaweza kuathiri uhusiano wa kidiplomasia, utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo, biashara, uwekezaji, utoaji wa huduma za kijamii, na ukuaji wa uchumi.

Hatua za kukabiliana na kihatarishi hiki ni pamoja na: Kupanua wigo wa vyanzo vya mapato ya ndani; kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya ndani; kuimarisha shughuli za utafiti na ubunifu; kuimarisha mahusiano ya kidiplomasia kwa kusimamia

utekelezaji wa Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo wa mwaka 2017/18-2029/30 na Sera ya Mambo ya Nje ya 2021 (Toleo la mwaka 2024).

3.3. Vihatarishi Mahsusi

48. Vihatarishi mahsusi ni pamoja na madeni sanjari, mabadiliko ya tabianchi na majanga, migogoro ya kisiasa na mahusiano ya kidiplomasia na shambulio la mifumo ya TEHAMA.

(i) **Madeni Sanjari**

49. Madeni sanjari hutokea pale ambapo Serikali na taasisi zake hazijatekeleza ipasavyo mikataba baina yake na wadau mbalimbali ikiwemo sekta binafsi. Kushindwa kutekeleza matakwa ya mikataba kunaweza kusababisha Serikali kugharamia malipo ya fidia na madai yatokanayo na amri za mahakama pamoja na taasisi za usuluhishi wa migogoro ya kibiashara. Aidha, Serikali inaweza ikabeba vihatarishi vya miradi inayotekelezwa kwa utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi iwapo itashindwa kutekeleza kikamilifu mikataba hiyo. Mazingira hayo yakijitokeza yanaweza kusababisha ongezeko la mzigo wa kibajeti kwa ajili ya kugharamia madai na deni la Serikali, hivyo kupunguza uwezo wa Serikali kugharamia mahitaji mengine hususan miradi ya maendeleo na uendeshaji wa shughuli za kawaida.

Hatua za kukabiliana na vihatarishi vya madeni sanjari ni pamoja na kuimarisha usimamizi wa Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana, Sura 134 na Sheria ya Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Sura 103, kuimarisha mifumo na taasisi za usimamizi wa mikataba, kuendelea kujenga uwezo katika usimamizi wa mikataba, na kuongeza uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa mikataba.

(ii) **Mabadiliko ya Tabianchi na Majanga**

50. Mabadiliko ya tabianchi na majanga yanasababishwa na shughuli za kibinadamu na mifumo asili ya mazingira. Majanga yanayoweza kujitokeza ni kama vile tetemeko la ardhi, mlipuko wa volkano, mlipuko wa magonjwa, baa la njaa, ukame, wadudu waharibifu wa mazao, matukio ya moto na maporomoko ya ardhi. Aidha, mabadiliko ya tabianchi yanaweza kusababisha mafuriko, uhaba wa mvua, vimbunga na kuongezeka kwa kiwango cha joto. Kutokea kwa mabadiliko ya tabianchi na majanga kunaweza kusababisha vifo, kudorora kwa shughuli za uchumi, uharibifu wa miundombinu, mali na mifumo ya ikolojia. Hivyo, Serikali itahitaji bajeti ya dharura kwa ajili ya kutoa msaada kwa wahanga na urejeshaji wa miundombinu iliyoharibika.

Hatua za kukabiliana na vihatarishi hivi ni pamoja na: Kuimarisha Mfuko wa Dharura wa Taifa; kuendelea kutekeleza Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022-2032); kuendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa 2022 – 2027; kuimarisha mfumo wa uandaaji wa miradi kwa kuzingatia Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma pamoja na maboresho

yake kuhusu mabadiliko ya tabianchi na mazingira; na Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati safi ya Kupikia (2024 – 2034). Hatua nyingine ni kuendelea kuwekeza katika miradi ya uhifadhi wa vyanzo vya maji na mazingira, ujenzi wa mabwawa makubwa ya kuhifadhi maji ya mvua, miradi ya umwagiliaji, matumizi ya mbegu bora zinazohimili mabadiliko ya tabianchi na wadudu waharibifu na teknolojia za kuhifadhi chakula.

(iii) **Migogoro ya Kisiasa na Mahusiano ya Kidiplomasia**

51. Migogoro ya kisiasa na mahusiano duni ya kidiplomasia ni matokeo ya mambo mbalimbali ikiwemo ushindani usio sawa wa kibiashara; ukiukaji wa misingi ya utawala bora na utawala wa sheria; ukosefu wa rasilimali; uchu wa madaraka; ukosefu wa ajira; na mabadiliko ya kisera na itikadi za kisiasa. Migogoro ya kisiasa ya ndani na nje ya nchi pamoja na kutetereka kwa mahusiano ya kidiplomasia kunaweza kuvuruga au kudumaza shughuli za kiuchumi na kijamii, na hivyo kuathiri upatikanaji wa mapato ya Serikali, kampuni, mashirika na watu binafsi; kupungua kwa misaada, mikopo na uwekezaji kutoka nje; kuvurugika kwa mnyororo wa uzalishaji, uhitaji na ugavi wa mazao, bidhaa na huduma; na kuongezeka kwa mahitaji ya ziada ya ulinzi na usalama.

Hatua za kukabiliana na vihatarishi hivyo ni pamoja na kuendelea kuimarisha mifumo ya utawala bora na utawala wa sheria; kuimarisha mifumo na taasisi za usimamizi wa ushindani wa kibiashara; kudumisha na kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa kupitia mikataba ya ushirikiano na kidiplomasia; kuzalisha ajira stahiki na zenye staha; kuendelea kusimamia utekelezaji wa Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo wa mwaka 2017/18-2029/30 pamoja na Sera ya Mambo ya Nje ya 2021 (Toleo la mwaka 2024).

(iv) **Shambulio la Mifumo ya TEHAMA**

52. Shambulio la mifumo linasababishwa na tabia ovu ya baadhi ya watu na taasisi, tamaa, ukiukwaji wa misingi ya utawala bora na utawala wa sheria, ukosefu wa ajira, na kasi ya mabadiliko ya teknolojia. Shambulio la mifumo ya TEHAMA linaweza kusababisha hasara za kifedha kutokana na uchepushaji wa mapato na matumizi ya serikali na kuathiri utekelezaji wa bajeti. Aidha, shambulio la mifumo linaweza kudhoofisha upatikanaji wa huduma, uvujaji wa taarifa na kuchafua taswira ya Serikali.

Hatua za kukabiliana na kihatarishi hiki ni pamoja na: Kuimarisha misingi ya utawala bora na utawala wa sheria; kuimarisha misingi ya uadilifu katika jamii; kuendelea kujenga uwezo na kuimarisha usalama wa mtandao wa Serikali; kutoa mafunzo endelevu kwa watumishi wa umma kuhusu utambuzi na namna ya kukabiliana na mashambulizi ya mtandao; kuongeza kasi ya uzalishaji wa ajira; utekelezaji wa Sheria ya Makosa ya Mtandao ya 2015; utekelezaji wa Sheria ya Miamala ya Kielektroniki ya 2015 na Sheria ya Serikali Mtandao ya 2019. Hatua nyingine ni pamoja na utekelezaji

wa Mkakati wa Taifa wa Usalama wa Mtandao 2024 – 2029 na Mkakati wa Ulinzi wa Kimtandao Serikalini wa Mwaka 2022–2027.

(v) **Kihatarishi cha Kiutendaji**

53. Ufanisi mdogo katika utekelezaji wa mpango na bajeti ni kihatarishi cha kiutendaji (operational risk) kinachojitokeza pale ambapo taasisi au serikali inashindwa kutekeleza shughuli zilizopangwa kwa wakati, kwa ubora, na kwa gharama zilizokadiriwa. Hali hii husababishwa na udhaifu wa ndani wa mifumo ya usimamizi, hususan usimamizi wa mikataba, ukosefu wa rasilimali fedha na watu wenye ujuzi, pamoja na uratibu hafifu miongoni mwa taasisi zinazohusika katika utekelezaji wa mpango na bajeti. Aidha, mabadiliko ya mara kwa mara ya kisera na kiutawala, urasimu katika maamuzi, kuweka malengo yasiyoendana na uhalisia, rushwa, na ukosefu wa uwazi na uwajibikaji huongeza uwezekano wa mpango na bajeti kutotekelezwa kwa ufanisi. Matokeo yake ni kuchelewa kwa miradi ya maendeleo, miradi na huduma kukosa thamani halisi ya fedha, kushuka kwa tija ya shughuli za kiuchumi, utegemezi wa kibajeti, na kupungua kwa imani ya wadau kwa taasisi za umma.

Hatua zitakazochukuliwa ni pamoja na kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi kwa kutumia mbinu shirikishi na teknolojia za kidijitali, kujenga uwezo wa watumishi katika usimamizi wa fedha na utendaji, kuimarisha uwazi na uwajibikaji, kushirikisha sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya umma yenye sifa za kibiashara, na kuhakikisha mawanda ya shughuli za umma katika mpango na bajeti yanazingatia uhalisia wa mapato na mazingira ya utekelezaji wake.

SURA YA NNE

MAELEKEZO YA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KATIKA MUDA WA KATI

4.1 Maandalizi ya Mpango na Bajeti

54. Wakati wa maandalizi ya mpango na bajeti, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia misingi, malengo na shabaha za Dira 2050; Mpango Elekezi wa Muda Mrefu 2026 – 2050; Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/27 – 2030/31); Ilani ya Chama Tawala; Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27; mpango mkakati wa taasisi na maagizo yanayotolewa na Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Aidha, Maafisa Masuuli wanapaswa kufungamanisha vipaumbele vya mafungu na taasisi zake ili kufikia shabaha ya pamoja katika matokeo tarajiwa.

4.1.1 Ratiba ya Maandalizi ya Mpango na Bajeti

55. Ratiba ya Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2026/27 ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 4.1**

Jedwali Na. 4.1: Ratiba ya Maandalizi ya Mpango na Bajeti

Mwezi	Shughuli
Agosti 2025 – Januari 2026	Maandalizi na uidhinishwaji wa Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali
Februari 2026	Usambazaji wa Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali pamoja na ukomo wa awali (indicative ceiling) wa bajeti za mafungu.
Februari 2026	Maandalizi ya mipango na bajeti za Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali; Ofisi za Wakuu wa Mikoa; Mamlaka za Serikali za Mitaa; Taasisi na Mashirika ya Umma.
Februari 2026	Kuwasilisha na kuidhinishwa kwa Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu Mapendekezo ya Mfumo na Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2026/27.
Januari - Mei 2026	Kufanya majadiliano kuhusu mapendekezo ya maboresho ya Mfumo wa Kodi.
Februari – Machi 2026	Wizara ya Fedha, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, Tume ya Taifa ya Mipango na Ofisi ya Msajili wa Hazina kufanya uchambuzi wa mipango na bajeti za kisekta na mafungu.
Machi 2026	Kuwasilisha randama kwa Katibu wa Bunge na nakala Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu kabla au ifikapo tarehe 10 Machi kulingana na Kanuni 116(iii)(a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2025.
Machi 2026	Kuwasilisha kwenye Kamati ya Bunge Mapendekezo ya Mfumo na Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2026/27
Machi 2026	Mafungu kuwasilisha mipango na bajeti kwenye Kamati za Kisekta za Bunge

Mwezi	Shughuli
Aprili – Juni 2026	Mafungu kuwasilisha mipango na bajeti bungeni
Juni 2026	Serikali kuwasilisha bungeni Muswada wa Sheria ya Fedha na Sheria ya Matumizi
1 Julai 2026 - 30 Juni 2027	Utekelezaji wa mipango na bajeti kama ilivyoidhinishwa na Bunge pamoja na kufanya ufuatiliaji na tathimini ya utekelezaji

4.1.2 Uingizaji wa Takwimu za Bajeti ya Serikali kwenye Mifumo ya Kibajeti

56. Maafisa Masuuli wote wanaelekezwa kuhakikisha kuwa, uingizaji wa takwimu za bajeti kwenye mifumo ya maandalizi ya bajeti unazingatia masuala muhimu yafuatayo:

(i) Kufungamanisha kwa usahihi shughuli zinazotengewa bajeti na Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/27 – 2030/31) na Ilani ya Chama Tawala;
(ii) Ukomo wa bajeti wa mwaka 2026/27 na makisio yanayoonesha uhalisia kulingana na ukomo wa miaka miwili inayofuata (2027/28 hadi 2028/29);
(iii) Kutumia kwa usahihi namba za miradi, mageresho ya kibajeti (*GFS codes 2014*) na vizio vya vipimo kama vilivyoainishwa kwenye mifumo;
(iv) Kukasimia katika vifungu husika, takwimu za bajeti ya mishahara, matumizi mengineyo na miradi ya maendeleo zinazoingizwa kama *transfers*; na
(v) Miongozo inayotolewa na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (OR – MUUUB) katika uingizaji wa viwango sahihi vya stahili za kisheria kama posho ya pango, samani, simu na umeme.

4.1.3 Uwasilishaji wa Mpango na Bajeti (MTEF)

57. Wakati wa uwasilishaji wa mpango na bajeti, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia yafuatayo:

(i) Muundo wa MTEF uliooneshwa katika **Kiambatisho Na. 1D**;
(ii) Ratiba ya uwasilishaji wa mpango na bajeti kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na.4.1**;
(iii) Wizara, Idara Zinazojitegemea na Ofisi za Wakuu wa Mikoa zinatakiwa kuwasilisha Wizara ya Fedha na Tume ya Taifa ya Mipango nakala tete za makadirio ya mapato na matumizi ya fungu husika, siku tano (5) kabla ya kuanza uchambuzi kwa kuzingatia ratiba ya uchambuzi;
(iv) Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma zinaelekezwa kuwasilisha Ofisi ya Msajili wa Hazina kupitia Mfumo wa PlanRep makadirio ya mapato na matumizi kwa ajili ya uchambuzi kwa kuzingatia ratiba itakayotolewa na Ofisi hiyo kwa mujibu wa Kifungu cha 17A cha Sheria ya Bajeti Sura 439. Aidha, taarifa ya uchambuzi huo iwasilishwe Wizara ya Fedha;
(v) Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia Ofisi za Wakuu wa Mikoa zinaelekezwa kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI kupitia mfumo wa PlanRep kwa kuzingatia ratiba itakayotolewa na Ofisi hiyo.

Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI itawasilisha HAZINA taarifa jumuishi ya fomu namba 3B, 4, 6 na 8B kwa mafungu yote ikiwa katika nakala tete zenye muundo wa *excel* au *access*; na

(vi) Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali na Ofisi za Wakuu wa Mikoa zinaelekezwa kuwasilisha Wizara ya Fedha, Tume ya Taifa ya Mipango na Ofisi ya Waziri Mkuu –TAMISEMI nakala tete zilizofanyiwa marekebisho ndani ya siku tano (5) baada ya bajeti ya fungu husika kuidhinishwa na Bunge.

4.1.4 Uwasilishaji wa Randama

58. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuwasilisha Randama ya Mpango na Bajeti ya mwaka 2026/27 kwa Katibu wa Bunge na nakala Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kabla au ifikapo tarehe 10 Machi, 2026 kwa mujibu wa Kanuni 118 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2025. Aidha, nakala tete ya Randama hiyo iwasilishwe Wizara ya Fedha siku mbili kabla ya Vikao husika. Muundo wa uandaaji wa randama ni kama unavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 1E.**

4.1.5 Maelekezo ya Kimkakati kwa Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa

59. Maelekezo haya yamezingatia malengo ya Dira 2050 na changamoto za utekelezaji wa mpango na bajeti ikiwemo: ukuaji wa uchumi hadi asilimia 10 au zaidi; Pato la Taifa kufikia dola za Marekani trilioni moja ifikapo 2050; wastani wa kipato cha mtu cha dola elfu saba ifikapo 2050; uzalishaji wa ajira zenye staha milioni nane ifikapo 2031; mabadiliko ya sera za washirika wa maendeleo; takribani asimilia 70 ya mapato ya ndani kugharamia huduma za deni la Serikali na mishahara ya watumishi; na kukamilisha utekelezaji wa miradi inayoendelea. Aidha, mapendekezo haya yanalenga kuandaa mazingira na miundombinu rafiki kwa sekta binafsi, ambayo inatarajiwa kuchangia asilimia 70 ya utekelezaji wa Dira 2050 na Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu 2050 kama ifuatavyo:

(i) Maafisa Masuuli wanaosimamia mifuko yenye vyanzo maalumu (TARURA, Mfuko wa Barabara, Mfuko wa Maendeleo ya Reli, Mfuko wa Taifa wa Maji, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, Mfuko wa Utalii na REF) kutenga asilimia tano (5) ya mapato ya mifuko husika kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za msingi za Mfuko kwenye miundombinu ya Maeneo Maalumu ya Kiuchumi (SEZs & EPZs) ili kuvutia uwekezaji na kuongeza fursa za ajira;

(ii) Ofisi za Wakuu wa Mikoa kusimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa kutumia kwa pamoja asilimia tano (5) kati ya asilimia 15 inayopendekezwa ya mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa ajili ya uwekezaji kwenye miradi ya kuboresha mazingira ya biashara na ujasiriamali ili kuvutia na kuongeza fursa za ajira kwa wanufaika;

(iii) Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu kuandaa na kutekeleza mpango wa dharura wa kutokomeza ugonjwa wa malaria ifikapo Desemba 2030 na kuendelea kuratibu utekelezaji wa bima ya afya kwa wote;

(iv) Ofisi ya Msajili wa Hazina kusimamia na kuwezesha mashirika ya umma yanayojiendesha kwa faida kushirikisha umma katika uwekezaji kupitia Soko la Hisa la Dar es Salaam;

(v) Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Mipango kuandaa nyenzo ya upangaji wa pamoja kwa kutumia mfumo wa programu (Programme Based Budgeting) ili kuanza kutumika mwaka 2027/28;

(vi) Tume ya Taifa ya Mipango kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha pamoja na wizara za kisekta zenye miradi inayovutia uwekezaji wa sekta binafsi kuandaa mkakati/nyenzo mahsusi kuwezesha na kurahisisha ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi hiyo;

(vii) Maafisa Masuuli kuzingatia mkakati wa kulinda wawekezaji wa ndani (local content) kwa kutoa kipaumbele cha kwanza katika zabuni, masharti ya mikataba na malipo ya hati za madai pamoja na kuweka msukumo katika *joint venture* kwa mikataba ya kigeni;

(viii) Maafisa Masuuli kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuimarisha uandaaji na usimamizi wa mikataba ili kupunguza, kuondoa na kudhibiti gharama zinazotokana na mashauri ya kimahakama;

(ix) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha kusimamia Maafisa Masuuli kutoingia mikataba bila kuwa na kasma zilizoidhinishwa na Bunge kwa mujibu wa kifungu cha 51 na 45(b) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439;

(x) Maafisa Masuuli kutenga bajeti kwa ajili ya kumalizia miradi inayoendelea na kusitisha mpango wa kuibua miradi mipya isipokuwa inayotekelezwa kwa utaratibu wa PPP;

(xi) Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuwa Serikali haitaruhusu mafungu kuvuka na fedha mwisho wa mwaka badala yake shughuli na miradi ambayo utekelezaji wake haujakamilika zitengewe bajeti katika mwaka wa fedha unaofuata;

(xii) Taasisi na mashirika ya umma hususan mashirika yanayojiendesha kibiashara yaweke mikakati ya kuondokana na utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu ifikapo Juni 2029;

(xiii) Wizara ya Fedha kufanya mageuzi ya kisheria, usimamizi na utawala kwa Benki za maendeleo na biashara nchini ili kuvutia uwekezaji wa mitaji kutoka sekta binafsi ndani na nje ya nchi na kutumia masoko ya fedha kupata mitaji ya kutosha kukidhi mahitaji ya mikopo kwa sekta binafsi kwa lengo la kukuza uchumi;

(xiv) Ofisi ya Msajili wa Hazina isimamie na kuziwezesha taasisi zenye miundombinu, vifaa na vitendea kazi kwa miradi iliyokamilika kuingia ubia na sekta binafsi katika uendeshaji ili kuongeza tija na ufanisi wa taasisi hizo;

(xv) Maafisa Masuuli kuandaa mikakati ya kuzalisha, kulea na kukuza wajasiriamali wadogo, wakati na wakubwa kupitia ushirikishaji katika utekelezaji wa dhana ya wazawa (Local Content) na kuwezesha upatikanaji wa mikopo ya gharama nafuu ili kuwezesha uibuaji wa fursa za ajira hasa kwa vijana;

(xvi) Kujenga uwezo wa Idara za Sera na Mipango pamoja na Vitengo vya Ufuatiliaji na Tathmini katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(xvii) Maafisa Masuuli kuimarisha ushirikishwaji wa taasisi za elimu ya juu na utafiti katika uandaaji wa sera na mipango ya kisekta;

(xviii) Tume ya Taifa ya Mipango kwa kushirikiana na COSTECH kuandaa *repository* ya tafiti zinazofanywa na taasisi za Serikali ili kuwezesha upatikanaji wake kwa ajili ya matumizi katika uandaaji na utekelezaji wa sera na mipango ya Serikali;

(xix) Tume ya Taifa ya Mipango kwa kushirikiana na sekta kuandaa na kusimamia utekelezaji wa vigezo vya upimaji wa ufanisi katika programu na miradi ya maendeleo;

(xx) Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI na Ofisi ya Waziri Mkuu kuandaa mpango wa kuanzisha jukwaa la viongozi (Leaders Club);

(xxi) Ofisi ya Msajili wa Hazina kuratibu na kusimamia mashirika yenye kampuni tanzu kutoa kipaumbele katika utekelezaji wa zabuni za kimkakati za mashirika husika ikiwa ni mkakati wa utekelezaji wa dhana ya mzawa (Local Content);

(xxii) Wizara ya Ardhi kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuandaa na kutekeleza mipango kabambe ya matumizi ya ardhi ili kuwezesha utekelezaji wa mikakati ya kufikia malengo ya Dira 2050;

(xxiii) Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara ya Maliasili na Utalii kuandaa na kutekeleza mpango wa muda mfupi wa kudhibiti ongezeko la makazi shikizi, uvamizi wa shoroba za wanyama pori na maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za kilimo na mifugo;

(xxiv) Wizara ya Fedha kuandaa mkakati wa kulipa na kudhibiti madeni ya huduma zinazotolewa na taasisi za Serikali kwenye Wizara, Idara Zianzojitegemea, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(xxv) Taasisi zinazohusika na uthibiti ubora ziboreshe mifumo ya uthibitishaji na ufuatiliaji wa viwango kwa bidhaa zote hasa bidhaa za kilimo, madini na viwandani, ili zitimize masharti ya ubora na usalama kwa viwango vya ndani na vya kimataifa na kuongeza ushindani wa bidhaa za Tanzania katika masoko ya kimataifa. Aidha, taasisi hizo zidhibiti uingizaji wa bidhaa kutoka nje zilizopo chini ya viwango vya ubora ili kulinda afya za walaji pamoja kuokoa fedha za kigeni zinazotumika katika uagizaji wa bidhaa husika;

(xxvi) Kuhakikisha mifumo ya kielektroniki ya ununuzi wa mazao inatumika kikamilifu na kupanuliwa wigo ili kuwezesha wakulima na wafanyabiashara kupata uhifadhi salama wa mazao na kuuza mazao yao kwa bei za ushindani; na

(xxvii) Kuhakikisha miradi na programu zenye mnasaba na uchumi wa buluu zinazotekelezwa na kuibuliwa kuwa jumuishi na fungamanishi kwa kushirikiana na sekta zote zenye mnasaba wa uchumi wa buluu.

4.2 Maelekezo ya Jumla ya Uandaaji wa Mpango na Bajeti

60. Sehemu hii inatoa maelekezo kuhusu: Kamati za Bajeti; kuimarisha ukusanyaji wa mapato; kiwango cha ubadilishaji wa fedha za kigeni; uzingatiaji wa vipaumbele na

majukumu ya msingi ya Taasisi; uandaaji wa bajeti ya mishahara; uendeshaji wa ofisi na miradi ya maendeleo; mkakati wa kuongeza fedha za kigeni na mapato. Maeneo mengine ni ulipaji na udhibiti wa madeni na udhibiti wa matumizi ya fedha za umma.

4.2.1 Kamati za Bajeti

61. Katika uandaaji na utekelezaji wa Mpango na Bajeti, Maafisa Masuuli wahakikishe:

(i) Kamati za Bajeti zinaimarishwa na wajumbe wote wanashiriki kikamilifu kuandaa na kutekeleza bajeti kwa mujibu wa Kifungu cha 18(2) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Kanuni ya 17 ya Kanuni za Sheria hiyo;
(ii) Vikao vya Kamati za Bajeti vinafanyika kwa ajili ya; kutathmini mikakati na mwenendo wa ukusanyaji wa mapato na ugawaji wa rasilimali fedha zilizopokelewa/kukusanywa;
(iii) Kamati za Bajeti zinaweka mikakati ya kudhibiti uzalishaji wa madeni kwa kuhakikisha kuwa mchakato wowote wa ununuzi unaanzishwa baada ya kujiridhisha uwepo wa bajeti na uhakika wa upatikanaji wa fedha; na
(iv) Taarifa ya vikao hivyo inaandaliwa kwa kuzingatia muundo ulioainishwa kwenye **Kiambatisho Na. 1F** cha mwongozo huu na kuwasilishwa Wizara ya Fedha kila robo mwaka.

4.2.2 Maelekezo ya Kuimarisha Ukusanyaji wa Mapato

62. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuwa na mikakati ya kuongeza mapato na ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ili kufikia malengo ya Serikali kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) Kuhakikisha kuwa mapato yote yanayokusanywa yanaingizwa Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa mujibu wa Kifungu cha 58(a) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 isipokuwa pale ilipoelekezwa vinginevyo kwa mujibu wa Sheria husika;
(ii) Kuandaa, kuhuisha na kufuatilia mikakati ya kuongeza mapato na kuiwasilisha Wizara ya Fedha wakati wa uchambuzi wa mpango na bajeti pamoja na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wake kila robo mwaka;
(iii) Wizara yenye dhamana ya biashara kwa kushirikiana na wadau kutambua na kurasimisha biashara zisizo rasmi katika maeneo wanayosimamia kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo iliyopo na kuwasilisha taarifa Wizara ya Fedha kila robo mwaka;
(iv) Kuhakikisha taasisi zenye mlengo wa utoaji huduma kwa pamoja kuboresha mifumo ya ukusanyaji kwa kutoa namba ya malipo jumuishi ili kurahisisha ulipaji wa kodi, ada na tozo kwa wateja na hivyo kuongeza uhiari wa ulipaji wa mapato ya Serikali;
(v) Kuandaa na kuhuisha kanzidata na takwimu za vyanzo vyote vya mapato katika ngazi zote ikijumuisha kata, vijiji na mitaa kwa lengo la kuimarisha ukusanyaji na udhibiti wa upotevu wa mapato;
(vi) Kushirikisha wadau muhimu katika mapendekezo ya uanzishaji ushuru, ada na tozo, kabla ya kuwasilisha kwa Waziri mwenye dhamana ya fedha kupata idhini;

(vii) Kuhakikisha matumizi sahihi ya mifumo ya kielektroniki ya Serikali ya ukusanyaji wa mapato kwenye vituo vyote vya makusanyo ikiwemo maeneo ya mipaka, viwanja vya ndege, bandari pamoja na vituo vya ukaguzi ili kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato;
(viii) Kutumia matokeo ya tafiti katika kubuni, kuibua na kuendeleza vyanzo vya mapato ili kuboresha ukusanyaji wa mapato ya Serikali;
(ix) Kuhakikisha gawio na michango stahiki inawasilishwa Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa wakati kwa kuzingatia sheria na miongozo iliyopo;
(x) Kuboresha mfumo wa TAUSI ili kuwezesha ukusanyaji wa mapato ya Vijiji, Mitaa na Mamlaka za Miji midogo;
(xi) Kuwajengea uwezo viongozi na watendaji kuhusu mbinu za ukusanyaji wa mapato na kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato ya Serikali; na
(xii) Wizara yenye dhamana ya ardhi kuandaa na kuhuisha kanzidata jumuishi ya Taifa ya matumizi na usajili wa ardhi ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato.

4.2.3 Kiwango cha Ubadilishaji Fedha

63. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutumia kiwango elekezi cha ubadilishaji wa fedha za kigeni ambacho ni dola moja ya Marekani kwa shilingi za Tanzania 2,750.37 wakati wa maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2026/27.

4.2.4 Uzingatiaji wa Vipaumbele na Majukumu ya Msingi ya Taasisi

64. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia vipaumbele na majukumu ya msingi ya Taasisi zao wakati wa uandaaji wa mpango na bajeti katika muda wa kati ili kudhibiti matumizi nje ya mpango.

4.2.5 Bajeti ya Mishahara

65. Wakati wa maandalizi ya ikama na bajeti ya mishahara, Maafisa Masuuli wanaelekezwa yafuatayo:

(i) Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma yanayotarajia kuhuisha viwango vya mishahara na motisha kwa watumishi wao, yanaelekezwa kutenga bajeti kwa ajili ya kugharamia ongezeko la mishahara kwa kutumia mapato yake ya ndani bila kuathiri utoaji wa gawio na michango katika Mfuko Mkuu wa Serikali pamoja na kuwasilisha vielelezo vinavyoonesha hali ya uwekezaji, ukusanyaji wa mapato na uwezo endelevu wa Wakala za Serikali au Taasisi kujiendesha kwa mapato yake bila kutegemea ruzuku ya Serikali;
(ii) Taasisi zinazokusudia kuhuisha mishahara, posho na marupurupu ziainishe sababu za msingi za kuongeza mishahara katika kipindi husika kwa kuzingatia maelekezo ya Sera ya Malipo na Motisha katika Utumishi wa Umma ya mwaka 2010 na matakwa ya Sheria ya Utumishi wa Umma Sura, 298 kuhusu kuoanisha na kuwianisha mishahara, posho na marupurupu mengineyo katika Utumishi wa Umma;
(iii) Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma yanayotarajiwa kuhuisha viwango vya mishahara na motisha kwa watumishi zinaelekezwa kuwasilisha Ofisi ya Rais – Utumishi rasimu za miundo ya mishahara, mipango ya motisha

na mikataba ya halibora kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina na Wizara mama katika kipindi cha robo ya pili kila mwaka wa fedha kwa ajili ya kuchambuliwa na kupata gharama halisi za utekelezaji wa nyongeza ya mishahara na mipango ya motisha inayopendekezwa;

(iv) Kutenga bajeti ya ajira mpya, ubadilishaji kada/kazi, upandishaji vyeo, uhamisho, uteuzi na nyongeza ya mshahara ya mwaka kwa kuzingatia Mwongozo wa Uandaaji wa Ikama na Makadirio ya Bajeti ya Mishahara kwa Mwaka 2026/27 kutoka Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (OR-MUUUB);

(v) Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma yanayolipa mishahara kwa makusanyo ya ndani na yanayopelekewa fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kuhakikisha kiwango sahihi cha michango ya kisheria ya watumishi kinatengwa na kuwasilishwa kwa wakati katika mifuko husika ili kuepuka tozo inayotokana na ucheleweshaji wa michango hiyo na usumbufu kwa watumishi pindi wanapostaafu, aidha wanapaswa kuhakiki na kuhuisha taarifa za watumishi;

(vi) Kuandaa bajeti ya mishahara kwa kuzingatia Waraka wa Watumishi wa Serikali Na. 1 wa Mwaka 2025 na Nyaraka za Msajili wa Hazina Na. 1, 2, 3, 4, 5, 6, 7 na 8 za Mwaka 2025 kuhusu Marekebisho ya Mishahara kwa Watumishi wa Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma;

(vii) Kuzingatia Waraka wa Utumishi wa Umma Na. 1 wa Mwaka 2021 kuhusu Matumizi ya Mfumo Jumuishi wa Usimamizi wa Taarifa za Rasilimaliwatu na Mishahara (e-Watumishi); na

(viii) Wizara, Halmashauri na Taasisi za Umma kuhakikisha wanaingiza kwa wakati makato ya watumishi walionufaika na mikopo ya elimu ya juu.

4.2.6 Bajeti ya Matumizi Mengineyo

66. Wakati wa maandalizi ya makadirio ya bajeti ya matumizi mengineyo, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia yafuatayo:

(i) Kutenga bajeti kwa ajili ya kuwezesha ukusanyaji wa mapato ya Serikali;

(ii) Kutenga bajeti kwa ajili ya kugharamia mikakati ya kukabiliana na vihatarishi vya utekelezaji wa mpango na bajeti;

(iii) Kutenga bajeti kwa ajili ya kuvijengea uwezo vitengo vya ufuatiliaji na tathmini, tafiti na ubunifu na ukaguzi wa ndani kwa lengo la kuimarisha utendaji ikiwemo usimamizi wa mapato na matumizi ya fedha za umma;

(iv) Kutenga bajeti kwa ajili ya kuimarisha matumizi ya TEHAMA ikiwemo kuwajengea uwezo watumishi ili kuongeza tija na kuboresha utoaji huduma;

(v) Kuimarisha matumizi ya gesi asilia na umeme katika vyombo vya moto na mitambo ya Serikali na sekta binafsi ili kupunguza matumizi ya fedha za kigeni na kuhifadhi mazingira. Aidha, Wizara ya Ujenzi iandae vigezo vya msawazo kwa ajili ya ununuzi wa magari/mitambo kwa ajili ya matumizi ya Serikali;

(vi) Kuboresha mfumo wa usimamizi wa mali za Serikali kwa kuongeza moduli ya usimamizi wa magari (Fleet Management System) ili kupunguza gharama za matumizi;

(vii) Kutenga bajeti kwa ajili ya upimaji na upatikanaji wa hatimiliki ya maeneo yanayomilikiwa na taasisi za umma;
(viii) Kusimika mifumo ya kisasa ya uendeshaji ofisi ili kudhibiti matumizi ya umeme na maji; na
(ix) Kutenga bajeti ya maandalizi na ushiriki wa mikutano/maonesho muhimu ya kitaifa, kikanda na kimataifa.

4.2.7 Bajeti ya Maendeleo

67. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuandaa makadirio ya bajeti ya miradi ya maendeleo kwa kuzingatia yafuatayo:

(i) Kuweka kipaumbele katika kukamilisha programu na miradi inayoendelea wakati wa maandalizi ya bajeti kabla ya kuibua miradi mipya;
(ii) Kuwasilisha Wizara ya Fedha makisio ya fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ndani ya robo ya kwanza ya kila mwaka wa fedha kwa ajili ya maandalizi ya mpango na bajeti ya mwaka unaofuata;
(iii) Wizara za kisekta kuwasilisha Wizara ya Fedha na Tume ya Taifa ya Mipango mchanganuo wa shughuli na bajeti zinazotekelezwa kwenye mafungu mengine ikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kujumuishwa kwenye ukomo wa bajeti wa mafungu husika wiki ya kwanza ya mwezi Desemba, 2025;
(iv) Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma wa Mwaka 2025 katika uibuaji, uandaaji na utekelezaji wa miradi ikiwemo kuzingatia masuala ya mazingira, mabadiliko ya tabianchi na masuala ya kijamii;
(v) Matakwa ya Kifungu cha 6 cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), Sura 148 kuhusu utaratibu wa kutoa msamaha wa VAT kwa miradi inayotekelezwa kwa fedha za Serikali na Washirika wa Maendeleo;
(vi) Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura 134 inayoelekeza kutoingia mikataba ya makubaliano na Washirika wa Maendeleo ya kupokea misaada na mikopo pasipo idhini ya Waziri mwenye dhamana na masuala ya Fedha ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa mikopo ya fedha za miradi ya maendeleo inaelekezwa kwenye maeneo yenye tija na yenye manufaa kwa Taifa;
(vii) Kwa miradi itakayohitaji kufanyiwa ununuzi kabla ya kusainiwa kwa mkataba wa mkopo/msaada (Advance Procurement), inaelekezwa kupata ridhaa ya Afisa Masuuli wa fungu husika na kibali/ridhaa ya Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mlipaji Mkuu wa Serikali kabla ya mchakato huo kuanza;
(viii) Kutenga mchango wa Serikali (counterpart fund) katika miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa ushirikiano na Washirika wa Maendeleo;
(ix) Kutenga bajeti ya kugharamia fidia katika maeneo yanayotwaliwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi;
(x) Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 iliyoweka ukomo wa zabuni zinazoweza kutolewa kwa wasio wazawa ili kuwawezesha wazawa kiuchumi (local content) na kuongeza mzunguko wa fedha katika uchumi;
(xi) Kutenga bajeti kwa ajili ya kugharamia shughuli za utafiti na ubunifu;
(xii) Kuibua na kutumia njia mbadala (Alternative Project Financing) kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo yenye mlengo wa kibiashara ikiwemo

uendeshaji wa miradi ya utoaji huduma ambayo serikali imeshaweka miundombinu kwa kuzingatia sheria, kanuni, miongozo na taratibu zilizopo;

(xiii) Matumizi ya Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo (NPMIS) kwenye uibuaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo;

(xiv) Ushirikishaji wa sekta husika katika miradi inayohusisha sekta zaidi ya moja kabla, wakati na baada ya utekelezaji wa miradi kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa miradi;

(xv) Kusimamia uandaaji na utekelezaji wa Mpango wa Wajibu wa Makampuni katika Jamii (Corporate Social Responsibility - CSR) wakati wa kuingia na kutekeleza mikataba na Wazabuni au wakandarasi;

(xvi) Kuhakikisha miradi inayogharamiwa kwa fedha za mikopo ya zamani na mipya inazingatiwa kwenye bajeti; na

(xvii) Kutenga bajeti kwa ajili ya uendeshaji na matengenezo (Operations and Maintainance - O&M) ya miundombinu ya miradi iliyokamilika ili kuhakikisha uendelevu wa utoaji wa huduma kwa jamii.

4.2.8 Mkakati wa Kuimarisha Upatikanaji wa Fedha za Kigeni

68. Katika kuimarisha upatikanaji wa fedha za kigeni, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuendelea kutekeleza:

(i) Mkakati wa Taifa wa Kuimarisha Upatikanaji wa Fedha za Kigeni wa Miaka Mitano 2023/24 – 2027/28; Kifungu cha 26 cha Sheria ya Benki Kuu, Sura 197;

(ii) Sheria ya Fedha za Kigeni, Sura 271; na Kifungu cha 60 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410.

4.2.9 Mikakati ya Ulipaji na Udhibiti wa Madeni

69. Katika kutekeleza Mkakati wa Kudhibiti na Kuzuia Malimbikizo ya Madeni wa Mwaka 2022, Maafisa Masuuli wanapaswa kuzingatia yafuatayo:

(i) Kutenga bajeti kwa ajili ya kugharamia ulipaji wa madeni yaliyohakikiwa na Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali kwa kuzingatia miongozo na Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348; na

(ii) Wahakikishe kuwa kabla ya kuingia mikataba ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayogharamiwa na fedha za ndani wawasilishe kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali mpango kazi wa malipo ya mradi husika kwa kuzingatia mkataba ili uweze kuingizwa kwenye miadi ya Serikali na kuzingatiwa katika ugawaji wa fedha kwa mujibu wa kifungu cha 51 cha Sheria ya Bajeti, Sura 349.

4.3 Maelekezo Mahsusi kwa Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma

70. Watendaji Wakuu wa Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma wanaelekezwa yafuatayo:

(i) Kuhakikisha taasisi za kibiashara na za kimkakati zinazingatia Waraka wa Msajili wa Hazina Na.1 wa mwaka 2023 kuhusu kuimarisha mfumo wa usimamizi na utendaji kazi katika taasisi hizo;

(ii) Kuhakikisha michango ya mapato ghafi inawasilishwa kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa kuzingatia: Kifungu cha 8(1)(f) cha Sheria ya Msajili wa Hazina (Madaraka na Majukumu), Sura 370;
(iii) Kuwasilisha asilimia 70 ya ziada katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa kuzingatia Kifungu cha 10(2) cha Sheria ya Msajili wa Hazina (Madaraka na Majukumu), Sura 370;
(iv) Kuhakikisha maombi ya kuvuka mwaka na fedha yanawasilishwa Wizara ya Fedha kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina na fedha hizo zinatumika kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti, Sura 439 pamoja na miongozo inayotolewa na Ofisi ya Msajili wa Hazina;
(v) Kuzingatia maelekezo ya Katibu Mkuu OR-MUUUB kuhusu siku za likizo na malipo ya nauli ya likizo yaliyotolewa kwa barua yenye Kumb. Na. CAC.17/228/01/07 ya tarehe 09 Novemba, 2023;
(vi) Kuzingatia Mwongozo wa Ofisi ya Msajili wa Hazina kuhusu Uanzishaji, Uendeshaji na Usimamizi wa Kampuni Tanzu za Taasisi na Mashirika ya Umma wa Mwaka 2021;
(vii) Bajeti za kampuni tanzu zilizosajiliwa ziwasilishwe kama kiambatisho cha bajeti ya taasisi na shirika husika wakati wa uwasilishaji wa bajeti ili kuimarisha usimamizi wa kampuni tanzu; na
(viii) Kushirikisha sekta binafsi katika kutoa huduma, kuendeleza na kujenga viwanda vya kuzalisha bidhaa ndani ya nchi ikiwemo Bohari ya Dawa (MSD) ili kupunguza utegemezi wa ununuzi wa bidhaa hizo kutoka nje ya nchi.

4.4 Maelekezo kwa Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa

71. Sehemu hii inatoa maelekezo yanayopaswa kufuatwa na Maafisa Masuuli wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa wakati wa maandalizi ya Mpango na Bajeti.

4.4.1 Maelekezo kwa Ofisi za Wakuu wa Mikoa

72. Maafisa Masuuli wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa wanaelekezwa kuzingatia Vipaumbele na majukumu ya msingi wakati wa maandalizi ya mpango na bajeti ikiwemo:

(i) Kutenga bajeti kwa ajili ya kusimamia na kudumisha masuala ya usalama, na kuboresha miundombinu ya ofisi na makazi ya Viongozi katika ngazi zote;
(ii) Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na kutoa taarifa kila nusu mwaka na kwa mwaka kwa Ofisi ya Waziri Mkuu -TAMISEMI na Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu;
(iii) Kutenga bajeti kwa ajili ya kujikinga dhidi ya majanga na maafa pamoja na kuhuisha mpango wa uratibu wa maafa ngazi ya Mkoa;
(iv) Kutumia mfumo jumuishi wa ufuatiliaji na tathimini (Intergrated Monitoring and Evaluation System- iMES) katika shughuli za miradi ya maendeleo;
(v) Kusimamia utekelezaji wa Kifungu cha 37A cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290 katika utoaji na usimamizi wa mikopo kwa vikundi vya wajasiriamali wanawake, vijana na watu wenye ulemavu;

(vi) Kuzingatia maelekezo ya Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI kupitia barua yenye Kumb.Na.EB.175/369/01/73 ya tarehe 27/02/2025 kuhusu Utekelezaji wa Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali 2024 - 2034; na
(vii) Kusimamia matumizi ya mfumo wa O&OD ulioboreshwa wa mwaka 2019 katika kupanga mipango na bajeti.

4.4.2 Maelekezo Mahsusi kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa

73. Wakati wa maandalizi ya Mpango na Bajeti, Maafisa Masuuli wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wanaelekezwa kuzingatia yafuatayo:

(i) Kuendelea kutenga fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo na matumizi ya kawaida kwa kuzingatia madaraja ya Halmashauri kwa mujibu wa Mwongozo kutoka ofisi ya Ofisi ya Waziri Mkuu -TAMISEMI;
(ii) Kuandaa na kujumuisha kwenye mpango na bajeti makadirio ya mapato na matumizi ya Kata, Vijiji/Mitaa na vituo vya kutolea huduma;
(iii) Kuzingatia maelekezo ya Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu -TAMISEMI kupitia barua yenye Kumb.Na.EB.175/369/01/73 ya tarehe 27/02/2025 kuhusu Utekelezaji wa Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali 2024 - 2034;
(iv) Kutenga bajeti kwa ajili ya kukamilisha miradi viporo hususan maboma yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi. Aidha, uanzishwaji wa maboma mapya ufanyike baada ya kufanya tathmini ya kina ya mahitaji na uwezo wa wananchi kukamilisha;
(v) Kutenga bajeti kwa ajili ya kutekeleza miradi mipya ya maendeleo kwa kuzingatia Mwongozo wa Kitaifa wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma wa Mwaka 2025 na Mwongozo Wa Utekelezaji na Usimamizi Wa Miradi Ya Kuzalisha Mapato Katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa Wa Mwaka 2025;
(vi) Kutenga, kutoa na kusimamia mikopo kwa vikundi vya wajasiriamali wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa kuzingatia Kifungu cha 37A cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290;
(vii) Kutenga bajeti ya ujenzi wa miundombinu ya elimu, afya na vitega uchumi kwa muundo wa ghorofa kwa ajili ya matumizi bora ya ardhi;
(viii) Kutenga bajeti kwa ajili ya kuwatambua, kuwapanga na kuwasajili wafanyabiashara wadogo (wamachinga) katika maeneo maalumu ikiwemo ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kufanyia biashara;
(ix) Halmashauri zinazodaiwa fedha za mkopo wa mradi wa kupima, kupanga na kumilikisha ardhi zinapaswa kutenga fedha kwa ajili ya kurejesha mkopo huo Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi;
(x) Kutenga bajeti kwa ajili ya kufanya maandalizi ya miradi kabla ya kuanza utekelezaji ili kuwa na miradi yenye tija;
(xi) Kutenga bajeti kwa ajili ya ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa majengo ya utawala ya Ofisi za Halmashauri, Kata na Vijiji/Mitaa;
(xii) Kutenga kiasi kisichopungua shilingi 200,000 kutokana na mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi kwa kila Kata, Kijiji/Mtaa kila robo mwaka. Aidha, kwa Halmashauri zinazokusanya mapato chini ya shilingi bilioni

1.5 zinaelekezwa kutenga kiasi kisichopungua shilingi 100,000 kwa Kata, Kijiji/Mtaa kila robo mwaka;

(xiii) Kuendelea kutenga shilingi 100,000 kila mwezi kwa ajili ya posho ya madaraka ya watendaji wa kata;

(xiv) Kutenga bajeti kwa ajili ya kusimika Mifumo ya Kielektroniki ya Usimamizi na Uendeshaji wa Vituo vya Kutolea Huduma za Afya Tanzania (Centralized GoT – HoMIS) kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika vituo ambavyo bado havijafunga mfumo huo;

(xv) Kutenga bajeti kupitia mapato ya ndani kwa ajili ya kuchangia Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa kwa kuzingatia Sheria ya Serikali za Mitaa, Sura 290;

(xvi) Halmashauri ambazo zimepata mkopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa kutenga bajeti kutoka kwenye mapato yao ya ndani kwa ajili ya marejesho ya mkopo;

(xvii) Kutenga bajeti kwa ajili ya usambazaji na unyunyuziaji wa dawa ya viuadudu vya malaria (biolarvicides) inayozalishwa na kiwanda chaTBPL - Kibaha;

(xviii) Kuzingatia Mwongozo wa Uanzishwaji na Usimamizi wa Kampuni Mahsusi za Uendeshaji wa Miradi ya Vitega Uchumi kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa wa mwaka 2024;

(xix) Kuzingatia mwongozo wa kitaifa wa biashara ya kaboni kwa ajili ya kuboresha mapato katika mamlaka ya Serikali za Mitaa wa mwaka 2022;

(xx) Kutenga bajeti kwa ajili ya kuhamasisha matumizi ya nishati safi;

(xxi) Kutenga bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za ustawi wa jamii;

(xxii) Kusimamia na kutekeleza uandaaji wa Mpango wa Wajibu wa Makampuni katika Jamii (Corporate Social Responsibility- CSR) kwa kutumia Kanuni za Wajibu wa Wamiliki wa Leseni za Madini kwa Jamii za mwaka 2023 na Mwongozo wa Wajibu wa Kampuni na Taasisi kwa Jamii wa mwaka 2025;

(xxiii) Kutenga bajeti kwa ajili ya kamati za Wilaya za ushauri wa kisheria, maadili, msaada wa kisheria na Mpango wa Pili wa Kitaifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA - II) wa Mwaka 2024/25 – 2028/29;

(xxiv) Kutenga bajeti kwa ajili ya kuwezesha chaguzi ndogo za viongozi wa Serikali za Mitaa; na

(xxv) Kutumia mfumo wa O&OD ulioboreshwa wa mwaka 2019 katika kupanga mipango na bajeti. Aidha, vipaumbele vya vijiji vitakavyoingizwa kwenye bajeti ya Halmashauri ziwe zinatokana na jitihada za jamii ikiwemo Kutenga bajeti kwa ajili ya kujenga uwezo kwa Waratibu wa O&OD na wawezeshaji ngazi ya Kata.

4.4.3 Maelekezo ya Kisekta katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

(i) Kutenga bajeti kwa ajili ya kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika shule za msingi na sekondari kwa kuzingatia Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023;

(ii) Kuandaa, kuhakiki na kuwasilisha takwimu Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI kwa ajili ya kuwezesha utengaji wa bajeti ya Elimumsingi na Sekondari ifikapo tarehe 31 Desemba, 2025;

(iii) Kutenga bajeti kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi na chanjo kwa ajili ya vituo vya kutolea huduma za afya pamoja na kutenga shilingi 1,000 kwa kila mtoto mwenye umri wa chini ya miaka mitano ili kuimarisha huduma za lishe;
(iv) Kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika shughuli za kiuchumi na kijamii;
(v) Kutenga na kurejesha bajeti ya mapato yatokanayo na mazao ya kilimo (asilimia 20), mifugo (asilimia 15) na uvuvi (asilimia 5) ili kuboresha na kuendeleza sekta hizo;
(vi) Kuendeleza mipango miji na kufanya matumizi bora ya ardhi katika vijiji, kuendeleza miji midogo inayochipukia, kurasimisha makazi yaliyojengwa kiholela pamoja na kutoruhusu kubadili matumizi ya maeneo ya Serikali yaliyotengwa kwa ajili ya mifugo, kilimo, shoroba za wanyama pori na maeneo ya viwanda; na
(vii) Kutenga bajeti ya usimamizi na uendelezaji wa maliasili, malikale na mazingira.

4.4.4 Programu za Maboresho katika Sekta ya Umma Nchini

74. Serikali inaendelea kutekeleza Programu mbalimbali za maboresho katika sekta ya umma ili kuendana na mabadiliko ya kiuchumi, kijamii, kisayansi na kiteknolojia. Hivyo, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuweka kipaumbele na kutenga bajeti kwa ajili ya kuendelea kutekeleza Programu zifuatazo:

(i) Programu ya Maboresho katika Utumishi wa Umma Awamu ya Tatu (2021-2026) ili kuhakikisha kuwa Utumishi wa Umma unatoa huduma kwa ufanisi na tija;
(ii) Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji Awamu ya Pili 2026 - 2030 (MKUMBI II) kwa lengo la kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini kwa kuondoa changamoto katika taratibu za uwekezaji na ufanyaji biashara;
(iii) Programu ya Uimarishaji Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (2020/21 – 2029/30) ili kuboresha huduma za kiuchumi na kijamii zitolewazo kwa wananchi kwa kufanya mageuzi ya uendeshaji na uwajibikaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, kuimarisha ugatuaji wa Madaraka, kukuza Uchumi na kubadili mtazamo;
(iv) Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma Awamu ya Sita (2022/23 - 2026/27) kwa ajili ya kuendeleza na kuboresha usimamizi wa rasilimali za Umma ili kutoa huduma bora kwa wananchi; na
(v) Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II, 2023/2024 – 2029/2030) kwa lengo la kuendeleza Sekta ya Kilimo nchini.

4.5 Masuala Mengine Muhimu ya Kuzingatiwa Wakati wa Uandaaji wa Mpango na Bajeti

75. Pamoja na maelekezo ya ujumla na mahsusi yaliyotolewa, masuala mengine muhimu yanayopaswa kuzingatiwa ni: Masuala ya muungano; ushirikiano wa kikanda na kimataifa; Ujenzi wa Mji wa Serikali na Taasisi za Umma Jijini Dodoma; Uchumi wa

Buluu; Uchumi wa kidijitali; masuala ya watu wenye ulemavu; masuala ya kijinsia; mazingira; afua za lishe; VVU, UKIMWI, afya ya akili na magonjwa sugu yasiyoambukiza; mapambano dhidi ya rushwa; mapambano dhidi ya dawa za kulevya; uwekezaji na ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi; uwezeshaji wananchi kiuchumi; masuala ya haki jinai; Mashindano ya *Africa Cup of Nations* – AFCON; na Dira 2050.

4.5.1 Masuala ya Muungano

76. Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma wanaelekezwa:

(i) Kuhuisha Masuala ya Muungano katika mipango na bajeti, Mipango yote izingatie masuala ya Muungano kama yalivyoainishwa kwenye **Nyongeza ya Kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977**;

(ii) Kutenga bajeti kwa ajili ya vikao vya kuimarisha ushirikiano baina ya Wizara/Idara na Taasisi za Serikali za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar;

(iii) Kutenga bajeti ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mambo ya Muungano na kuimarisha utekelezaji wa Taasisi za Muungano pande zote mbili za Muungano; na

(iv) Kutenga fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya Muungano na kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa pande zote mbili za Muungano. Aidha, Wizara kuhakikisha zinaandaa na kuwasilisha Ofisi ya Makamu wa Rais taarifa ya utekelezaji wa miradi hiyo mara mbili kwa mwaka (Januari na Julai).

4.5.2 Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

77. Katika kuimarisha ushirikiano wa maendeleo wa kikanda na kimataifa, Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

(i) Kuzingatia maelekezo ya Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo (*Development Cooperation Framework* - DCF) wa mwaka 2017/18 - 2029/30 pamoja na mpango kazi wake;

(ii) Kuendelea kuzingatia itifaki, mikataba na makubaliano baina ya Tanzania na nchi nyingine na ile ya kikanda inayojumuisha Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Mashirika ya Kimataifa;

(iii) Kuwasilisha Wizara ya Fedha makadirio ya ada na michango ya uanachama wa Tanzania katika taasisi za kikanda na kimataifa ndani ya wiki ya kwanza ya Disemba, 2025 kwa ajili ya kujumuishwa kwenye bajeti;

(iv) Kutumia kikamilifu fursa zilizopo katika makubaliano kati ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa kwa manufaa ya Taifa kwa kuzingatia diplomasia ya uchumi; na

(v) Kutenga bajeti ya kugharamia utekelezaji wa viashiria vilivyoainishwa na Washirika wa Maendeleo kama vigezo vya kuipatia nchi msaada wa kibajeti ili kuiwezesha nchi kukidhi vigezo vya kupata fedha hizo.

4.5.3 Ujenzi wa Miundombinu na Ofisi za Wizara na Taasisi za Umma Katika Mji wa Serikali Jijini Dodoma

78. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia mahitaji ya ujenzi wa miundombinu na ofisi za Wizara na Taasisi katika Mji wa Serikali na Makao Makuu Dodoma. Hii ni pamoja na kuzingatia ulipaji wa madeni na madai ya wakandarasi na washauri elekezi pamoja na gharama za samani.

4.5.4 Uchumi wa Buluu

79. Maafisa Masuuli wa Sekta zenye mnasaba na uchumi wa buluu wanaelekezwa kuendelea kutekeleza Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu ya Mwaka 2024 na Mkakati wa Taifa wa Utekelezaji wa Sera ya Uchumi wa Buluu wa Mwaka 2024 – 2034 kwa kuzingatia yafuatayo:-

(i) Kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za uchumi wa buluu ili kuhakikisha shughuli hizo zinatekelezwa kwa ufanisi na kuwasilisha taarifa za utekelezaji Ofisi ya Makamu wa Rais kila nusu mwaka;na
(ii) Kuendelea kutumia fursa za kifedha zinazopatikana kupitia Mikataba na Itifaki mbalimbali zenye mnasaba na uchumi wa buluu katika kutekeleza miradi na programu za uchumi wa buluu.

4.5.5 Uchumi wa Kidijitali

80. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Uchumi wa Kidijitali 2024–2034 kwa kuzingatia yafuatayo:

(i) Kutenga bajeti kwa ajili ya kujenga mfumo jumuishi wa kisekta na kuhakikisha mfumo huo unabadilishana taarifa na mifumo mingine;
(ii) Kuhakikisha mifumo inayotoa huduma kwa wananchi inaunganishwa na mfumo wa utambuzi wa watu (Jamii Namba);
(iii) Kuhakikisha vituo vya kutolea huduma kwa wananchi vinaunganishwa na mtandao wa intaneti ili kuboresha utoaji wa huduma;
(iv) Kutenga bajeti kwa ajili ya kuandaa miongozo ya matumizi ya dijitali kwa sekta;
(v) Kutenga bajeti kwa ajili ya kutoa elimu/ mafunzo kuhusu usalama na matumizi ya TEHAMA kwa sekta; na
(vi) Kushirikisha sekta binafsi ili kuwezesha ubunifu na teknolojia, kuharakisha usimikaji wa mifumo na miundombinu ya kidijitali.

4.5.6 Masuala ya Watu Wenye Ulemavu

81. Katika eneo hili Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuendelea kuzingatia Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2004 na Sheria ya Watu Wenye Ulemavu, Sura 183 hususan kwa:

(i) Kuhakikisha kuwa bajeti za ujenzi na ukarabati wa miundombinu zinazingatia mahitaji ya Watu Wenye Ulemavu;
(ii) Kuzingatia maelekezo ya Mwongozo wa Utekelezaji, Ujumuishwaji na Uimarishaji wa Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu Tanzania wa mwaka 2022;
(iii) Kutenga bajeti kwa ajili ya kutoa elimu kwa jamii kuhusu masuala ya Watu Wenye Ulemavu; na

(iv) Kutenga bajeti kwa ajili ya mahitaji ya watumishi wa umma wenye ulemavu kwa kuzingatia Mwongozo wa Huduma kwa Watumishi wa Umma Wenye Ulemavu wa Mwaka 2008.

4.5.7 Uandaaji wa Bajeti yenye Mlengo wa Kijinsia

82. Serikali imedhamiria kuendeleza maboresho ya bajeti ya Serikali yatakayohakikisha uimarishaji wa usawa wa kijinsia unaokwenda sambamba na Lengo Namba 5 la Maendeleo Endelevu (SDGs); Dira 2050; na Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake (2023). Dhana ya bajeti ya jinsia inalenga kuimarisha na kuhakikisha kuwa makundi yote yanazingatiwa ipasavyo katika mipango na bajeti za kila Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

83. Katika bajeti ya Mwaka 2026/27 Serikali itaanza kutumia dhana ya bajeti yenye mlengo wa kijinsia (Gender Responsive Budgeting- GRB) kwa Wizara 9 za majaribio (Pilot) zilizopata mafunzo ambazo ni **Kilimo; Elimu, Sayansi na Teknolojia; Katiba na Sheria; Maji; Afya; Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Mifugo na Uvuvi; Viwanda na Biashara; Mambo ya Ndani;** pamoja na **Mikoa ya Geita na Singida; na Halmashauri za Wilaya za Tandahimba na Chalinze.** Maafisa Masuuli wazingatie yafuatayo:

(i) Kufanya uchambuzi wa masuala ya kijinsia (Gender analysis) ili kubaini pengo la kijinsia katika upatikanaji na matumizi ya rasilimali na kutenga fedha kwa ajili ya kutekeleza afua za kupunguza pengo husika;

(ii) Taasisi za Majaribio zitatakiwa kuandaa na kuwasilisha Wizara ya Fedha Taarifa ya Bajeti ya Kijinsia Mwezi Februari, 2026 kwa kuzingatia **Kiambatisho Na. 1G** ili kuwezesha uandaaji wa GBS itakayokuwa sehemu ya bajeti kuu ya Serikali;

(iii) Kuandaa na kutekeleza mipango inayozingatia takwimu zilizonyumbulishwa kijinsia (gender disaggregated data) ili kurahisisha upimaji wa matokeo;

(iv) Kutenga bajeti kwa ajili ya mafunzo kuhusu uandaaji wa mipango na bajeti zenye mlengo wa kijinsia ili kuleta usawa wa kijinsia na kuwa na jamii jumuishi; na

(v) Kutekeleza Mpangokazi wa Pili wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA II 2024/25 – 2028/29).

4.5.8 Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi

84. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia mabadiliko ya tabianchi katika uandaaji na utekelezaji wa mipango na bajeti ikiwa ni pamoja na:

(i) Kutenga bajeti kupitia *Objective X* kwa kuzingatia vipaumbele katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ikiwa ni pamoja na mipango na mikataba ya Kimataifa ambayo nchi imeingia katika kutekeleza masuala ya mabadiliko ya tabianchi mathalan, Mchango wa Kitaifa wa Kupunguza Gesijoto (National Determined Contribution - NDC 3.0, 2025-2035);

(ii) Kuendelea kutekeleza Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022 - 2032) pamoja na mkakati wa Taifa wa kukabiliana mabadiliko ya tabianchi ili kuongeza ufanisi katika kushughulikia uhifadhi wa mazingira na mabadiliko ya tabiachini;
(iii) Kuendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024 – 2034) kwa kuvutia uwekezaji na kuongeza matumizi ya nishati safi kwa taasisi zinazolisha zaidi ya watu 100;
(iv) Kuendelea kutekeleza Mwongozo wa Biashara ya Kaboni wa Mwaka 2022 na kuhimiza taasisi kuandaa maandiko ya kutumia fursa zilizopo kwenye biashara ya kaboni ili kuongeza mapato ya serikali na kuendelea kutunza mazingira;
(v) Kutoa elimu na kuhamasisha jamii ili kuwezesha Taifa kunufaika na fursa ya biashara ya kaboni;
(vi) Kuongeza juhudi katika kuandaa miradi na kutumia fursa za upatikanaji wa fedha katika Mifuko ya mazingira na mabadiliko ya Kimataifa (GEF, AF, LDCF, GBFF, UNCDF na Loss and Damage Fund);
(vii) Kubuni mbinu mpya za kuwezesha upatikanaji wa fedha kutoka benki za maendeleo za kimataifa, sekta binafsi na vyanzo vya ndani vya fedha kwa ajili ya miradi/programu za mazingira na mabadiliko ya tabianchi;
(viii) Kutambuana kutoa alama (code) maalum kwa kutaja programu na shughuli ndani ya Wizara zinazohusu mazingira na mabadiliko ya tabianchi kwa kuzingatia Objective X na kuziwasilisha Wizara ya Fedha; na
(ix) Kuendelea kujumuisha masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi na kuzingatia usawa wa jinsia katika mikakati ya kuhimili na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi wakati wa maandalizi na utekelezaji wa mipango na bajeti.

4.5.9 Afua za Lishe

85. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya afua za lishe kupitia *Objective* Y kwa ajili ya kutekeleza afua za lishe ikiwemo: kutoa elimu kwa jamii juu ya mbinu za kukabiliana na tatizo la ongezeko la uzito uliozidi, kiribatumbo na umuhimu wa matumizi sahihi ya chakula ili kuimarisha hali ya lishe; Kuimarisha ushirikishaji wa sekta mbalimbali ikiwemo sekta binafsi katika masuala ya lishe; na kuongeza upatikanaji wa huduma za lishe bora ngazi ya jamii na vituo vya kutolea huduma za jamii na kugharamia masuala ya uratibu, ufuatiliaji na tathmini kuhusu utekelezaji wa afua za lishe katika ngazi zote.

4.5.10 VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza

86. Maafisa Masuuli wanaelekezwa:
(i) Kutekeleza Sera ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI ya Mwaka 2001 na Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa VVU na UKIMWI, Sura 431;
(ii) Kutenga bajeti na kuzingatia maelekezo ya Mwongozo na Waraka Na. 2 wa Utumishi wa Umma wa Mwaka 2014 kuhusu kudhibiti VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa Mahali pa Kazi katika Utumishi wa Umma;

(iii) Kutenga bajeti kwa ajili ya kutekeleza Mpango Mkakati wa Taifa wa Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa Yasiyoambukiza wa mwaka 2021 – 2026; na
(iv) Kutenga bajeti kwa ajili ya kutekeleza afua za kudhibiti changamoto za afya ya akili na msaada wa kisaikolojia kwa watumishi wa umma.

4.5.11 Mapambano Dhidi ya Rushwa

87. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutenga bajeti kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Nne 2023/24- 2029/30 na afua zake pamoja na kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji huduma kwa umma. Vilevile, wanaelekezwa kuimarisha ushirikiano na Taasisi zisizo za kiserikali katika utekelezaji wa Mkakati husika. Aidha, wanahimizwa kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa mkakati kupitia mfumo wa e-Maboresho.

4.5.12 Mapambano Dhidi ya Dawa za Kulevya

88. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuendelea kuzingatia Sera ya Taifa ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya Mwaka 2024, Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura 95 na maelekezo ya Mwongozo wa Utoaji Elimu Kuhusu Tatizo la Dawa za Kulevya Nchini wa Mwaka 2022.

4.5.13 Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

89. Katika kuvutia Sekta binafsi kuchangia upatikanaji wa rasilimali (fedha, teknolojia na ujuzi) kupitia utaratibu wa PPP. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia yafuatayo:
(i) Kuzingatia Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Sura 103, Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma, 2025 Kuhusu miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa utaratibu wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi – PPP;
(ii) Kuanzisha na kutenga bajeti kwa ajili ya kuimarisha utendaji kazi wa PPP *Node* na madawati ya PPP;
(iii) Kutenga bajeti kwa ajili ya kuwajengea uwezo maafisa wanaohusika na uibuaji, uandaaji na usimamizi wa miradi ya ubia katika ngazi ya kisekta, mikoa na Halmashauri;
(iv) Kutenga bajeti kwa ajili ya uhamasishaji kuhusu dhana na umuhimu wa kutumia utaratibu wa PPP;
(v) Kukamilisha maandalizi ya miradi iliyopo ili kuharakisha utekelezaji;
(vi) Wakala za Serikali, Idara Zinazojitegemea, Taasisi na Mashirika ya Umma yanapaswa kuibua na kufanya maandalizi ya miradi isiyo pungua minne (4) inayoweza kutekelezwa kwa utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi na kuwasilisha miradi hiyo Wizara ya Fedha baada ya kupata kibali kutoka Tume ya Taifa ya Mipango;
(vii) Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Ofisi za wakuu wa mikoa zinapaswa kuibua na kufanya maandalizi ya miradi isiyo pungua mitatu (3) inayoweza kutekelezwa kwa utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta

binafsi na kuwasilisha miradi hiyo Wizara ya Fedha baada ya kupata kibali kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI na Tume ya Taifa ya Mipango; na

(viii) Kutenga bajeti kwa ajili ya maandalizi ya miradi kwa kuzingatia ukubwa na aina ya mradi. Aidha, kwa ajili ya miradi ya PPP inayohitaji ruzuku katika hatua ya utekelezaji, inapaswa kutengewa bajeti kwa kuzingatia mahitaji ya kila mwaka ya ruzuku hiyo.

4.5.14 Fursa na Taarifa za Ajira Zilizozalishwa

90. Katika kufikia malengo yaliyobainishwa katika mipango ya maendeleo kuhusu uzalishaji na upatikanaji wa taarifa sahihi za ajira, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia yafuatayo:

(i) Kuratibu upatikanaji wa fursa na ajira zilizozalishwa katika sekta ya umma na binafsi ikiwemo ajira nje ya nchi;
(ii) Kujisajili katika Mfumo wa Kitaifa wa Kieletroniki wa taarifa za soko la ajira kupitia www.nlmis.go.tz;
(iii) Kujaza maoteo ya ajira zitakazozalishwa kutokana na utekelezaji wa bajeti, programu na miradi yao kupitia Mfumo wa Kitaifa wa Kielektroniki wa Taarifa za Soko la Ajira; na
(iv) Kujaza kwa ukamilifu Fomu Na.15A na15B na kuzipandisha katika Mfumo wa Kitaifa wa Kieletroniki wa taarifa za soko la ajira kwa kila robo mwaka.

4.5.15 Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

91. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia yafuatayo:

(i) Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya Mwaka 2004 na Sheria ya Taifa uwezeshaji wananchi kiuchumi, Sura 386;
(ii) Kutenga bajeti kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma kuhusu fursa zilizopo kwenye miradi zinazoweza kutekelezwa na wananchi;
(iii) Kutoa upendeleo wa kipekee kwa wazawa; makundi maalum; bidhaa zilizotengenezwa, zilizozalishwa au kuchimbwa nchini na kampuni za ndani katika ununuzi wa umma kwa kuzingatia kanuni za ununuzi wa Umma za Mwaka 2024;
(iv) Kutenga bajeti kwa ajili ya miundombinu wezeshi ya kuimarisha mafunzo kwa vitendo ikiwemo ununuzi wa mitambo, mashine, teknolojia na vifaa vya kufundishia kwa lengo la kuendana na mahitaji ya sasa ya soko la ajira;
(v) Sheria na Miongozo kuhusu utekelezaji wa afua za uwezeshaji wa wananchi kiuchumi na kuwasilisha taarifa OWM – SBU; na
(vi) Kuweka mazingira wezeshi ya kupata mikopo nafuu kwa wakandarasi na wazabuni wa ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

4.5.16 Masuala ya Haki Jinai

92. Maafisa Masuuli wanaohusika katika mnyororo wa Haki Jinai wanaelekezwa kuweka kipaumbele katika utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai kwa kutenga fedha na kutekeleza mipango na mikakati ya utekelezaji wa mapendekezo hayo. Pamoja na mikakati na mipango hiyo, wanaelekezwa pia kutekeleza yafuatayo:

(i) Kutenga bajeti kwa ajili ya kuwajengea uwezo watumishi wa taasisi za haki jinai ili waweze kutekeleza majukumu kwa weledi na ufanisi;
(ii) Kutenga bajeti kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma kuhusu haki na wajibu wa kila mwananchi katika mnyororo wa haki jinai kwa ajili ya ustawi wa utawala bora nchini;
(iii) Kusimamia na kuimarisha miundombinu na mifumo ya TEHAMA ili kuwezesha taasisi zilizopo katika mnyororo wa haki jinai kuendelea kubadilishana taarifa na kuboresha utendaji kazi;
(iv) Kuendelea kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi ili kuongeza kasi na tija ya utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai;
(v) Kutekeleza programu za maboresho na kuratibu marekebisho ya sheria ili kuboresha utendaji wa taasisi za Haki Jinai na mfumo wa utoaji haki nchini;
(vi) Kuimarisha na kuhimiza matumizi ya mfumo wa uratibu na usimamizi wa utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai;
(vii) Kuandaa na kutekeleza mikakati ya kubaini na kuzuia uhalifu kulingana na majukumu ya taasisi; na
(viii) Taasisi zinazohusika na mnyororo wa haki jinai ziwasilishe kila robo mwaka taarifa za utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai kupitia mfumo wa e-Maboresho.

4.5.17 Mashindano ya *African Cup of Nations* – AFCON

Maafisa Masuuli wa Sekta zinazohusika na maandilizi ya AFCON wahakikishe wanatenga bajeti kwa ajili ya:

(i) Ujenzi wa miundombinu ya msingi kwa ajili ya mashindano ikiwemo viwanja vya michezo na mazoezi;
(ii) Ujenzi wa miundombinu wezeshi ikiwemo barabara, maji, umeme na mawasiliano;
(iii) Kuandaa mkakati maalum kwa ajili ya kuhakikisha Taifa linanufaika na fursa za kibiashara na utalii kwa kushirikiano na sekta binafsi;
(iv) Huduma bora za afya;
(v) Maandalizi ya Timu ya Taifa; na
(vi) Kuimarisha ulinzi na usalama.

4.5.18 Dira 2050

93. Katika kuhakikisha Dira 2050 inatekelezwa kikamilifu, ikiwa ni pamoja na kuwianisha na mipango na mikakati ya kitaifa, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutekeleza yafuatayo:

(i) Kutenga bajeti kwa ajili ya kufanya tathmini na mapitio ya sera, sheria, mipango, mikakati na miongozo ili iendane na Dira 2050;
(ii) Kuandaa nyenzo za kupima matokeo ya utendaji kwa kuzingatia malengo ya Dira 2050;
(iii) Kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathimini;
(iv) Kushirikisha sekta binafsi katika utekelezaji wa Dira 2050; na

(v) Kutoa elimu kwa umma na mawasiliano ya kimkakati kuhusu Dira 2050.

4.6 Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji Taarifa za Utekelezaji wa Mpango na Bajeti

94. Katika ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa za utekelezaji wa mpango na bajeti, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia yafuatayo:

(i) Kutenga bajeti na kuwajengea uwezo wataalam wa ufuatiliaji na tathmini pamoja na kurithisha maarifa kwa watumishi wapya;
(ii) Kujumuisha gharama za ufuatiliaji na tathmini kwenye bajeti za miradi ya maendeleo ili miradi itekelezwe kwa ubora uliokusudiwa (Value for money);
(iii) Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini uandaliwe sambamba na Mpango kazi na Mtiririko wa fedha kupitia mifumo ya NPMIS, CBMS na PlanRep;
(iv) Kuwasilisha Wizara ya Fedha taarifa za utekelezaji za kila robo mwaka ndani ya siku 30 baada ya kukamilika kwa robo ya mwaka husika kwa mujibu wa Kifungu cha 55 (4) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439;
(v) Kuwasilisha Tume ya Taifa ya Mipango taarifa za ufuatiliaji, tathmini na utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kuzingatia Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma wa Mwaka 2025;
(vi) Kusimamia maandalizi ya taarifa za ufuatiliaji, tathmini na utendaji kulingana na miundo iliyobainishwa katika Mwongozo Jumuishi wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mwaka 2024 na kuwasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu kila robo mwaka na pindi itakapohitajika; na
(vii) Nakala za taarifa za utekelezaji za robo mwaka na mwaka mzima kutoka Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ziwasilishwe Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, Taasisi na Mashirika ya Umma ziwasilishwe Ofisi ya Msajili wa Hazina na Wizara mama.

VIAMBATISHO VYA MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KATIKA MUDA WA KATI (2026/27 - 2028/29)

YALIYOMO

Kiambatisho Na. 1A **.. 1**
1. MAPITIO YA MWENENDO NA MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI..... 1
1.1 Utangulizi 1
1.2 Mwenendo na Mwelekeo wa Uchumi 1
Kiambatisho Na. 1B **.. 18**
2 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2024/25 18
2.1 Utangulizi 18
2.2 Mapato na Matumizi 18
2.3 Mafanikio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2024/25.... 19
2.4 Fursa zilizojitokeza katika utekelezaji wa bajeti 45
2.5 Hatua za kuchukua ili Kutumia Fursa Zilizopo 46
Kiambatisho Na. 1C **.. 48**
3 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAELEKEZO YA MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2025/26 48
3.1 Utangulizi 48
3.2 Sura ya Bajeti ya Mwaka 2025/26 48
3.3 Utekelezaji wa Maelekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2025/26 50
3.4 Mwenendo wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2025/26.................... 54
3.4.1 Mapato 54
3.4.2 Matumizi 55
3.4.3 Kugharamia Nakisi 55
Kiambatisho Na. 1D **.. 56**
MUUNDO WA MTEF 2026/27 - 2028/29 56
Kiambatisho Na. 1E **.. 57**
RANDAMA YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/27. 57
Kiambatisho Na. 1F **.. 61**
MUUNDO WA TAARIFA YA KAMATI YA BAJETI 61
Kiambatisho Na. 1G **.. 62**
Gender Budget Statement Format **.. 62**

Kiambatisho Na. 1A

1. MAPITIO YA MWENENDO NA MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI

1.1 Utangulizi

1. Sehemu hii inatoa tathmini ya mwenendo na mwelekeo wa viashiria vya hali ya uchumi ikiwemo ukuaji wa uchumi, mfumuko wa bei, mikopo kwa sekta binafsi, viwango vya riba, urari wa biashara na deni la Serikali.

1.2 Mwenendo na Mwelekeo wa Uchumi

1.2.1 Ukuaji wa Uchumi wa Dunia na Kikanda

2. Uchumi wa dunia umeendelea kuimarika licha ya kukabiliana na changamoto mbalimbali ikiwemo zilizotokana na migogoro ya kikanda na kutokutabirika kwa sera za biashara. Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa - IMF World Economic Outlook (WEO), toleo la Oktoba 2025, uchumi wa dunia ulikua kwa wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 3.5 mwaka 2023. Ukuaji wa uchumi wa dunia unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 3.2 mwaka 2025 na asilimia 3.1 mwaka 2026. Maoteo hayo yanatokana na utekelezaji wa sera za bajeti zinazolenga kuongeza fedha katika uchumi na kupungua kwa athari zitokanazo na utekelezaji wa sera za bajeti zinazolenga kuongeza ushuru kwa mataifa yaliyoendelea hususan nchi ya Marekani.

3. Katika nchi zilizoendelea, uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 1.8 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 1.7 mwaka 2023 na unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 1.6 mwaka 2025 na mwaka 2026. Uchumi wa nchi zinazoibukia kiuchumi na zinazoendelea ulikua kwa wastani wa asilimia 4.3 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 4.7 mwaka 2023 na unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 4.2 mwaka 2025 na asilimia 4.0 mwaka 2026.

4. Uchumi wa nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara ulikua kwa wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 3.7 mwaka 2023 na unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2025 na asilimia 4.4 mwaka 2026. Uchumi wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika - SADC ulikua kwa wastani wa asilimia 3.0 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 3.8 mwaka 2023 na unatarajiwa kukua kwa asilimia 3.4 na asilimia 3.7 mwaka 2025 na 2026, mtawalia.

5. Kwa mujibu wa taarifa ya IMF ya Oktoba 2025, uchumi wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki - EAC ulikua kwa wastani wa asilimia 1.7 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 5.3 mwaka 2023. Kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi wa ukanda wa EAC ilichangiwa na kuporomoka kwa uchumi wa nchi ya Sudani Kusini ambao ulikuwa na ukuaji hasi wa asilimia 26.1 mwaka 2024. Uchumi wa nchi za EAC unakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 7.7 mwaka

2025 na mwaka 2026. Mwenendo wa uchumi wa Dunia na baadhi ya jumuiya za kikanda ni kama unavyoonekana katika **Jedwali Na. 1.1**.

Jedwali Na. 1.1: **Mwenendo na Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia na Kikanda**

	2022	**2023**	**2024**	**2025**	**2026**
Dunia	3.6	3.5	3.3	3.0	3.1
Nchi zilizoendelea	2.9	1.8	1.8	1.5	1.6
Nchi zinazoibukia na zinazoendelea	4.1	4.7	4.3	3.7	3.9
Nchi zilizo chini ya Jangwa la Sahara	4.1	3.6	4.0	3.8	4.2
SADC	4.9	3.8	3.0	3.4	3.7
Jumuiya ya Afrika Mashariki*	5.6	5.6	5.6	5.3	5.6

Chanzo: IMF – WEO, Oktoba 2025
Tanbihi; * Haijumuishi takwimu za Sudani Kusini

1.2.2 Ukuaji wa uchumi wa Tanzania

6. Kwa mujibu wa takwimu zilizokokotolewa kwa kuzingatia mwaka wa kizio wa 2019, Pato halisi la Taifa lilikua kwa asilimia 5.6 mwaka 2024 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.2 mwaka 2023. Ukuaji huo ulichangiwa na: uwekezaji wa Serikali kwenye miradi ya kimkakati na ya kielelezo inayohusisha miundombinu ya nishati na usafirishaji; kuanza kwa uzalishaji wa umeme katika Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Julius Nyerere; kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi; usimamizi madhubuti wa sera za fedha; kuimarika kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo; kuimarika kwa huduma za fedha na bima; pamoja na uwekezaji wa Serikali katika huduma za jamii ikiwemo elimu, afya, maji na hifadhi ya jamii.

7. Shughuli za kiuchumi za kilimo zimeendelea kuwa na mchango mkubwa katika Pato la Taifa kwa kuchangia asilimia 24.9, ikifuatiwa na shughuli za ujenzi (asilimia 12.5), biashara na matengenezo (asilimia 8.6) na usafiri na usafirishaji (asilimia 8.1). Aidha, shughuli za kiuchumi zilizochangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa Pato la Taifa ni kilimo (asilimia 20.8) ikifuatiwa na usafiri na usafirishaji (asilimia 10.4) na fedha na bima (asilimia 9.3) kama inavyooneka katika **Kielelezo Na. 1.1**. Kwa mujibu wa taarifa ya Benki ya Dunia iliyotolewa tarehe 01 Julai 2025, wastani wa pato kwa kila mtu (Per Capita GNI) ilikua dola za Marekani 1,200 mwaka 2024 ikilinganishwa na dola za Marekani 1,136 ambao ni wigo wa chini kwa nchi zenye uchumi wa kipato cha chini ngazi ya kati (lower middle income).

Kielelezo Na. 1.1: Mwenendo wa Pato la Taifa, 2020 – 2024

(Asilimia)



*Baadhi ya shughuli za kiuchumi zilizoongoza

8. Katika nusu ya kwanza (Januari - Juni) ya mwaka 2025, ukuaji wa Pato la Taifa kwa bei za mwaka wa kizio wa 2015 ulifikia wastani wa asilimia 5.8 ikilinganishwa na asilimia 5.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ukuaji huo ulitokana na: uwekezaji wa Serikali katika miradi ya kimkakati ya miundombinu ya nishati, maji, na usafirishaji; kuongezeka kwa shughuli za uzalishaji hususan kilimo, viwanda na uchimbaji wa madini na mawe; pamoja na kuendelea kuimarika kwa sekta ya fedha na shughuli za usafirishaji nchini. Aidha, sekta zilizochangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji ni sekta ya madini iliyochangia asilimia 15.4 ikifuatiwa na kilimo (asilimia 15.3), ujenzi (asilimia 11.7) na fedha na bima (asilimia 10.7) kama inavyooneka katika **Kielelezo Na.1.2**.

9. Tathmini ya awali iliyofanywa kuhusiana na athari za matukio ya wakati na baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 inaonesha uwezekano wa kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi hususani katika robo ya nne ya mwaka 2025. Sekta zilizoathirika ni pamoja na utalii, usafirishaji na mawasiliano. Kutokana na hili, lengo la ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2025 la asilimia 6.0 linakadiriwa kupungua hadi asilimia 5.9.

Kielelezo Na. 1.2: Mwenendo wa Pato la Taifa kwa Nusu ya Kwanza, 2021 – 2025



*Baadhi ya shughuli za kiuchumi zilizoongoza

10. Kwa kuzingatia mwenendo wa viashiria mbalimbali ikiwemo ukuaji halisi wa Pato la Taifa katika nusu ya kwanza na athari za matukio ya wakati na baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025, uchumi unatarajiwa kukua kwa asilimia 5.9 mwaka 2025 na kuongezeka hadi asilimia 6.3 mwaka 2026. Aidha, katika kipindi cha muda wa kati (2025 – 2029) uchumi unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 6.9. Ukuaji huu utategemea utekelezaji endelevu wa miradi mikubwa ya kimkakati inayohusisha miundombinu ya nishati na usafirishaji, jitihada za Serikali kuboresha mazingira ya uwekezaji, utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili – ASDP II na Mpango Kabambe wa Sekta ya Kilimo 2050, utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha pamoja na uwekezaji wa Serikali katika sekta ya huduma za kijamii. Mwelekeo wa uchumi katika kipindi cha muda wa kati ni kama unavyoonekana katika **Kielelezo Na. 1.3**.

Kielelezo Na. 1.3: Mwelekeo wa Uchumi wa Tanzania



*Mwaka 2025 – 2030 ni maoteo

1.2.3 Mfumuko wa Bei wa Dunia na Kikanda

11. Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa - IMF World Economic Outlook (WEO), toleo la Oktoba 2025, mfumuko wa bei uliendelea kupungua katika nchi nyingi kutokana na utekelezaji wa sera za fedha zilizolenga kuwa na utulivu wa mfumuko wa bei. Mfumuko wa bei wa dunia unatarajiwa kupungua kutoka wastani wa asilimia 5.6 mwaka 2024 hadi asilimia 4.2 mwaka 2025 na asilimia 3.7 mwaka 2026.

12. Mwaka 2024/25, mwenendo wa mfumuko wa bei katika nchi za ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ulikuwa ndani ya wigo wa wastani usiozidi asilimia 8 kutokana na kupungua kwa bei za nishati, hususan bidhaa za petroli na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti katika nchi hizo. **Kielelezo Na. 1.4** kinaonesha mwenendo wa mfumuko wa bei kwa baadhi ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kielelezo Na. 1.4: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei kwa Baadhi ya Nchi za EAC

(Asilimia)



1.2.4 Mfumuko wa Bei Tanzania

13. Katika kipindi cha Julai hadi Novemba 2025, wastani wa mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 3.4 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Aidha, mfumuko wa bei kwa mwezi Novemba, 2025 ulikuwa asilimia 3.4 ikilinganishwa na asilimia 3.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Hii ilitokana na kupungua kwa ugavi wa bidhaa za vyakula katika soko la ndani kufuatia ongezeko la mauzo kwenda nchi jirani. Kiwango hicho kipo ndani ya lengo la nchi la asilimia 3.0 hadi 5.0. Vilevile, kiwango hicho kipo ndani ya lengo la Jumuiya ya Afrika Mashariki la kutozidi asilimia 8.0 na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika la kati ya asilimia 3.0 hadi asilimia 7.0. Hii ilitokana na utekelezaji wa sera madhubuti za fedha, kuimarika kwa bei ya mafuta na bidhaa katika soko la dunia, na utulivu wa thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani iliyochangia kupunguza kasi ya ongezeko la bei ya bidhaa na huduma.

14. Katika kipindi cha Julai hadi Novemba 2025, mfumuko wa bei usiojumuisha vyakula visivyochakatwa na nishati (Core Inflation) umepungua na kufikia wastani wa asilimia 2.1 ikilinganishwa na asilimia 3.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Aidha, mfumuko wa bei za vyakula na vinywaji baridi uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 7.3 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 2.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2024 (**Kielelezo Na. 1.5**). Hali

hiyo ilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa bei za baadhi ya bidhaa kuu za chakula kama vile ulezi, mahindi na mchele.

Kielelezo Na. 1.5: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei Nchini (Desemba 2024 hadi Novemba 2025)

(Asilimia)



15. Mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki ndani ya lengo la nchi la kati ya asilimia 3.0 hadi 5.0, lengo la Jumuiya ya Afrika Mashariki (usiozidi asilimia 8.0) na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (asilimia 3.0 – 7.0). Matarajio hayo yatategemea kuendelea kuimarika kwa upatikanaji wa chakula nchini na katika nchi jirani; uwepo wa umeme wa uhakika; kutengemaa kwa bei za bidhaa, hususan bidhaa za mafuta katika soko la dunia; utekelezaji wa sera madhubuti za fedha na bajeti; kuendelea kuimarika kwa uchumi wa dunia na utekelezaji wa mikakati mbalimbali ya kuongeza mauzo ya bidhaa na huduma nje; na kuongeza uzalishaji wa ndani ili kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje.

1.2.5 Sekta ya Fedha

1.2.5.1 Utekelezaji wa Sera ya Fedha

16. Katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2025, utekelezaji wa sera ya fedha ulilenga kuhakikisha kuwa matarajio ya mfumuko wa bei yanabaki ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5 na kuchagiza ukuaji wa uchumi. Kwa muktadha huo, Kamati ya Sera ya Fedha, iliamua kupunguza Riba ya Benki Kuu - CBR kutoka asilimia 6.00 kwa kipindi cha mwaka 2024/25 hadi asilimia 5.75 kwa kipindi cha Julai hadi Desemba 2025. Uamuzi huu ulilenga kuongeza ukuaji wa mikopo kwenye sekta ya binafsi ili kuchochea zaidi shughuli za kiuchumi. Uamuzi huu pia ulizingatia mwelekeo wa mfumuko wa bei ambao unatarajiwa kuendelea kuwa chini ya asilimia 5; kukabiliana na vihatarishi vinavyotokana na kutotabirika kwa mwenendo wa uchumi wa dunia, na kuendelea kuimarika kwa hali ya uchumi wa ndani. Hivyo, Benki Kuu imeendelea kutekeleza sera ya fedha kwa lengo la kuhakikisha kuwa riba ya mikopo ya siku saba katika soko la fedha baina ya benki inakuwa ndani ya wigo wa asilimia 3.75 hadi asilimia 7.75.

17. Utekelezaji wa sera ya fedha ulikuwa na matokeo ya kuridhisha kuendana na malengo ya uchumi kwa mwaka 2025/26. Mfumuko wa bei uliendelea kuwa tulivu huku kiwango cha ukwasi kikiendana na mahitaji ya shughuli za kiuchumi, hivyo kuchochea ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi. Riba ya mikopo ya siku saba katika soko la fedha baina ya mabenki, ambayo hutumika kama kiashiria cha utekelezaji wa sera ya fedha, ilikuwa tulivu na ndani ya wigo wa CBR.

18. Utekelezaji wa sera ya fedha uliwezesha, ujazi wa fedha (M3) kukua na kufikia wastani wa asilimia 21.0 kwa kipindi cha miezi mitano ya kwanza ya mwaka 2025/26, kutoka asilimia 12.1 katika kipindi kama hicho cha mwaka 2024/25, kufuatia uwepo wa ukwasi wa kutosha kwenye uchumi. Aidha, M3 ilikua kwa asilimia 23.0 Novemba 2025 ikilinganishwa na asilimia 13.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2024.

1.2.5.2 Mikopo kwa Sekta Binafsi

19. Katika kipindi cha Julai hadi Novemba 2025, mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa wastani wa asilimia 16.5, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 16.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Hadi Novemba 2025, ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ulifikia asilimia 18.1 kwa mwaka, ikilinganishwa na asilimia 15.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Hii ilitokana na utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi kwenye uchumi.

20. Shughuli za kilimo zimeendelea kuwa na ukuaji wa kasi wa mikopo zikifuatiwa na biashara, uchimbaji madini, shughuli za usafirishaji pamoja na ujenzi. Mikopo kwa shughuli za kilimo imeendelea kukua kwa kasi kutokana na hatua za kisera zilizochukuliwa na Benki Kuu kuchochea ukuaji wa mikopo kwa

shughuli za kilimo kwa gharama nafuu ambazo ni pamoja na mkopo maalumu wa shilingi trilioni moja, pamoja na sera wezeshi za kibajeti sambamba na ongezeko la mahitaji ya mikopo kwenye sekta ya kilimo kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji. Aidha, shughuli binafsi zimeendelea kuchukua sehemu kubwa ya mikopo kwa sekta binafsi, ikifuatiwa na biashara, kilimo na uzalishaji viwandani. **Kielelezo Na. 1.6** kimeainisha mchanganuo wa mikopo kwa sekta binafsi.

Kielelezo Na. 1.6: Mwenendo wa Mikopo kwa Sekta Binafsi



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

1.2.5.3 Viwango vya Riba

21. Riba za mikopo zilipungua na kufikia wastani wa asilimia 15.27 mwezi Novemba 2025 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 15.67 Novemba 2024 (**Kielelezo Na. 1.7**). Aidha, katika kipindi cha miezi mitano ya kwanza ya mwaka 2025/26 riba za mikopo zilipungua na kufikia wastani wa asilimia 15.18 ikilinganishwa na asilimia 15.49 katika kipindi kama hicho mwaka 2024/25. Mwenendo huu unaakisi utekelezaji madhubuti wa sera ya fedha pamoja na hatua nyingine zilizochukuliwa na Benki Kuu katika kuhakikisha kunakuwa na ukwasi wa kutosheleza shughuli za kiuchumi na kuchochea ongezeko la ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi.

Kielelezo Na. 1.7: Riba za Mikopo



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

22. Wastani wa riba za amana uliongezeka na kufikia asilimia 8.54 Novemba 2025, ikilinganishwa na asilimia 8.18 Novemba 2024. Ongezeko hilo lilitokana na jitihada za mabenki kuvutia amana kwa kutoa riba shindani. Aidha, katika kipindi cha miezi mitano ya kwanza ya mwaka 2025/26 wastani wa riba za amana ulikuwa asilimia 8.57 ikilinganishwa na asilimia 8.15 katika kipindi kama hicho mwaka 2024/25 (**Kielelezo Na. 1.8**). Kwa kuzingatia mwenendo huo, wigo kati ya riba za mikopo na amana za mwaka mmoja (*interest rate spread*) ulipungua hadi asilimia 5.51 Novemba 2025 kutoka asilimia 5.93 mwaka 2024.

Kielelezo Na. 1.8: Riba za Amana



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

1.2.5.4 Huduma Jumuishi za Fedha

23. Serikali kwa kushirikiana na wadau wa sekta binafsi, imeendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Fedha wa 2023 – 2028. Mpango huo unalenga kutatua changamoto za huduma jumuishi za fedha na kuhakikisha kuwa walengwa wote wanafikiwa na kutumia bidhaa na huduma za fedha zenye ubora ili kuboresha ustawi wa maisha yao ya kila siku. Katika kuhakikisha malengo ya Mpango yanafikiwa, Serikali imeendelea kuboresha mazingira wezeshi ya kuongeza upatikanaji na utumiaji wa huduma za fedha nchini; kutoa elimu ya fedha kwa makundi mbalimbali ikiwemo wanawake, vijana, wajasiriamali wadogo na wa kati na watu wenye mahitaji maalumu; na kuhamasisha watoa huduma za fedha kubuni huduma na bidhaa za sekta ya fedha zinazokidhi matakwa ya mahitaji ya makundi mbalimbali katika jamii.

1.2.5.5 Ukwasi na Faida katika Benki za Biashara

24. Hali ya ukwasi katika sekta ya benki iliendelea kuwa ya kuridhisha, ikiwa juu ya ukomo unaokubalika kisheria. Uwiano kati ya mali inayoweza kubadilishwa kuwa fedha taslimu na amana zinazoweza kuhitajika kwa muda mfupi (Liquid Assets to Demand Liabilities) ulikuwa asilimia 28.3 mwezi Novemba 2025 ikilinganishwa na asilimia 27.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2024, kiwango ambacho ni zaidi ya uwiano wa chini unaohitajika kisheria wa asilimia 20. Aidha, uwiano wa mtaji wa msingi na rasilimali za benki ilikuwa asilimia 18.7 mwezi Novemba 2025 kama ilivyokuwa Novemba 2024. Uwiano huo ni zaidi ya ukomo wa chini unaokubalika kisheria wa asilimia 10. Hii inaashiria kuwa benki zina ukwasi wa kutosha kwa ajili ya shughuli zake za kila siku ikiwemo kutoa mikopo.

25. Mapato ya benki yatokanayo na rasilimali (Returns on Asset - ROA) yalikuwa asilimia 4.9 mwezi Novemba 2025, ikilinganishwa na asilimia 5.3 mwezi Novemba 2024. Aidha, mapato yatokanayo na mtaji (Returns on Equity - ROE) yalifikia wastani wa asilimia 22.2 mwezi Novemba 2025 kutoka asilimia 24.1 kipindi kama hicho mwaka 2024. Hali hii inaashiria sekta ya benki inaendelea kuwa himilivu na yenye kutengeneza faida..

1.2.5.6 Mikopo Chechefu

26. Mikopo chechefu ilipungua na kufikia asilimia 3.1 mwezi Novemba, 2025, ikilinganishwa na asilimia 3.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Kupungua kwa mikopo chechefu kulitokana na hatua mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali kwa kushirikiana na Benki Kuu zikiwemo: Kutoa maelekezo kwa benki kuendelea kutumia kanzidata ya taarifa za wakopaji (credit reference system) katika utoaji wa mikopo; kuimarisha mifumo ya udhibiti wa benki; benki kuendelea kuimarisha viwango vya uchambuzi wa maombi ya mikopo; kusimamia maadili ya wafanyakazi wa benki; na kufanya ukaguzi maalum wa wafanyakazi (staff audit) wa benki mara kwa mara. Lengo

la hatua hizi ni kuhakikisha kiwango cha mikopo chechefu kinaendelea kuwa chini ya wastani wa asilimia 5.0.

1.2.5.7 Huduma Ndogo za Fedha (Microfinace)

27. Huduma ndogo za fedha zina mchango mkubwa katika upatikanaji na utumiaji wa huduma za fedha nchini. Huduma hizi zimewezesha wajasiriamali wadogo na wa kati kupata mitaji ya kugharamia shughuli za maendeleo na hivyo kujikwamua na umaskini. Hadi Juni 2025, watoa huduma ndogo wa daraja la pili waliopewa leseni na Benki Kuu ya Tanzania walifikia 2,626 kutoka watoa huduma 1,951 katika kipindi kama hicho mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 34.6. Aidha, watoa huduma ndogo za fedha daraja la pili walitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 1,317.1 mwaka 2024/25 ikilinganishwa na shilingi bilioni 718.13 mwaka 2023/24, sawa na ongezeko la asilimia 83.4.

28. Kwa upande mwingine, watoa huduma wa daraja la tatu (SACCOS) waliopewa leseni na Tume ya Maendeleo ya Ushirika walifikia 984 Juni 2025 ikilinganishwa na leseni 937 zilizotolewa katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Vilevile, watoa huduma wa daraja la nne (Vikundi vya Kifedha vya Kijamii) waliosajiliwa na Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa waliongezeka hadi 67,098 Juni 2025 kutoka watoa huduma 53,448 katika kipindi kama hicho mwaka 2024.

1.2.5.8 Mwenendo wa Soko la Hisa

29. Hadi Juni 2025, mtaji wa jumla wa Soko la Hisa la Dar es Salaam ulikuwa shilingi bilioni 19,638.8 ikilinganishwa na shilingi bilioni 16,834.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 16.7. Hali hii ilitokana na kuongezeka kwa bei ya hisa za baadhi ya kampuni zilizoorodheshwa katika Soko la Hisa. Aidha, mauzo ya hisa yalikuwa shilingi bilioni 407.5 ikilinganishwa na shilingi bilioni 272.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 49.4. Hii ilitokana na kuongezeka kwa ushiriki wa wawekezaji kulikochangiwa na elimu ya uwekezaji inayoendelea kutolewa na Serikali kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya fedha.

1.2.5.9 Huduma za Bima

30. Mwaka 2024, mwenendo wa soko la bima nchini ulikuwa wa kuridhisha ukichagizwa na kuimarishwa kwa mifumo ya usimamizi, mageuzi ya kidijitali, miongozo mipya ya udhibiti na uboreshaji wa huduma kwa wateja na wanufaika, kuanza kwa utekelezaji wa kanuni za Bima ya Afya kwa Wote na elimu ya bima. Thamani ya ada za bima (Gross Premium Written – GPW) ilikuwa shilingi trilioni 1.52 ikilinganishwa na shilingi trilioni 1.24 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 20.2. Mchanganuo wa mauzo ya ada za bima (GPW) kwa mwaka 2024 ulionesha kuwa bima za kawaida zilichangia asilimia

63.0, bima za maisha asilimia 20.0, bima za afya asilimia 12.0, bima ya takaful asilimia 0.3 na bima mtawanyo (reinsurance) asilimia 4.7.

31. Idadi ya watoa huduma waliosajiliwa iliongezeka kwa asilimia 26.4 na kufikia 1,741 mwaka 2024. Ongezeko hilo lilichangiwa na kuongezeka kwa watoa huduma waliosajiliwa kutoka katika kada za afya na karakana za magari. Aidha, idadi ya wakatabima na wanufaika wa huduma za bima iliongezeka kwa asilimia 10.2 na kufikia milioni 25.9 mwaka 2024. Vilevile, uwekezaji uliofanywa na kampuni za bima uliongezeka hadi shilingi trilioni 1.41 ikilinganishwa na shilingi trilioni1.27 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 10.3.

1.2.5.10 Viwango vya Ubadilishaji Fedha

32. Mwenendo wa thamani ya shilingi dhidi ya sarafu nyingine duniani ulibadilika kuendana na hali ya ukwasi wa fedha za kigeni nchini sambamba na mwenendo wa uchumi wa Dunia, misimu ya mauzo ya mazao ya biashara na dhahabu nje ya nchi pamoja na shughuli za utalii. 36. Katika kipindi cha miezi mitano ya kwanza ya mwaka 2025/26 thamani ya shilingi dhidi ya sarafu za nchi washirika wakuu wa kibiashara iliendelea kuwa imara. Mwenendo huo ulitokana na kuimarika kwa uchumi wa dunia na kuongezeka kwa mapato ya fedha za kigeni kutokana na shughuli za utalii na mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi. Vilevile, mabadiliko ya Kifungu cha 26 cha Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania kinachozuia matumizi ya fedha za kigeni katika miamala ya ndani, ulichangia kupunguza mahitaji ya fedha za kigeni nchini. Kutokana na hali hii, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,444.81 mwezi Novemba 2025, ikilinganishwa na shilingi 2,659.03 katika kipindi kama hicho mwaka 2024, sawa na ongezeko la thamani ya shilingi kwa asilimia 8.1, kwa mwaka.

1.2.5.11 Akiba ya Fedha za Kigeni

33. Hadi Novemba 2025, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za Marekani milioni 6,432.9 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 5,056.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Kiasi hicho kinatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi 4.9, juu ya lengo la nchi la kutosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kwa kipindi cha angalau miezi minne (4). Ongezeko hilo lilichangiwa na utekelezaji thabiti wa programu ya Benki Kuu ya ununuzi wa dhahabu nchini, pamoja na kuongezeka kwa mapato ya fedha za kigeni yatokanayo na mauzo ya dhahabu, korosho na kuimarika kwa shughuli za utalii nchini.

1.2.6 Sekta ya Nje

34. Sekta ya nje imeendelea kuimarika sambamba na kuimarika kwa uchumi wa dunia. Katika kipindi cha Julai hadi Novemba 2025, nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamishaji mali nje ya nchi ilipungua na kufikia dola za Marekani milioni 433.1 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani

milioni 632 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Mwenendo huu ulitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi, hususan mapato yatokanayo na utalii na mauzo ya bidhaa zisizo asilia sambamba na kasi ndogo ya uagizaji wa bidhaa nje ya nchi.

35. Katika kipindi cha Julai hadi Novemba 2025, thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma iliongezeka hadi dola za Marekani milioni 8,316.9 kutoka dola za Marekani milioni 7,728.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 7.6. Aidha, thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje iliongezeka kwa kasi ndogo ya asilimia 2.4 na kufikia dola za Marekani milioni 7,929.9 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 7,742.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. **Jedwali Na. 1.2** linaonesha mwenendo wa urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamishaji mali nje ya nchi.

Jedwali Na. 1.2: Mwenendo wa Urari wa Biashara ya Bidhaa, Huduma na Uhamishaji Mali Nje ya Nchi

(Dola za Marekani Milioni)

	Julai - Novemba		
	2024	2025	Ukuaji
Urari wa bidhaa	-1,708.2	-1,620.6	-5.1%
Zilizouzwa nje	4,664.2	4,928.9	5.7%
Zilizonunuliwa nje	-6,372.4	-6,549.4	2.8%
Urari wa huduma	1,694.2	2,007.6	18.5%
Mapato	3,064.3	3,388.1	10.6%
Malipo	-1,370.0	-1,380.5	0.8%
Urari wa bidhaa na huduma	-13.9	387.0	-2879.4%
Bidhaa na huduma zilizouzwa nje	7,728.5	8,316.9	7.6%
Bidhaa na huduma zilizonunuliwa kutoka nje	-7,742.4	-7,929.9	2.4%
Urari wa malipo wa vitega uchumi	-816.6	-892.3	9.3%
Yaliyoingia	121.4	194.0	59.8%
Yaliyotoka	-938.0	-1,086.4	15.8%
Urari wa uhamisho mali ya kawaida	198.5	72.2	-63.6%
Iliyoingia	445.5	346.1	-22.3%
ambapo Serikali	23.2	16.5	-29.0%
Iliyotoka	-247.0	-273.9	10.9%
Urari wa Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali	-632.0	-433.1	-31.5%

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

1.2.6.1 Mwenendo wa Biashara ya Bidhaa

36. Katika kipindi cha Julai hadi Novemba 2025, thamani ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 5.7 na kufikia dola za Marekani milioni 4,928.9, ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2024. Ongezeko hilo lilichangiwa zaidi na mauzo ya dhahabu, bidhaa za viwandani na tumbaku.

37. Katika kipindi cha Julai hadi Novemba 2025, thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje ya nchi iliongezeka hadi dola za Marekani milioni 6,549.4 kutoka dola za Marekani milioni 6,372.4 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 2.8. Hii ilichangiwa zaidi na ongezeko la uagizaji wa

mashine na bidhaa za matumizi ya kawaida. Aidha, thamani ya uagizaji wa bidhaa za petroli iliongezeka kwa kiasi kidogo cha asilimia 2.8 kufikia dola za Marekani milioni 1,136.5 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,106.5. Hii ilichangiwa na kupungua kwa bei ya mafuta katika soko la dunia, wakati kiasi cha uagizaji kiliongezeka.

1.2.6.2 Mwenendo wa Biashara ya Huduma

38. Katika kipindi cha Julai hadi Novemba 2025, mapato yatokanayo na huduma nje ya nchi yaliongezeka kufikia dola za Marekani milioni 3,388.1 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 3,064.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2024, sawa na ongezeko la asimia 10.6. Ongezeko hilo lilitokana na kukua kwa mapato ya utalii na usafirishaji. Aidha, ongezeko hilo lilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa idadi ya watalii walioingia nchini. Watalii walioingia nchini walifikia 1,101,036 katika kipindi cha Julai hadi Novemba 2025 ikilinganishwa na watalii 978,880 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Idadi hii inajumuisha watalii walioingia nchini kwa ajili ya matibabu, mikutano, pamoja na waliokuja kutembelea vivutio vya utalii nchini.

39. Katika kipindi cha Julai hadi Novemba 2024, malipo ya huduma nje ya nchi yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 1,380.5 kutoka dola za Marekani milioni 1,370 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 0.8. Hii ilitokana na kuongezeka kwa malipo ya huduma za usafirishaji sambamba na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi.

1.2.6.3 Uwekezaji wa Moja kwa Moja Kutoka Nje (FDI)

40. Uwekezaji wa Moja kwa Moja Kutoka Nje (Foreign Direct Investment) umeendelea kuimarika, ambapo mwaka 2023 uliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 1,648.2 kutoka dola za Marekani milioni 1437.0 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 14.7. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mikopo baina ya makampuni (intercompany loans), ambapo mchango wake katika jumla FDI ulikuwa asilimia 43.1 mwaka 2023 kutoka asilimia 8.7 mwaka 2022. Mwenendo huu unaakisi juhudi za Serikali katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini.

1.2.7 Deni la Serikali

41. Hadi Novemba 2025, Deni la Serikali lilikuwa shilingi bilioni 109,012.72 ikilinganishwa na shilingi bilioni 100,352.49 katika kipindi kama hicho mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 8.63. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani lilikuwa shilingi bilioni 38,181.30 (sawa na asilimia 35 ya deni lote) na deni la nje lilikuwa shilingi bilioni 70,831.42. Ongezeko la deni limetokana na Serikali kuendelea kupokea fedha za mikopo kutoka vyanzo mbalimbali kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege, umeme na maji.

1.2.7.1 Tathmini ya Uhimilivu wa Deni

42. Matokeo ya tathmini ya Uhimilivu wa Deni iliyofanyika Oktoba 2025 yalionesha kuwa deni limeendelea kuwa himilivu kwa kipindi cha muda wa kati na mrefu. Tathmini hiyo huzingatia vigezo vya uhimilivu ambavyo ni pamoja na uwiano wa deni halisi kwa Pato la Taifa, uwiano wa deni halisi kwa malipo ya nje na uwiano wa malipo ya deni kwa mapato ya ndani na mapato yatokanayo na mauzo ya nje.

43. Viashiria vya deni vilionesha kuwa: mwaka 2024/25 thamani ya sasa ya deni la nje kwa Pato la Taifa ni asilimia 24.9 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 40; thamani ya sasa ya deni la nje kwa mauzo ya nje ni asilimia 125.4 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 180; ulipaji wa deni la nje kwa kutumia mapato yatokanayo na mauzo ya nje ni asilimia 11.6 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 15; na ulipaji wa deni la nje kwa kutumia mapato ya ndani ni asilimia 14.7 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 18. Aidha kwa upande wa viashiria vya deni lote (deni la nje na la ndani), thamani ya deni kwa Pato la Taifa ni asilimia 40.7 ukilinganisha na ukomo wa asilimia 55 (**Jedwali Na. 1.3)**. Katika kuhakikisha kuwa Deni la Serikali linaendelea kuwa himilivu, Serikali inatekeleza mikakati ifuatayo:

(i) Kuhakikisha mikopo inayopewa kipaumbele ni ile yenye masharti nafuu kadri inavyopatikana. Mikopo yenye masharti ya kibiashara itaelekezwa katika miradi inayochochea kasi ya ukuaji wa uchumi na mauzo nje ya nchi;

(ii) Kuimarisha utekelezaji wa mikakati ya ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kuhakikisha sehemu kubwa ya bajeti inagharamiwa na mapato ya ndani pamoja na kupunguza matumizi yanayoweza kuepukika bila kuathiri uendeshaji wa shughuli za Serikali;

(iii) Kusimamia utoaji wa dhamana kwa mashirika ya Umma. Hatua hii itasaidia kutokuongeza deni linalotokana na taasisi hizo kushindwa kulipa madeni; na

(iv) Kuendeleza mabadiliko ya kimuundo katika uchumi, na kutumia nafasi nzuri ya kijiografia ya nchi kuongeza mauzo ya nje na ushindani wa biashara ili kuongeza mapato ya fedha za kigeni.

Jedwali Na. 1.3: Tathmini ya Uwiano wa Viashiria vya Deni la Taifa (Thamani ya sasa ya deni)

Tathmini Deni la nje	**Ukomo**	**2024 /25**	**2025 /26**	**2026 /27**	**2027 /28**	**2028 /29**	**2029 /30**	**2030 /31**	**2035 /36**
Uwiano deni kwa pato la Taifa	40	24.9	24.4	23.6	22.4	21.1	20.0	19.5	18.0
Uwiano deni kwa mauzo ya nje	180	125.4	123.1	123.8	119.3	114.3	110.4	108.2	103.0
Malipo ya deni kwa mauzo ya nje	15	11.6	12.8	12.2	13.7	13.3	13.1	12.0	10.2
Uwiano malipo ya deni kwa makusanyo ya ndani	18	14.7	15.4	13.8	15.1	14.3	13.9	12.9	10.6
Tathmini Deni la Umma									
Uwiano deni kwa Pato la Taifa	55	40.7	39.6	38.6	36.9	35.9	34.8	34.6	34.7

1.2.7.2 Tathmini ya Uwezo wa Nchi Kukopesheka

44. Mwaka 2024/25, Tanzania ilifanyiwa tathmini ya kukopesheka katika masoko ya mitaji ya kimataifa na kampuni za Moody’s Investors Service na Fitch Ratings, ambapo matokeo yanaonesha nchi kuendelea kuwa na mwelekeo imara kwa kutunukiwa daraja B1 na B+ mtawalia. Matokeo mazuri ya tathmini hizo yanaakisi uhimilivu wa deni la serikali kutokana na ukuaji mzuri wa uchumi unaoweza kuhimili majanga ya kimataifa, utekelezaji wa mageuzi ya kimuundo yanayoboresha mazingira ya biashara, ufanisi wa ukusanyaji wa mapato na usimamizi wa fedha za umma.

Kiambatisho Na. 1B

2 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2024/25

2.1 Utangulizi

45. Mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/25 yamefanyika katika maeneo ya ukusanyaji wa mapato na matumizi ya Serikali ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kuzingatia malengo na shabaha za bajeti. Aidha, maelezo ya kina ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo yanapatikana katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2026/27.

2.2 Mapato na Matumizi

46. Katika mwaka 2024/25, Serikali ilikadiria kukusanya na kutumia shilingi bilioni 50,291.4 ambapo jumla ya shilingi bilioni 49,821.2 zilikusanywa sawa na asilimia 99.1 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kiasi hiki kinajumuisha shilingi bilioni 34,845.9 mapato ya ndani, sawa na asilimia 100.7 ya lengo la mwaka la shilingi bilioni 34,610.6; shilingi bilioni 5,075.1 ni misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, sawa na asilimia 83.5 ya lengo la shilingi bilioni 6,076.3; na shilingi bilioni 9,900.3 ni mikopo ya kibiashara ya ndani na nje ya nchi, sawa na asilimia 103.1 ya lengo la mwaka la shilingi bilioni 9,604.1. Mafanikio haya yametokana na utekelezaji madhubuti wa sera ya fedha na bajeti pamoja na usimamizi wa utekelezaji wa Mkakati wa Mashirikiano na Washirika wa Maendeleo – DCF hususan upatikanaji wa misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

47. Katika mwaka 2024/25, Serikali ilitoa ridhaa ya matumizi ya jumla ya shilingi bilioni 49,821.2, sawa na asilimia 99.1 ya bajeti. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 34,418.4 zilitolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikiwemo mishahara ya watumishi wa umma, ugharamiaji wa deni la Serikali na uendeshaji wa shughuli za Serikali. Aidha, shilingi bilioni 15,402.7 zilitolewa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. **Jedwali Na. 2.1** linaonesha mchanganuo wa makadirio ya mapato na matumizi pamoja na ufanisi katika eneo la mapato na matumizi.

Jedwali Na. 2.1: Mchanganuo wa Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2024/25 (Shilingi bilioni)

	BAJETI	HALISI	UFANISI
Mapato ya ndani	34,610,646	34,845,867	100.7%
TRA	29,415,289	30,095,736	102.3%
Mapato yasiyo ya kodi (MDAs)	3,839,017	3,312,853	86.3%
Mapato ya Halmashauri	1,356,341	1,437,278	106.0%
Misaada	794,390	880,052	110.8%
Mikopo nafuu	5,281,943	4,194,993	79.4%
Mikopo ya kibiashara nje	2,986,638	2,410,774	80.7%
Mikopo ya kibiashara ndani	6,617,790	7,489,466	113.2%
Kulipa mtaji	4,022,373	4,087,193	101.6%
Kugharamia bajeti (NDF)	2,595,417	3,402,273	131.1%
JUMLA YA MAPATO	**50,291,408**	**49,821,151**	**99.1%**
JUMLA YA MATUMIZI	**50,291,408**	**49,821,151**	**99.1%**
Matumizi ya kawaida	34,937,808	34,418,429	98.5%
Mishahara	11,767,987	11,238,563	95.5%
Deni la Serikali	13,121,466	12,461,866	95.0%
Matumizi mengine	10,048,356	10,718,000	106.7%
Matumizi ya maendeleo	15,353,600	15,402,723	100.3%
Ndani	11,712,762	12,715,894	108.6%
Nje	3,640,838	2,686,829	73.8%

Chanzo: *Wizara ya Fedha*

2.3 Mafanikio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2024/25

48. Utekelezaji wa mpango na bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/25 umekuwa na mafanikio makubwa katika ukusanyaji wa mapato ya ndani na utekelezaji wa miradi na shughuli katika sekta mbalimbali kama ifuatavyo:

a) Ukusanyaji wa mapato ya ndani

49. Kwa mwaka 2024/25, Serikali imefanikiwa kufikia na kuvuka lengo la makusanyo ya mapato ya ndani kwa ufanisi wa asilimia 100.7 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 34,845.9. Mafanikio haya yamechochewa na ufanisi wa asilimia 102.3 na asilimia 105.9 uliofikiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania na Mamlaka za Serikali za Mitaa mtawalia. Ufanisi uliofikiwa ni matokeo ya: uhiari wa ulipaji kodi kupitia uboreshwaji wa huduma na mahusiano na walipakodi; uboreshwaji wa mifumo ya TEHAMA ya ukusanyaji

mapato nchini ikiwemo kuunganishwa kwa mifumo ya ukusanyaji; uboreshwaji wa mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji nchini kupitia majadiliano katika majukwaa mbalimbali ikiwemo Baraza la Biashara la Taifa; na kutekeleza mikakati na kampeni mbalimbali za uhamasishaji uhiari wa ulipaji kodi, elimu ya umuhimu wa kodi kwa maendeleo ya nchi na matumizi sahihi ya risiti za kielektroniki za EFD.

b) Sekta ya Uchukuzi

50. Katika mwaka 2024/25, Sekta ya Uchukuzi iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 2,117.5 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo kiasi cha shilingi bilioni 1,687.6 zilitolewa, sawa na asilimia 79.7 ya bajeti iliyoidhinishwa. Miradi ya maendeleo iliyotekelezwa katika kipindi hicho inajumuisha:

(i) **Ujenzi na uendeshaji wa Reli ya Kisasa ya *Standard Gauge Railway* (SGR):** Ujenzi wa reli ya SGR unaendelea katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo; Dar es Salaam – Morogoro (km 300) asilimia 99.83 ikilinganishwa na asilimia 99.15 katika mwaka 2023/24, Morogoro – Makutupora (km 422) asilimia 98.30 ikilinganishwa na asilimia 96.89 katika mwaka 2023/24; Mwanza – Isaka (km 341) asilimia 64.16 ikilinganishwa na asilimia 59.29 katika mwaka 2023/24, Makutupora – Tabora (km 371) asilimia 14.54 ikilinganishwa na asilimia 14.44 katika mwaka 2023/24, Tabora – Isaka (km 165) asilimia 7.41 ikilinganishwa na asilimia 5.91 katika mwaka 2023/24, na Tabora – Kigoma (km 506) asilimia 8.00 ikilinganishwa na asilimia 5.84 katika mwaka 2023/24. Pamoja na hatua hizo, Serikali imefanikiwa kuanza uendeshaji wa SGR kwa Dar es Salaam – Dodoma, ambapo jumla ya abiria 3,047,232 walisafirishwa na kiasi cha shilingi bilioni 89.55 kilikusanywa.

(ii) **Uboreshaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL):** Hatua iliyofikiwa ni pamoja na; kukamilika kwa ununuzi wa ndege moja aina ya Boeing 787-8 Dreamliner ambayo iliwasili nchini Agosti 2024, pamoja na kuendelea na ukarabati na uboreshaji wa karakana za matengenezo ya ndege zilizopo katika viwanja vya ndege vya kimataifa vya JNIA na KIA ambapo awamu ya kwanza ya ukarabati wa karakana ya matengenezo JNIA umekamilika na KIA umefikia asilimia 80. Jumla ya shilingi bilioni 356.16 zilitumika. Maboresho yaliyofanyika yameiwezesha ATCL kuongeza mtandao wa safari kwa kurejesha safari zake katika vituo vya Mtwara, Iringa na Johannesburg, hivyo kuwa na jumla ya vituo 27 vya ndani na nje ya nchi. Vilevile, maboresho hayo yamewezesha kuongezeka kwa idadi ya abiria waliosafirishwa kufikia abiria 1,178,025 ikilinganishwa na abiria 1,123,696 waliosafirishwa katika mwaka 2023/24.

(iii) **Ujenzi na Ukarabati wa Viwanja vya Ndege**: Serikali ilikamilisha ujenzi wa njia ya kurukia ndege (runway) katika Kiwanja cha Ndege cha Iringa, ujenzi wa jengo jipya la abiria na mifumo ya TEHAMA katika Kiwanja cha Ndege cha Arusha

pamoja na mifumo ya usimamizi wa taarifa za viwanja vya ndege katika viwanja vya JNIA, KIA, Arusha, Bukoba, Dodoma na Songwe. Aidha, ujenzi wa uzio wa usalama katika Kiwanja cha Ndege cha Geita umefikia asilimia 65; Ujenzi wa jengo jipya la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Mwanza umefikia asilimia 15; maboresho ya jengo la mizigo katika Kiwanja cha Ndege cha Mwanza umefikia asilimia 7; Upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Moshi umefikia asilimia 69; na Ufungaji wa mfumo wa Taa za kuongozea Ndege (AGL) katika Kiwanja cha Ndege Arusha umefikia asilimia 10.

Miradi mingine inayoendelea kutekelezwa ni ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Msalato, ambapo kazi za Package I (miundombinu) ilifikia asilimia 95.95 na Package II (majengo) ilifikia asilimia 62.98; Ukarabati na upanuzi wa kiwanja cha Ndege cha Musoma umefikia asilimia 60; Ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kigoma Awamu ya III umefikia asilimia 16; Ukarabati na upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Sumbawanga umefikia asilimia 70; Ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga upo asilimia 83.50; Ukarabati na Upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Tabora Awamu ya III umefikia asilimia 94; na umaliziaji wa jengo la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Songea umefikia asilimia 70. Jumla ya shilingi bilioni 172.13 zilitumika.

(iv) **Ujenzi na Ukarabati wa Meli katika Maziwa Makuu:** Hatua iliyofikiwa ni pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa Meli ya MV Mwanza katika Ziwa Victoria. Aidha, ukarabati wa Meli ya MT Sangara katika Ziwa Tanganyika umekamilika na inaendelea kusafirisha shehena ya mafuta baina ya Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC). Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na ukarabati wa Meli ya MV Liemba ambao umefikia asilimia 32, ukarabati wa Meli ya MV Ukerewe ambao umefikia asilimia 43 na hatua za awali kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha kujengea meli katika Ziwa Tanganyika zinaendelea. Jumla ya shilingi bilioni 75.14 zilitumika.

(v) **Uboreshaji wa Rada na Vifaa vya Hali ya Hewa**: Serikali imeendelea kuboresha miundombinu, rada na vifaa vya hali ya hewa ambapo katika mwaka 2024/25, uboreshaji (upgrading) wa rada mbili (2) za Dar es Salaam na Mwanza umekamilika na kuwezesha rada hizo kuendana na teknolojia ya kisasa katika uendeshaji na utoaji wa taarifa za hali ya hewa. Hatua hii imeongeza uwezo na ufanisi katika utoaji wa huduma za hali ya hewa na kuendelea kuzingatia viwango vya kimataifa ambapo usahihi wa utabiri wa hali ya hewa umefikia asilimia 88.2. Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni ufungaji, ukarabati na uboreshaji wa vituo vya hali ya hewa pamoja na mifumo ya TEHAMA. Jumla ya shilingi bilioni 8.86 zilitumika.

(vi) **Uboreshaji wa Bandari**: Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya uboreshaji wa bandari nchini zikiwemo bandari za Maziwa Makuu na Bahari ya Hindi. Hatua

iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ujenzi na upanuzi wa Bandari ya Bukoba; kukamilika kwa ujenzi wa Bandari ya Kemondo; ujenzi wa Bandari Kavu ya Kwala umefikia asilimia 96.6; ujenzi wa Bandari ya Mwanza North (asilimia 68); ujenzi wa gati katika Bandari ya Kibirizi (asilimia 99); na ujenzi wa Bandari ya Mbambabay (asilimia 36). Aidha, Serikali kupitia Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) ipo katika hatua za awali za uboreshaji wa Gati la Malindi katika Bandari ya Dar es Salaam (asilimia 5), ujenzi wa Bandari ya Kisiwa Mgao (asilimia16), ujenzi wa mantanki 15 ya mafuta (asilimia 28), na ujenzi wa Bandari ya Kigoma (asilimia 2.5). Jumla ya shilingi bilioni 334.3 zilitumika. Vilevile, Maboresho ya miundombinu na mifumo ya bandari yamewezesha kuongezeka kwa shehena ya mizigo iliyohudumiwa katika bandari za Tanzania kufikia tani milioni 32.75 ikilinganishwa na tani milioni 27.55 katika mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la asilimia 18.9.

c) Sekta ya Nishati

51. Katika mwaka 2024/25, Sekta ya Nishati iliidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 1,883.8 ambapo shilingi bilioni 1,275.7 zilitolewa sawa na asilimia 68 ya bajeti iliyoidhinishwa. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

(i) **Miradi ya Kuzalisha Umeme:** Utekelezaji wa mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (JNHPP) – MW 2,115 umefikia asilimia 99.98 ambapo jumla ya Megawati 2,115 za umeme zinazalishwa kupitia mitambo tisa (9). Aidha, Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Jua - Shinyanga wa Megawati 150 unaendelea, ambapo awamu ya kwanza ya utekelezaji inayohusisha uzalishaji wa Megawati 50 imefikia asilimia 80. Vilevile, mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maji wa Malagarasi (Megawati 49.5) umefikia asilimia 54.9. Hatua hizi ziliwezesha kuongezeka kwa uwezo wa mitambo ya kufua umeme iliyounganishwa katika mfumo wa Gridi ya Taifa na kufikia Megawati 4,352.13 Juni, 2025 ikilinganishwa na Megawati 2,372.96 za Juni, 2024 sawa na ongezeko la asilimia 83.5. Jumla ya shilingi bilioni 328.58 zilitumika.

(ii) **Mradi wa Kuimarisha Gridi ya Taifa:** Mradi huu ni wa uimarishaji wa miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme pamoja na vituo vya kupoza umeme katika mikoa yote ambapo umefikia asilimia 51.8 kwa awamu ya kwanza. Mradi huu umeimarisha usafirishaji na upatikanaji wa umeme nchini. Jumla ya shilingi bilioni 266.11 zilitumika.

(iii) **Mradi wa usambazaji umeme Vijijini:** Mradi umewezesha usambazaji wa umeme katika vijiji 12,318 sawa na lengo la mradi na vitongoji 37,327 kati ya vitongoji 64,359 vya Tanzania Bara ambayo ni sawa na asilimia 58. Aidha, mradi umewezesha kuunganisha umeme katika taasisi na maeneo ya huduma 63,140,

ikiwemo vituo vya afya (2,658), taasisi za elimu (18,597), taasisi za biashara (26,988), nyumba za ibada (6,651) na pampu za maji (8,246). Hatua hizi zimeendelea kuchachusha shughuli za kiuchumi na kijamii katika maeneo ya vijijini. Jumla ya shilingi bilioni 332.38 zilitumika.

(iv) **Miradi ya Njia za Kusafirisha Umeme (Msongo wa kV 400):** Mradi wa Singida - Arusha - Namanga wenye urefu wa km 414 kupitia Babati na Arusha umekamilika na kuwezesha kuunganishwa kwa Gridi za Taifa za Tanzania na Kenya. Hatua hii inatoa fursa ya kufanyika kwa biashara ya umeme baina ya Tanzania na nchi za Afrika Mashariki ikiwa ni pamoja na kupitia EAPP. Aidha, Mradi wa Chalinze - Dodoma wenye urefu wa km 345 na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme vya Chalinze na Dodoma umefikia asilimia 18.1. Hatua hizi zilichangia kuongezeka kwa miundombinu ya usafirishaji wa umeme kufikia urefu wa jumla ya km 8,025.75 ikilinganishwa na km 7,745.4 mwaka 2024. Vilevile, kukamillika kwa mradi wa kusafirisha umeme wa Chalinze - Dodoma kutaimarisha usafirishaji na usambazaji wa umeme unaozalishwa katika Bwawa la Julius Nyerere kupitia kituo cha kupoza umeme huo cha Chalinze. Jumla ya shilingi bilioni 119.59 zilitumika.

(v) **Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia Nchini:** Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024 - 2034) umeendelea kutekelezwa ili kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2034, angalau asilimia 80 ya watanzania wawe wanatumia nishati safi ya kupikia. Ili kufikia azma hiyo, Mkakati umejikita katika kutoa elimu kwa wananchi kuhusu manufaa ya nishati safi ya kupikia katika kulinda afya na mazingira, kupunguza gharama za upatikanaji wa vifaa na teknolojia za nishati safi ya kupikia pamoja na kuwezesha na kurahisisha upatikanaji wa nishati na teknolojia hizo nchini. Serikali imekamilisha Mkakati wa Taifa wa Mawasiliano wa Nishati Safi ya Kupikia na imeendelea kutoa elimu kuhusu matumizi ya nishati hiyo kwa wananchi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, ikiwemo sekta binafsi. Aidha, ili kuimarisha matumizi ya nishati safi ya kupikia katika Taasisi za Umma hususan zinazohudumia zaidi ya watu 100, mifumo ya nishati safi ya kupikia imefungwa katika magereza 129, kambi za jeshi 22 na shule za sekondari 52. Vilevile, mitungi ya gesi 251,757 na majiko banifu 4,300 yamegawiwa kwa wananchi. Jumla ya shilingi milioni 700.00 zilitumika. Kutokana na hatua zilizochukuliwa, matumizi ya nishati safi ya kupikia nchini yameongezeka na kufikia asilimia 23.2 kutoka asilimia 6.9 ya mwaka 2021.

(vi) **Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Uganda hadi Tanzania *(EACOP):*** Serikali imekamilisha mchango wa mtaji wa shilingi bilioni 643.30 sawa na asilimia 15 ya hisa katika mradi wa EACOP. Utekelezaji wa mradi kwa ujumla umefikia asilimia 62.5 na kazi zilizokamilika ni pamoja na ujenzi wa nyumba 340 za makazi mbadala kwa wananchi 294 waliopoteza makazi yao,

ujenzi wa makambi na vituo vya kuhifadhia mabomba na kiwanda cha kuweka mfumo wa joto kwenye mabomba (Thermal Insulation System (TIS) Plant) ambacho kimeanza kazi ya kuweka mfumo ya kuhifadhi joto katika mabomba yenye urefu wa kilomita 890. Kati ya mabomba yaliyofanyiwa TIS, mabomba yenye urefu wa kilomita 460 yameshachomelewa tayari kwa ajili ya kuchimbiwa ardhini. Aidha, mabomba ya kuwezesha kujenga kilomita 1,391 yamefika nchini tayari kwa kuwekewa mfumo wa kuhifadhi joto. Vilevile, tayari fidia imelipwa kwa wananchi 9,863 kati ya 9,923 (asilimia 99.3) wanaopisha eneo la mkuza wa ujenzi wa mradi ambapo jumla ya Shilingi bilioni 35.06 zilitumika. Kazi zinazoendelea kutekelezwa kwa sasa ni pamoja na uchomeleaji wa matanki manne katika miundombinu ya kituo cha kupokelea na kuhifadhi mafuta cha Chongoleani (Marine Storage Terminal - MST) ambapo ujenzi wake umefikia asilimia 79.3, ujenzi wa kituo (terminal) umefikia asilimia 39 na ujenzi wa jeti ya kupakilia mafuta umefikia asilimia 85.2.

(vii) **Mradi wa kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika *(Liquefied Natural Gas – LNG)*:** Mradi huu unatekelezwa katika eneo la Likong'o mkoani Lindi na utahusisha usindikaji wa gesi asilia iliyogunduliwa katika Vitalu Na. 1, 2 na 4 vilivyopo katika kina kirefu cha bahari. Majadiliano baina ya Serikali na Wawekezaji kuhusu mradi huu unaotarajiwa kugharimu takribani dola za Marekani bilioni 42 yameendelea na yanatarajiwa kukamilika katika mwaka 2025/26 na hivyo kuwezesha hatua ya utekelezaji wa mradi kuanza. Jumla ya shilingi bilioni 5 zilitumika.

(viii) **Usambazaji wa Gesi Asilia:** Ujenzi wa vituo vya Gesi Asilia (*Compressed Natural Gas-CNG*) kwa ajili ya matumizi ya vyombo vya moto umeendelea ambapo tayari jumla ya vituo tisa (9) vinavyomilikiwa na Serikali pamoja na sekta binafsi vimejengwa hadi mwezi Juni 2025. Hatua hiyo imeimarisha matumizi ya CNG katika vyombo vya moto. Aidha, usambazaji wa gesi asilia kwa ajili ya matumizi ya viwandani, katika taasisi na majumbani umeendelea, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa bomba la gesi asilia kutoka Kinyerezi - Dar es Salaam hadi Chalinze – Pwani na usambazaji wa gesi asilia katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Lindi na Mtwara. Jumla ya shilingi bilioni 6 zilitumika.

(ix) **Utafutaji na Uendelezaji wa Mafuta na Gesi Asilia:** Utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia umeendelea katika vitalu vya Eyasi – Wembere, Songo Songo Magharibi, Lindi – Mtwara, Ruvuma (Eneo la Ntorya) na Vitalu 4/1B & 4/1C kwa kutekeleza kazi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kuchukua taarifa za mitetemo za mfumo wa 2D na 3D na kufanya tathmini za mazingira. Jumla ya shilingi bilioni 4 zilitumika.

d) Sekta ya Ujenzi

52. Katika mwaka 2024/25, Sekta ya Ujenzi iliidhinishiwa bajeti ya shilingi bilioni 2,448.02 ambapo shilingi bilioni 2,291.95 zilitolewa sawa na asilimia 93.62. Baadhi ya miradi ya kipaumbele iliyotekelezwa katika sekta hii ni pamoja na:

(i) **Ujenzi na Ukarabati wa Barabara na Madaraja kupitia TANROADS:** Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara kuu zenye urefu wa km 127.07 umekamilika na ujenzi wa km 257.93 za barabara na madaraja matano (5) unaendelea. Aidha, jumla ya km 29.09 za barabara za mikoa zilijengwa kwa kiwango cha lami na km 458.64 zilikarabatiwa kwa kiwango cha changarawe. Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na matengenezo ya kawaida (km 28,563.76), matengenezo ya muda maalum (km 2,336.73), matengenezo ya sehemu korofi (km 268.64) na matengenezo ya madaraja 2,463. Vilevile, ujenzi wa madaraja ya J. P Magufuli (Kigongo – Busisi) lenye urefu wa km 3.2, Mpwapwa na Kitengule pamoja na barabara ya Kidatu – Ifakara (km 68) ilikamilika. Pia, Serikali imeendelea na ujenzi wa barabara ya Mkange – Tungamaa – Pangani (km 170.8) ambao umefikia asilimia 45; Daraja la Pangani (m 525) umefikia asilimia 50; ujenzi wa madaraja mengine matatu (3) ya Simiyu (Mwanza) umefikia asilimia 37, Mbangala (Mtwara) umefikia asilimia 66 na Sukuma (Mwanza) umefikia asilimia 25. Afua hizi zimesaidia kupunguza adha ya usafiri na usafirishaji na kuhamasisha utalii. Jumla ya shilingi bilioni 149.82 zilitumika.

(ii) **Ujenzi na Ukarabati wa Barabara za Vijijini na Mijini kupitia TARURA:** Serikali kupitia TARURA iliendelea kutekeleza miradi ya kuboresha miundombinu ya barabara nchini. Hatua zilizofikiwa ni pamoja na ujenzi wa barabara za lami km 276.84 na barabara za changarawe km 3,405.17. Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na; Kukamilika kwa ujenzi na ukarabati wa madaraja 17, makalavati 262 na mifereji ya kuondoa maji ya mvua barabarani yenye urefu wa mita 46,772.39. Aidha, maabara tatu (3) za kupima ubora wa sampuli za ujenzi wa miundombinu ya barabara zilijengwa katika mikoa ya Pwani, Dar es Salaam na Rukwa na kufikia maabara 14. Jumla ya shilingi bilioni 659.62 zilitumika.

(iii) **Ujenzi wa Barabara kwa ajili ya Kupunguza Msongamano:** Serikali imeendelea na ujenzi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka katika Jiji la Dar es Salaam: City Center - Gongo la Mboto (km 23.3) asilimia 90.12; Maktaba ya Taifa - Mwenge/Ubungo (km 13.5) asilimia 24 na Mwenge - Tegeta (km 15.63) asilimia 29.92. Ujenzi wa Barabara ya Mzunguko katika Jiji la Dodoma (km 112.3) ambapo Lot 1 Nala - Veyula - Mtumba - Ihumwa Bandari Kavu (km 52.3) asilimia 83.12 na Lot 2 Ihumwa Bandari Kavu - Matumbulu - Nala (km 60)

asilimia 85.51; na upanuzi wa barabara ya Uyole - Ifisi - Songwe Airport Jijini Mbeya (km 36) umefikia asilimia 23. Jumla ya shilingi bilioni 255.90 zilitumika.

(iv) **Ujenzi na Ukarabati wa Vivuko:** Vivuko sita (6) vipo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Vivuko hivyo ni; Kisorya - Rugezi (asilimia 94.5), Bwiro - Bukondo (asilimia 94), Mafia - Nyamisati (asilimia 40.5), Ijinga - Kahangala (asilimia 91), Nyakariro- Kome (asilimia 90) na Buyagu - Mbalika (asilimia 88.5). Aidha, Serikali imekamilisha ukarabati wa vivuko vya Mv Ujenzi na Mv Mara na inaendelea na ukarabati wa vivuko vitatu (3) vya Mv Magogoni (asilimia 81.3), Mv Nyerere (asilimia 81) na Mv Kilombero II (asilimia 90). Jumla ya shilingi bilioni 6.09 zilitumika.

e) **Sekta ya Kilimo**

53. Katika mwaka 2024/25, Sekta ya Kilimo iliidhinishiwa shilingi bilioni 851.68, ambapo shilingi bilioni 375.24 zilitolewa sawa na asilimia 44.05. Shughuli za vipaumbele zilizotekelezwa ni pamoja na:

(i) **Uzalishaji wa Mazao ya Kilimo:** Uzalishaji wa mazao ya chakula katika msimu wa kilimo wa 2024/25 ulifikia tani 23,472,201 ikilinganishwa na tani 22,803,316 katika msimu wa kilimo wa 2023/24, sawa na ongezeko la asilimia 2.9. Uzalishaji wa chakula kwa msimu wa kilimo wa 2024/25 ulitosheleza mahitaji ya chakula ya tani 18,261,154 kwa mwaka 2025/26 na kuwepo kwa ziada ya tani 5,211,047. Kutokana na hali hiyo, Taifa limejitosheleza kwa chakula kwa asilimia 128.5. Ongezeko hilo limechangiwa na kuongezeka kwa matumizi ya mbolea ya ruzuku kutoka tani 622,054 mwaka 2023/24 hadi tani 802,372 mwaka 2024/25 na matumizi ya tani 9,639.63 za mbegu bora za mahindi za ruzuku. Vilevile, uzalishaji wa mazao asilia ya biashara umeongezeka kutoka tani 1,201,832.65 mwaka 2023/24 hadi tani 1,451,694.11 mwaka 2024/25 kulikochangiwa na matumizi ya pembejeo za kilimo na programu ya ugawaji wa miche bora iliyoanza kutekelezwa ndani ya miaka mitano (5) iliyopita. Jumla ya shilingi bilioni 114.60 zilitumika.

(ii) **Programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora (BBT):** Serikali imeendelea kutekeleza programu ya BBT katika mashamba ya Chinangali II (ekari 1,772) na Ndogowe (ekari 11,430) mkoani Dodoma. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na: vijana 686 (vijana wa kiume 431 na wa kike 255) wamepatiwa mashamba; uwekaji wa miundombinu ya umwagiliaji kwa njia ya matone katika eneo lenye ukubwa wa ekari 220 umefikia asilimia 80; ujenzi wa kituo cha kusindika zabibu chenye uwezo wa kusindika tani 300 na kuhifadhi mchuzi wa zabibu lita 220,000 kwa mwaka umekamilika; ujenzi wa nyumba 53 umekamilika na ujenzi wa nyumba nyingine saba (7) umefikia wastani wa asilimia 92; na usimikaji na utandazaji wa mfumo wa umwagiliaji kwa mabomba umefikia asilimia 65.

Wahitimu wa vyuo vya kilimo 1,243 (wanaume 745 na wanawake 498) wamepata ajira ya mkataba ya kutoa huduma za ugani katika mazao ya pamba na korosho, kuanzisha kituo atamizi cha kuzalisha bidhaa kwa kutumia singa za mkonge ambapo vijana 344 wanaendelea na mafunzo na mashine 66 zenye uwezo wa kubangua korosho kilo 20 kwa siku kwa kila moja zilisambazwa katika vikundi 12 vya wakulima. Jumla ya shilingi bilioni 19.67 zilitumika.

(iii) **Uendelezaji wa Kilimo cha Umwagiliaji:** Serikali imekamilisha ujenzi wa skimu mpya tatu (3) za Magurukenda - Buchosa (hekta 150), Sukuma - Buchosa (hekta 350) na Tlawi - Mbulu (hekta 350). Ujenzi wa skimu mpya 55 umefikia wastani wa asilimia 52. Aidha, ukarabati wa skimu saba (7) za Madibira - Mbarali (hekta 3,200), Mgambalenga - Kilolo awamu ya kwanza (hekta 3,000), Myamba - Same (hekta 1,470), Muhukuru - Songea (hekta 300), Idudumo - Nzega awamu ya kwanza (hekta 400), Mbaka - Busokelo (hekta 600) na Mtula - Mufindi (hekta 75) umekamilika na ukarabati wa skimu 41 umefikia wastani wa asilimia 60.

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na: kukamilika kwa ujenzi wa Bwawa la Tlawi (Mbulu) lenye mita za ujazo 1,100,000 na ukarabati wa Bwawa la Ulyanyama (Sikonge) lenye mita za ujazo 2,070,000. Ujenzi wa mabwawa 19 yenye mita za ujazo 326,449,973 umefikia wastani wa asilimia 57.2. Kadhalika, Serikali imenunua mitambo 18 ya kuchimba visima vya kati na virefu kwa ajili ya shughuli za umwagiliaji. Jumla ya shilingi bilioni 154.59 zilitumika.

f) Sekta ya Mifugo

54. Katika mwaka 2024/25, Sekta ya Mifugo iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 45.65 ambapo Shilingi bilioni 33.35 zilitolewa sawa na asilimia 73.06 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi. Miradi ya kipaumbele iliyotekelezwa ni pamoja na:

(i) **Kuimarisha Afya ya Mifugo:** Serikali imezindua Mpango wa Chanjo na Utambuzi wa Mifugo Kitaifa 2024/25 – 2029/30 unaolenga kudhibiti magonjwa ya mifugo nchini ili kupunguza hasara wanazozipata wafugaji kutokana na magonjwa; Nchi kupata ithibati kutoka Shirika la Afya ya Wanyama Duniani kama uthibitisho wa kufanya biashara salama na mataifa mengine; kuondoa vikwazo na kuiwezesha Tanzania kuingia katika masoko ya kikanda na kimataifa; na kupunguza matumizi ya madawa na hivyo kudhibiti usugu wa vimelea dhidi ya dawa.Aidha, pikipiki 700 kwa ajili ya zoezi la chanjo, vishikwambi 4,500 na dawa lita 56,000 za kuogesha mifugo zilinunuliwa. Jumla ya shilingi bilioni 11.8 zilitumika.

(ii) **Ujenzi wa Miundombinu ya Mifugo:** Kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa mabwawa manne (4) ya Bukabwa (Butiama), Kihumbu (Bunda), Isulamilomo (Nsimbo) na Kwenikwembe (Kilindi) kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa maji

kwa mifugo; ujenzi wa mbauti tatu (3) za kunyweshea mifugo katika Wilaya ya Mwanga; na uanzishwaji wa mashamba darasa manne (4) ya malisho katika Wilaya ya Longido (Lerang'wa, Sinya, Tingatinga na Olmolog). Aidha, shughuli nyingine zilizokamilika ni kujenga na kukarabati minada 51 ya mifugo ikijumuisha ya awali, upili na mipakani; kukamilisha ujenzi wa vituo vitano (5) vya kukusanyia maziwa na kuendelea na ujenzi wa vituo vingine vitano (5); na kukamilisha ujenzi wa majosho 746 katika mikoa yote 26 nchini. Jumla ya shilingi bilioni 6.4 zilitumika.

g) Sekta ya Uvuvi

55. Katika mwaka 2024/25, Sekta ya Uvuvi iliidhinishiwa shilingi bilioni 110.30 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo shilingi bilioni 67.55, sawa na asilimia 61.24 zilitolewa. Shughuli na miradi ya kipaumbele iliyotekelezwa ni pamoja na:

(i) **Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko:** Serikali inatekeleza mradi wa ujenzi wa bandari ya uvuvi - Kilwa Masoko kwa lengo la kukuza uchumi wa buluu na kuongeza pato la Taifa. Utekelezaji wa mradi huu kwa ujumla umefikia asilimia 83 ya lengo na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2025. Aidha, ujenzi wa miundombinu ya msingi ya bandari ya uvuvi upo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji ikiwemo ujenzi wa jengo la utawala (asilimia 90), jengo la kupoza na kusambaza umeme (asilimia 90), jengo la soko (asilimia 85), ghala la kuhifadhia zana za uvuvi (asilimia 80) na jengo la karakana ya meli (asilimia 85).

Bandari hiyo itawezesha meli 10 zenye urefu wa mita 30 kutia nanga kwa wakati mmoja na itaongeza fursa za ajira za moja kwa moja takribani 30,000; kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja na Taifa kwa kuwa na uhakika wa usalama wa chakula na lishe; Kuongeza uzalishaji wa mazao ya uvuvi, hususan katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari; kuwezesha meli za uvuvi kushusha samaki wasiolengwa na kufanyika kwa shughuli ya kuhaulisha (transhipment) mazao ya uvuvi; kukuza soko la ndani na nje ya nchi kwa kuongeza ubora wa bidhaa za uvuvi; Kuongeza uwekezaji katika viwanda vya kuchakata samaki; na kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi baada ya kuvunwa kutoka asilimia 40 hadi 20. Jumla ya shilingi bilioni 64.40 zilitumika.

(ii) **Usimamizi, Uhifadhi na Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi:** Kazi zilizofanyika ni pamoja na: kununua na kusanikisha maboya 32 kwenye maeneo ya mazalia ya samaki katika Halmashauri za Misungwi na Nyamagana kwa lengo la kulinda na kuhifadhi maeneo hayo; kununua ndege nyuki moja (1) kwa ajili ya ulinzi wa rasilimali za uvuvi ikiwemo kudhibiti uvuvi haramu; kutambua na kuanzisha kanzidata ya wavuvi na wachakataji wa mazao ya uvuvi; ujenzi wa chanja 40 za kukaushia dagaa katika eneo la Kilwa Kivinje mkoani Lindi kwa lengo la

kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi baada ya kuvunwa; na kujenga boti 59 na zana za uvuvi kwa ajili ya kuwakopesha wavuvi katika mikoa ya Tanga (33), Mtwara (5), Pwani (8), Lindi (5), Dar es Salaam (5) na Kigoma (3). Manufaa yaliyopatikana ni pamoja na kuimarika kwa uhifadhi wa mazao ya uvuvi na kupungua kwa uvuvi haramu. Jumla ya shilingi bilioni 12.08 zilitumika.

(iii) **Ukuzaji Viumbe Maji:** Kazi zilizofanyika ni: ujenzi na ukarabati wa vituo viwili (2) vya ukuzaji viumbe maji vya Kingolwira (asilimia 90) na Rubambagwe (asilimia 83) ili viweze kutoa huduma bora za ugani na kuzalisha vifaranga; ujenzi wa vizimba 480 na kuvikopesha kwa wanufaika 1,909 ambapo tani 216.68 za samaki zenye thamani ya shilingi bilioni 1.57 zilivunwa kutoka katika vizimba 157 na kufanya marejesho ya shilingi bilioni 1,528.73. Jumla ya shilingi bilioni 8.08 zilitumika.

h) **Sekta ya Madini**

56. Katika mwaka 2024/25, Sekta ya Madini iliidhinishiwa shilingi bilioni 468.92 ambapo shilingi bilioni 418.57 zilitolewa, sawa na asilimia 89.27. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na:

(i) **Uwezeshaji wa Wachimbaji Wadogo**: Shughuli zilizofanyika ni pamoja na utoaji mafunzo kwa vitendo na nadharia kwa wachimbaji wadogo 3,763 kuhusu uchenjuaji dhahabu fanisi na rafiki kwa mazingira, masuala ya afya na usalama migodini, masuala ya fedha, matumizi ya taarifa za utafiti kwenye shuguli za madini na mafunzo kwa wachimbaji chumvi.

(ii) **Utafiti wa Madini**: Tafiti za kijiolojia na jiokemia kwa ajili ya kutambua maeneo yenye madini ya viwandani zilifanyika katika Mkoa wa Pwani ambapo kulibainika uwepo wa madini ya chokaa, kaolini, *sulfur* na madini tembo kwenye maeneo ya Kibiti na Rufiji. Aidha, Serikali imefanya ununuzi wa mitambo ya uchorongaji ukiwemo mtambo mkubwa mmoja (1) wenye uwezo wa kuchoronga miamba hadi kina cha mita 3000 chini ya ardhi na mitambo 10 midogo kwa ajili ya kufanya uchorongaji kwenye maeneo ya wachimbaji wadogo ili kubaini uwepo wa madini chini ya ardhi.

(iii) **Utoaji wa Leseni**: Serikali imefanikiwa kutoa leseni 12,129 zikiwemo leseni za: utafutaji madini (497), uchimbaji wa kati wa madini (37), uchimbaji mdogo wa madini (8,974)), uchenjuaji madini (21), uyeyushaji madini (2), biashara ya madini (2,597) na usafishaji madini (1) ikilinganishwa na jumla ya 11,510 zilizotolewa mwaka 2023/24. Aidha, ilitolewa leseni moja (1) ya uchimbaji mkubwa wa madini ya kinywe katika eneo la Mahenge Morogoro

(iv) Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: kuwezesha kuanza kwa mradi wa uchimbaji mkubwa wa madini ya urani kwenye eneo la Mto Mkuju (Namtumbo); kuanza ujenzi wa jengo la kituo cha utoaji mafunzo ya uongezaji thamani madini cha TGC jijini Arusha; na ununuzi wa magari (32), pikipiki (40), vifaa vya masoko ya madini (mizani 18 na kangavuke 1) na vya maabara kwa ajili ya kuimarisha utendaji kazi na ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na rasilimali madini. Aidha, Serikali imeandaa mkakati wa madini muhimu, mkakati wa madini ya kimkakati na mkakati wa uongezaji thamani madini ndani ya nchi kabla ya madini kusafirishwa nje ya nchi. Katika kusimamia ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na rasilimali madini, kwa mwaka 2024/25, sekta imekusanya shilingi bilioni 1,071.27, sawa na ongezeko la asilimia 41.95 ikilinganishwa na shilingi bilioni 754.69 kwa mwaka 2023/24. Makusanyo hayo ni sawa na asilimia 107.13 ya lengo la shilingi bilioni 1,000. Katika makusanyo ya mwaka 2024/25, wachimbaji wadogo walichangia kwa wastani wa asilimia 40 na wachimbaji wakubwa asilimia 60.

i) Sekta ya Maji

57. Katika mwaka 2024/25, Sekta ya Maji iliidhinishiwa bajeti ya shilingi bilioni 558.1 ambapo shilingi bilioni 496.6, sawa na asilimia 88.98 zilitolewa. Baadhi ya miradi iliyotekelezwa ni kama ifuatavyo:

(i) **Miradi ya Maji Vijijini**: Miradi 775 ya maji vijijini ilikamilika ambapo wananchi wapatao 5,361,460 wamenufaika na huduma ya maji safi na salama. Baadhi ya miradi ya maji iliyokamilishwa ni: Kemondo - Maruku (Bukoba); Luduga - Mawindi awamu ya nne (Mbalali); Bupandwa (Sengerema); Malangali - Hanjawanu - Igando – Kijombe (Wanging'ombe); Liuli (Nyasa); Igaga - Lagana (Kishapu); Igumila (Sikonge); Ukarabati Gombero (Mkinga); Ruaha (Kilosa); Mnima - Vijiji vya Miyuyu (Lot I - VI) (Newala); Kazunzu (Sengerema); Karumo (Sengerema); Hungumalwa (Kwimba); Mkunda (Sumbawanga) pamoja na Lipaya, Lipokela na Kizuka (Songea). Aidha, ukamilishaji wa miradi hiyo umewezesha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama vijijini kufikia asilimia 83. Jumla ya shilingi bilioni 152.6 zilitumika.

(ii) **Miradi ya Maji Mijini**: Miradi 73 ya maji mijini ilikamilika ambapo wananchi wapatao 3,622,710 wamenufaika. Baadhi ya miradi iliyokamilika ni: Mradi wa maji Mugango, Kiabakari - Butiama; Same -Mwanga - Korogwe; Dareda, Singu, Sigino na Bagara (Manyara); mabwawa matatu (3) ya ukubwa wa kati ya Ipililo, Lulago (Simiyu) na Misigiri (Singida); na ujenzi wa chanzo cha maji Butimba katika Jiji la Mwanza. Ukamilishaji wa miradi hiyo umewezesha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama mijini kufikia asilimia 91.6. Jumla ya shilingi bilioni 161.4 zilitumika.

(iii) **Miradi ya Maji ya Kimkakati**: Serikali imeendelea na utekelezaji wa miradi ya kimkakati inayohusisha ujenzi wa miradi na mabwawa makubwa ikiwemo: Bwawa la Kidunda ambao utekelezaji umefikia asilimia 32.36; Mradi wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi Simiyu utakaotoa maji Ziwa Victoria ambao umefikia asilimia 23. Aidha, utekelezaji wa mradi wa maji wa miji 28 unaendelea ambapo umefikia hatua mbalimbali katika vipande vifuatavyo: Kilwa Masoko na Nanyumbu (asilimia 82.93); Handeni, Korogwe, Muheza na Pangani (asilimia 69.8); Kasulu, Mpanda, Sikonge, Urambo na Kaliua (asilimia 57.40); Kayanga, Chato na Geita (asilimia 64.30); Ifakara, Rujewa, Chunya, Njombe, Makambako na Wanging'ombe (asilimia 42.80); Mafinga (asilimia 16.85); Rorya na Tarime (asilimia 14.50); Kiomboi, Singida, Manyoni, Mugumu, Chemba na Chamwino (asilimia 30.65); Songea (asilimia 5.8); na kipande cha Makonde Plateau kwenye miji ya Newala, Nanyamba, Tandahimba na Wilaya ya Mtwara (asilimia 24). Jumla ya shilingi bilioni 98.7 zilitumika.

j) Sekta ya Elimu

58. Kwa mwaka 2024/25, Sekta ya Elimu iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 2,858.68 kwa ajili ya utekelezaji wa programu na miradi mbalimbali ambapo shilingi bilioni 2,442.29 zilitolewa, sawa na asilimia 85 ya bajeti iliyoidhinishwa. Baadhi ya programu na miradi iliyotekelezwa ni pamoja na:

(i) **Elimu bila Ada**: Serikali iliendelea na utekelezaji wa mpango wa utoaji wa elimu bila malipo kuanzia shule ya msingi hadi sekondari kwa kutoa jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 484.27, ambapo wanafunzi 12,208,153 wa shule za msingi na wanafunzi 3,126,937 wa shule za sekondari walinufaika.

(ii) **Mikopo na ufadhili wa Elimu:** Serikali ilitoa mikopo kwa wanafunzi 248,331 wa elimu ya juu yenye thamani ya shilingi bilioni 787.4. Kati ya fedha zilizotolewa, shilingi bilioni 19.95 zilitolewa kwa wanafunzi 7,534 wa ngazi ya stashahada katika fani ya sayansi na ufundi na shilingi bilioni 7.29 zilitolewa kuwezesha ufadhili kwa wanafunzi 1,400 wenye ufaulu wa juu katika fani za sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati kupitia *SAMIA scholarship*. Vilevile, Serikali kupitia vyanzo vya mapato ya ndani kwa mara ya kwanza ilitoa ufadhili kwa wanafunzi wa Kitanzania wanaosoma shahada ya uzamili katika sayansi na teknolojia ya nyuklia nje ya nchi kupitia *SAMIA Extended scholarship* ambapo wanafunzi watano (5) walinufaika.

(iii) **Miradi ya ujenzi na ukarabati**: Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya elimu kupitia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya ujenzi na ukarabati katika ngazi za elimu msingi na sekondari. Katika elimu ya msingi, Serikali imekamilisha ujenzi wa shule mpya za awali na msingi 277, vyumba vya madarasa ya awali 930, vyumba vya madarasa ya Elimu maalum 71, vyumba vya madarasa ya

shule za msingi 2,706, mabweni tisa (9) ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu, matundu ya vyoo 5,016 na ukarabati wa shule 227. Aidha, kwa upande wa elimu sekondari, Serikali imekamilisha ujenzi wa shule 241 ambapo shule saba (7) ni za bweni kwa ajili ya wavulana na shule za kutwa 234. Vilevile, Serikali ipo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji wa ujenzi wa shule mpya 103 za sekondari za amali (shule 29 ni za amali za kihandisi na shule 74 ni za amali zisizo za kihandisi), madarasa 679, mabweni 717, mabwalo saba (7), nyumba za walimu 229 na matundu ya vyoo 152. Shughuli nyingine ni umaliziaji shule za mikoa 16, ukamilishaji wa maboma ya madarasa 50, maabara 43 na mabweni 15. Jumla ya shilingi bilioni 1,023 zilitumika.

(iv) **Vyuo vya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi**: Serikali imeendelea na ujenzi wa vyuo 65 vya elimu ya ufundi na ufundi stadi ambapo 64 ni vya wilaya na kimoja (1) ni cha mkoa (Songwe). Ujenzi wa vyuo hivyo umefikia wastani wa asilimia 65. Jumla ya shilingi bilioni 30 zilitumika. Aidha vyuo hivi vikikamilika, jumla ya wanafunzi 23,840 watadahiliwa kwa awamu ya kwanza.

(v) **Ujenzi wa Vituo vya Umahiri (Centers of Excellence)**: Ujenzi unaendelea kufanyika ili kuimarisha utoaji wa mafunzo kwa vitendo kwa fani za kipaumbele kupitia: Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam - Kampasi ya Mwanza - umahiri katika uchakataji na utengenezaji wa bidhaa za ngozi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 86; DIT - Kampasi ya Dar es Salaam - umahiri katika masuala ya TEHAMA umefikia asilimia 94; Chuo cha Ufundi Arusha - umahiri katika utafiti na mafunzo ya nishati jadidifu; na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji - umahiri katika usafiri wa anga umefikia asilimia 93. Vilevile, Serikali iliendelea kuboresha Kituo cha umahiri wa magonjwa ya Moyo – Mloganzila. Jumla ya shilingi bilioni 36.9 zilitumika.

(vi) **Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET):** Ujenzi na ukarabati wa kampasi 16 za taasisi za elimu ya juu katika mikoa mbalimbali ulifikia hatua zifuatazo: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kampasi ya Zanzibar - Buyu (asilimia 50), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kampasi ya Kagera (asilimia 50), Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kampasi ya Katavi (asilimia 15); Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili kampasi ya Kigoma (asilimia 10); Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kampasi ya Lindi (asilimia 50); Chuo Kikuu Ardhi kampasi ya Mwanza (asilimia 10); Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kampasi ya Rukwa (asilimia 87); Chuo cha Ushirika Moshi kampasi ya Shinyanga (asilimia 46), Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere cha Kilimo na Teknolojia kampasi ya Tabora (asilimia 10); na Chuo Kikuu cha Mzumbe kampasi ya Mkinga (asilimia 45). Aidha, utekelezaji wa mradi wa HEET kwa ujumla umefikia wastani wa asilimia 43. Jumla ya shilingi bilioni 251.7 zilitumika.

k) Sekta ya Afya

59. Katika mwaka 2024/25, Sekta ya Afya iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 1,317.62 ambapo Shilingi bilioni 929.36 zilitolewa, sawa na asilimia 70.5. Serikali ilitekeleza programu na miradi mbalimbali iliyolenga kuboresha huduma za afya nchini ikiwa ni pamoja na:

(i) **Afya ya Msingi**: Serikali imeendelea kuboresha huduma za afya ya msingi kwa kukamilisha ujenzi wa hospitali 25, vituo vya afya 90 na zahanati 143. Vilevile, ujenzi wa zahanati 349, vituo vya afya 130 na hospitali 104 upo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji. Jumla ya shilingi bilioni 119.3 zilitumika.

(ii) **Ngazi ya Rufaa:** Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na: ujenzi na upanuzi wa miundombinu ya kutolea huduma za afya katika Hospitali ya Taifa - Muhimbili umefikia asilimia 95 kwa awamu ya pili, hospitali za Rufaa za Kanda ya Burigi - Chato awamu ya tatu (asilimia 88), Kanda ya Kusini - Mtwara awamu ya pili (asilimia 30), Kanda ya Kati - Benjamin Mkapa (asilimia 65); Kanda ya Kaskazini - KCMC ilikamilika pamoja na Hospitali Maalum ya Magonjwa Ambukizi - Kibong'oto awamu ya pili (asilimia 51). Vilevile, ujenzi wa miundombinu katika hospitali saba (7) za Rufaa za Mikoa umekamilika na kuanza kutoa huduma katika hospitali za (Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere) Mara, Katavi, (Ligula) Mtwara, (Maweni) Kigoma, (Mawenzi) Kilimanjaro, Simiyu na (Songea) Ruvuma. Aidha, ujenzi wa miundombinu ya hospitali sita (6) za Rufaa za Mikoa upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama ifuatavyo; Manyara (asilimia 88), Singida (asilimia 75), Songwe (asilimia 65), Kitete - Tabora (asilimia 70), Geita (asilimia 50) na Sokoine - Lindi (asilimia 82). Jumla ya shilingi bilioni 27.26 zilitumika.

(iii) **Dawa, Vifaa, Vifaa Tiba, Vitendanishi na Chanjo:** Serikali imeendelea kuboresha huduma za afya kwa kuhakikisha kuwa bidhaa za afya na chanjo muhimu zinapatikana na kuwafikia wananchi kwa wakati. Upatikanaji wa bidhaa 290 muhimu za afya ulifikia wastani wa asilimia 86 na chanjo muhimu ulifikia wastani wa asilimia 94. Jumla ya shilingi bilioni 404.43 zilitumika.

l) Sekta ya Viwanda na Biashara

60. Katika mwaka 2024/25, Sekta ya Viwanda na Biashara iliidhinishiwa shilingi bilioni 29.78 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo ambapo shilingi bilioni 19.78 zilitolewa, sawa na asilimia 66.4. Utekelezaji katika sekta ni kama ifuatavyo:

Viwanda

(i) **Miradi ya Kielelezo na Kimkakati:** Mradi unganishi wa Mchuchuma na Liganga umefanikiwa kupata mwekezaji mpya ambapo majadiliano ya mkataba na mwekezaji yanaendelea. Mafanikio yanayotarajiwa ni pamoja na: Makubaliano

katika vipengele muhimu vya mikataba ikiwemo misingi sahihi ya mgawanyo wa hisa na muundo wa uwekezaji (Financing structure); kiwango cha mtaji wa uwekezaji unaohitajika; muundo wa usimamizi na uendeshaji wa mradi; na muda wa mkataba wa uwekezaji. Aidha, kwa upande wa mradi wa Magadi Soda Engaruka, Serikali imelipa fidia na ada ya leseni ya uchimbaji madini ili kuruhusu mradi kuendelea. Jumla ya shilingi bilioni 7.33 zilitumika.

(ii) **Mradi wa Kiwanda cha *Kilimanjaro Machine Tools Company Limited* (KMTC):** Serikali iliendelea na jitihada za kuimarisha kiwanda cha KMTC ili kiweze kujiendesha kibiashara ambapo mashine mpya za kisasa za kukunja chuma, kusokota chuma (sheet roller machine) na kukata chuma (gantry plasma cutting machine) zilinunuliwa na kuanza kutumika na mashine 12 pamoja na vipuri 123 vilizalishwa. Aidha, kiwanda hicho kimekuwa tegemeo la vipuri kwa viwanda vya ndani vikiwemo kiwanda cha sukari (TPC), *Tanzania Breweries Limited* (TBL), *Kili Leather* na viwanda vya mkonge, ambavyo awali vilikuwa vinaagiza baadhi ya mashine na vipuri kutoka nje ya nchi. Jumla ya shilingi bilioni 1.0 zilitumika.

(iii) **Mradi wa Kiwanda cha Viuadudu (TBPL) Kibaha**: Serikali iliendelea na jitihada za kukiendeleza kiwanda cha *Tanzania Biotech Company Limited* (TBPL) kilichopo Mkoa wa Pwani ambacho kinazalisha dawa za kibaiolojia (Bio-Products) za viuadudu vya kuua mazalia ya mbu na viuatilifu hai kwa ajili ya kuua wadudu waharibifu wa mazao. Jumla ya lita 335,416 za viuadudu zilizalishwa na lita 208,333 ziliuzwa na kusambazwa katika halmashauri 57 zenye maambukizi makubwa ya malaria ambapo dawa hii imeonesha mafanikio katika kuangamiza mbu. Pia kiwanda kilikamilisha majaribio ya dawa mpya ya kibaiolojia (Thurisave - 24) kwa ajili ya kuua wadudu dhurifu kwenye mazao na kitaanza kuzalisha kibiashara baada ya kupata ithibati za mamlaka za udhibiti na kupata usajili. Bidhaa hii imeonesha mafanikio makubwa kwenye kuangamiza wadudu kwenye mazao ya mahindi, matunda na mbogamboga.

(iv) **Kuweka mazingira wezeshi ya ujenzi wa viwanda nchini:** Serikali imefanikiwa kuvutia uwekezaji katika viwanda ambapo kwa mwaka 2024/25 viwanda vikubwa mbalimbali vimejengwa nchini ikiwemo: kiwanda cha magari cha *Saturn Corporation Limited* (Kigamboni - Dar es salaam); kiwanda cha vioo cha *Sapphire Float Glass (Tanzania) Company Limited* (Mkuranga – Pwani) chenye uwezo wa kuzalisha tani 700 za vioo kwa siku; Keda *Float Glass T. Ltd* (Mkuranga – Pwani); Kiwanda cha Mafuta ya alizeti cha *Wild Flower and Grains Ltd* (Singida); kiwanda cha *Moli Investment Co.Ltd* cha kutengeneza mabomba ya plastiki na marobota ya pamba (Bariadi - Simiyu); kiwanda cha *Triwin Agricultural Resources T. Ltd* cha kuchakata mafuta ya pamba na alizeti (Bariadi – Simiyu); kiwanda cha *Sunshine Industrial Co. Ltd cha mafuta ya alizeti*

(Dodoma); kiwanda cha chaki - *Ng'hami Chalk Industry* (Maswa - Simiyu); *na kiwanda Mainland Agro Processing Co. Ltd* cha mafuta ya alizeti (Dodoma). Viwanda hivyo vimetoa ajira za moja kwa moja 4,625 na zisizo za moja kwa moja 19,777.

Aidha, viwanda vikubwa vilivyofanyiwa upanuzi katika mwaka 2024/25 ni pamoja na: kiwanda cha kuunganisha magari cha GF Trucks and Equipment Ltd (TAMCO Kibaha – Pwani); Kiwanda cha saruji cha Maweni Limestone Limited (Tanga); kiwanda cha Sukari cha Kilombero – K4 (Morogoro); kiwanda cha Sukari cha Mkulazi (Morogoro); na Kiwanda cha Sukari Kagera (Kagera). Viwanda hivyo vimezalisha ajira za moja kwa moja 97,450 na zisizo za moja kwa moja 40,901.

(v) **Kuwezesha Uanzishwaji wa Kongani za Viwanda:** Ujenzi wa miundombinu ya Kongani ya Viwanda *Sino Tan Industrial Park* (Kwala – Pwani) kwa hatua ya awali ya ujenzi wa ekari 500 kati ya ekari 2,500 imefikia asilimia 80. Shughuli zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa barabara kuu ya ndani, miundombinu ya maji, jengo la utawala, jengo la zimamoto, jengo la hosteli, majengo sita (6) ya viwanda na jengo la kufundishia mafundi. Aidha, katika kongani hiyo, viwanda vitatu (3) vimeanza uzalishaji ikiwemo kiwanda cha nguo cha *House of Garments*, kiwanda cha vipodozi cha *KVS Chemicals* na kiwanda cha *Snowsea* kinachozalisha vifaa vya umeme vya majokofu, viwanda hivyo vimezalisha ajira za moja kwa moja 140 na sisizo za moja kwa moja 200.

Katika Kongani ya Kisasa ya Viwanda *Modern Industrial Park* (Mlandizi - Pwani), shughuli zilizokamilika ni: ujenzi wa miundombinu ya jengo la utawala; kituo cha huduma za pamoja kwa ajili ya Taasisi za Serikali (one stop centre); ujenzi wa kituo cha zimamoto; na ujenzi wa kituo cha Afya na uzio wa kilomita 9. Ujenzi wa viwanda vitano (5) unaendelea ikiwemo: kiwanda cha *Sulphur and minerals sulphur pesticides* cha pembejeo; kiwanda cha *Tan Smart lyf - lubricants* cha vilainishi vya magari na mashine mbalimbali; kiwanda cha *Nadeem- food processing*; *Mohamed Maaz Abdul – General industry;* na kiwanda cha *TanTurk-generator assembly* cha kutengeneza majenerata. Jumla ya ajira 500 za muda mfupi zilitolewa ili kuwezesha shughuli za ujenzi.

Aidha, Katika kongani ya TAMCO Kibaha, Pwani, uboreshaji wa miundombinu unaendelea ikiwemo kukamilisha usanifu wa barabara za eneo lote. Katika kipindi tajwa, ujenzi wa mita 230 za barabara kwa kiwango cha lami umekamilika kwa asilimia 100. Vilevile, ujenzi wa kiwanda kikubwa cha kuunganisha vichwa vya magari, tipa pamoja na pikipiki (TATA) unaofanywa na mwekezaji unaendelea ambapo umefikia asilimia 70. Kupitia wawekezaji waliopo katika kongani ya TAMCO, jumla ya ajira 282 kwa watanzania zimezalishwa na

kuchangia upatikanaji wa bidhaa zinazozalishwa ndani ya nchi na hivyo kupunguza matumizi ya fedha za kigeni kuagiza bidhaa nje ya nchi.

(vi) **Urasimishaji wa Shughuli za Wajasiriamali Wadogo na wa Kati:** Serikali iliendelea kutoa huduma kwa wajasiriamali wadogo na wa kati kwa kuwapatia msaada wa teknolojia, mafunzo, masoko na mikopo kupitia SIDO. Huduma hizo zimechangia uanzishwaji wa viwanda vidogo vipya 604 na kutengeneza ajira 2,818. Aidha, ukarabati wa miundombinu ya majengo ya viwanda ya vituo viwili (2) vya uendelezaji teknolojia (TDCs) cha Arusha na Chato – Geita ulikamilika na kuwezesha utengenezaji na uuzaji wa mashine 545 na vipuri 3,728. Ujenzi wa majengo na miundombinu katika mitaa ya viwanda (Industrial Clusters) ambapo majengo mawili (2) ya viwanda yamejengwa Kahama – Shinyanga na ujenzi wa jengo moja (1) la mtaa wa viwanda Zuzu – Dodoma umefikia asilimia 65. Jumla ya shilingi bilioni 1.68 zilitumika.

(vii) **Mikopo kwa Wajasiriamali kupitia SIDO:** Serikali ilitoa mikopo 1,498 yenye thamani ya shilingi bilioni 8.525 kwa wajasiriamali wadogo na wa kati. Kati ya mikopo hiyo, mikopo 1,470 yenye thamani ya Shilingi bilioni 4.47 ilitolewa kupitia Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wajasiriamali (NEDF); mikopo 13 yenye thamani ya shilingi milioni 395 ilitolewa kupitia Mfuko wa Dhamana wa Serikali (CGS); na mikopo 15 yenye thamani ya shilingi bilioni 3.66 kupitia programu ya *SANVN Viwanda Scheme.* Mikopo hiyo iliwezesha kupatikana kwa ajira 1,395 ambapo wanawake ni asilimia 42.5 na wanaume asilimia 57.5. Vilevile, wastani wa kiwango cha urejeshaji mikopo kiliimarika na kufikia asilimia 92 Desemba 2024 kutoka asilimia 90.1 Desemba 2023.

Biashara

(i) **Kuweka Mazingira Wezeshi ya Kuchochea Maendeleo ya Biashara Nchini:** Baadhi ya shughuli zilizotekelezwa ni: kuzinduliwa kwa Sera ya Taifa ya Biashara 2003 Toleo la 2023; kuongeza bidhaa 29 mpya katika mfumo rahisi wa ufanyaji biashara (STR) kwa wafanyabiashara wadogo wanaovuka mpaka wa Tanzania na Zambia; na kuhamasisha wafanyabiashara kusafirisha shehena ya bidhaa 21 tofauti (tani 1,000) zenye thamani zaidi ya dola za Marekani milioni 9.36 katika nchi 18 za Afrika kupitia soko la AfCFTA kwa nchi ambazo tulikuwa hatutangamani nazo. Aidha, bidhaa zilizosafirishwa ni pamoja na; mkonge, kahawa, viungo, parachichi, ngozi, tumbaku, mchele na vioo. Vilevile, Serikali imetoa jumla ya vyeti 131 vya uasili wa bidhaa kwa kampuni kuuza kupitia soko la AfCFTA. Kwa ujumla, sekta ya biashara nchini imefanikiwa kuongeza mauzo ya bidhaa katika masoko ya kikanda na kimataifa, hususan EAC, SADC, AGOA na Umoja wa Ulaya.

(ii) **Kusajili Kampuni, Majina ya Biashara, Alama za Biashara na Huduma na Leseni za Viwanda:** Serikali kupitia BRELA iliendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu kurasimisha biashara ambapo jumla ya kampuni 18,541 zilisajiliwa kati ya 16,200 zilizokusudiwa, sawa na asilimia 114; kusajili majina ya biashara 31,123 kati ya 29,912 yaliyopangwa, sawa na asilimia 104; kusajili alama za biashara na huduma 2,615 kati ya 4,300 zilizokuwa zimepangwa, sawa na asilimia 61; Leseni za Viwanda 435 kati ya 235 zilizokuwa zimepangwa sawa na asilimia 185 na kutoa Leseni za Biashara kundi "A" 22,718 kati ya 15,120 zilizopangwa sawa na asilimia 150.

(iii) **Kuhamasisha Matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala:** Serikali iliendelea kuhamasisha wakulima kutumia mfumo wa stakabadhi za ghala ambapo katika kipindi cha mwaka 2024/25 umewezesha ukusanyaji wa mazao tani 978,912.95 kwa mazao ya kahawa, korosho, kakao, maharage, mihogo, mpunga, mbaazi, choroko, mchele, ufuta, chai, soya na dengu yenye thamani ya shilingi bilioni 3,440 ikilinganishwa na tani 485,925 zenye thamani ya shilingi bilioni 1,303 mwaka 2023/24. Aidha, mapato ya Serikali kupitia ushuru wa mazao hayo yameongezeka kufikia shilingi bilioni 88.3 kutoka shilingi bilioni 35 mwaka 2023/24. Vilevile, uwazi katika mnada, ubora wa mazao na usalama wa stakabadhi za kidigitali umeongeza imani ya wanunuzi wa ndani na wa kimataifa. Nchi kama Japani, India, Saudi Arabia na Uturuki zinatumia mfumo huu kama kigezo cha ubora na uaminifu katika biashara ya mazao ya Tanzania.

Bei za mazao zimeongezeka kwa wastani wa asilimia 15 - 25, zikionyesha ushindani mzuri na imani ya soko, mapato ya Serikali kupitia Cess yameongezeka kwa wastani wa asilimia 40 - 60. Aidha, mfumo umewezesha zaidi ya asilimia 70 ya mazao ya kimkakati kama korosho, ufuta, kakao na dengu kuuzwa, ikilinganishwa na mauzo ya chini ya asilimia 30 kabla ya mfumo kuwepo.

(iv) **Utafutaji wa masoko ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi:** Serikali ilifanikisha kuratibu ushiriki wa nchi katika Maonesho ya EXPO 2025 Osaka ambapo wafanyabiashara 175 walishiriki na mikataba (MoU) nane (8) yenye thamani ya shilingi bilioni 38 ilisainiwa wakati wa maonesho hayo. Serikali pia, iliratibu warsha na ziara za kibiashara katika mikoa sita (6) na kampuni 120 ziliwezeshwa kupata uelewa wa masoko ya kikanda na kimataifa (EAC, SADC, AfCFTA, AGOA, na soko la China). Jumla ya shilingi milioni 400 zilitumika.

(v) **Utayarishaji wa Viwango pamoja na Utoaji wa Leseni za Ubora:** Serikali kupitia Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ilifanikiwa kuandaa jumla ya viwango 604 vya ubora kati ya 690 vilivyopangwa sawa na asilimia 87.5. Viwango hivyo ni pamoja na viwango vya kilimo na chakula, kemikali, nguo, madini, na uhandisi. Leseni 751 za nembo ya ubora zilitolewa sawa na asilimia 83.4 ya lengo la kutoa

leseni 900 kwa mwaka. Aidha,TBS ilisajili majengo, maeneo ya uzalishaji, uuzaji na usambazaji wa bidhaa za chakula na vipodozi 15,156 ambavyo ni sawa na asilimia 116.6 ya lengo la kusajili na kutoa vibali 13,000 kwa mwaka. Pia ilisajili bidhaa za chakula na vipodozi vipatavyo 2,345 sawa na asilimia 111.7 ya lengo la kusajili bidhaa 2,100. Hatua hizi zimewezesha wazalishaji kuzalisha bidhaa zenye ubora wa kimataifa, kupanua fursa za masoko na kulinda walaji. Vilevile, TBS iliandaa na kuendesha jumla ya program maalum 20 za kaguzi katika masoko ya maeneo yote nchini na kuwezesha kuondoa katika soko na kuteketeza jumla ya tani 29,711 za bidhaa hafifu zenye thamani ya shilingi bilioni 5.6. Kaguzi hizo maalum hutumika kama nyenzo muhimu ya kuhakikisha bidhaa zinazotumiwa na wananchi ni zile zinazokidhi vigezo vya ubora na usalama.

m) Sekta ya Uwekezaji

61. Katika mwaka 2024/25, Sekta ya Uwekezaji iliidhinishiwa shilingi bilioni 276.59 ambapo shilingi bilioni 251.21 zilitolewa sawa na asilimia 90.83. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na:

(i) **Maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050:** Serikali ilifanikiwa kuratibu uandaaji wa DIRA 2050 iliyozinduliwa rasmi tarehe 17 Julai, 2025 na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ambayo inabainisha mwelekeo wa Taifa kwa kipindi cha miaka 25. Dira hiyo imeandaliwa na watanzania kwa kutumia fedha za mapato ya ndani.

(ii) **Usajili wa Miradi ya Uwekezaji Nchini:** Serikali kupitia kilichokuwa Kituo Cha Uwekezaji Tanzania (TIC) ilisajili miradi mipya 940 yenye thamani ya dola za Marekani milioni 11,267.29 ambapo inatarajiwa kuzalisha ajira mpya 298,257. Usajili wa miradi hiyo ni sawa na ongezeko la asilimia 32.96 ya miradi iliyosajiliwa mwaka 2023/24. Aidha, Serikali kupitia iliyokuwa Mamlaka ya Maeneo ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA) ilisajili na kutoa leseni mpya 29 za uwekezaji katika maeneo ya uzalishaji kwa mauzo ya nje zikiwemo leseni nane (8) za uendeshaji na leseni 21 za uendelezaji. Miradi hiyo 29 inatarajiwa kuwekeza dola za Marekani milioni 430.62, kuchangia mauzo ya nje kwa dola za Marekani milioni 259.28 na kutoa ajira 27,085. Usajili wa miradi hiyo ni sawa na ongezeko la asilimia 21 ya miradi iliyosajiliwa kwa mwaka 2023/24.

(iii) **Marekebisho ya Sheria na Kanuni:** Jumla ya sheria na kanuni 94 zilifanyiwa marekebisho ili kuweka mazingira wezeshi ya ufanyaji biashara na uwekezaji. Aidha, jumla ya tozo, ada na faini 628 zilizokuwa kikwazo katika ufanyaji biashara na uwekezaji ziliweza kupunguzwa/kufutwa. Marekebisho hayo yameendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji hapa nchini na hivyo kuvutia wawekezaji wa nje na ndani ya nchi.

(iv) **Kujenga na Kuimarisha Mifumo ya Elektroniki kwa ajili ya Utoaji Huduma:** Serikali ilijenga na kuimarisha mifumo mbalimbali ya kielektroniki kwa ajili ya utoaji huduma na hivyo kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji. Baadhi ya mifumo hiyo ni pamoja na mfumo wa kanzidata za uwekezaji (National Investment Database System -NIDS), Mfumo wa Dirisha moja la kuhudumia wawekezaji lililopo TISEZA (Tanzania electronic investment Window- TeIW); Moduli ya utoaji wa leseni za biashara kwenye halmashauri kupitia mfumo wa TAUSI; kuunganisha mfumo wa BRELA na mifumo ya Bodi ya Utalii na kuunganisha mfumo wa uombaji wa vibali vya ujenzi kwa taasisi za usajili wa wahandisi (ERB), wakandarasi (CRB), wasanifu majengo na wakadiriaji majenzi (AQRB).

(v) **Uwekezaji wa Umma:** Serikali iliendelea na maboresho ya kimuundo na kiutawala ambayo yalichangia ufanisi wa kiutendaji na kuimarika kwa ukusanyaji maduhuli ambapo katika mwaka 2024/25 Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina iliidhinishiwa kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi trilioni 1.113 ambapo ilifanikiwa kukusanya shilingi trilioni 1.028 sawa na asilimia 92 ya lengo hilo la mwaka. Kiasi hiki ni sawa na ongezeko la asilimia 34 ikilinganishwa na shilingi bilioni 767.08 zilizokusanywa mwaka 2023/24.

(vi) **Tathmini ya Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (MKUMBI):** Serikali ilifanya tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (MKUMBI) kwa lengo la kupata halihalisi ya utekelezaji wa MKUMBI. Pamoja na kuwepo kwa mafanikio mbalimbali kama vile kupungua kwa muda wa kushughulikia maombi ya vibali kutoka wastani wa siku 14 hadi siku tatu (3) kwa vibali vingi; na muda wa kushughulikia maombi ya vibali vya kazi kutoka zaidi ya siku 14 hadi kati ya siku tatu (3) hadi saba (7), tathmini hiyo ilionesha umuhimu wa kuandaa Mpango wa Pili wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji nchini (MKUMBI II) kwa kuzingatia: maono ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050; mahitaji ya sasa ya uwekezaji na ufanyaji biashara; mabadiliko ya teknolojia na kiuchumi; kuendeleza sekta binafsi ambayo ni msingi wa mageuzi ya kiuchumi; kujumuisha sekta nyingi zaidi zikiwemo elimu, miundombinu, na kampuni changa bunifu (startups); pamoja na kutatua changamoto.

n) Utawala Bora

62. Katika mwaka 2024/25, shughuli na miradi mbalimbali zilitekelezwa ikiwa ni pamoja na:

(i) **Masuala ya Rushwa na Haki Jinai**: Serikali iliendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa utekelezaji Awamu ya Nne 2023-2030. Aidha, kupitia Mkakati huu, Serikali iliendelea kuwezesha jamii kushiriki kikamilifu

katika kuimarisha uadilifu na kuchukia rushwa; kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma; kuimarisha uwazi na uwajibikaji wa watumishi wa umma; kushirikiana na sekta binafsi na asasi za kiraia katika kukabiliana na vitendo vya rushwa; na kuimarisha mfumo wa usimamizi wa uchaguzi nchini ili kuepusha vitendo vya rushwa. Vilevile, Serikali iliendelea kutekeleza mipango na mikakati ya kuimarisha Haki Jinai nchini kwa kuimarisha mifumo ya TEHAMA ili kurahisisha utendaji kazi na kuwezesha kubadilishana taarifa baina ya taasisi za Haki Jinai.

(ii) **Mahakama**: Katika kipindi cha mwaka 2024/25, Mahakama ilifanikiwa kumaliza mashauri 245,809 sawa na asilimia 85 ya mashauri 303,237 yaliyokuwepo Mahakamani. Mrundikano wa mashauri ulipungua hadi kufikia asilimia 3 Juni 2025. Matumizi ya TEHAMA yameendelea kuimarishwa, ambapo mashauri yote yanasajiliwa na kushughulikiwa kielektroniki kupitia mfumo wa usimamizi na uendeshaji wa mashauri kieletroniki ambao umeanza kutumika kuanzia Mahakama za Wilaya hadi Mahakama ya Rufani mwaka 2024/25. Aidha, mifumo mingine ya kuharakisha usikilizaji wa mashauri imeendelea kuimarishwa na kutumika, ikiwemo mfumo wa kunukuu na kutafsiri mwenendo wa mashauri na mfumo wa kusikiliza mashauri kwa njia ya mtandao (virtual court). Katika kuongeza ufanisi wa utoaji haki, ukaguzi wa mahakama pia ulifanyika kwa asilimia 99.7.

Miradi ya ujenzi wa majengo ya Mahakama 95 imetekelezwa kwa hatua mbalimbali ikiwemo kukamilika kwa ujenzi wa jengo la makao makuu ya Mahakama na nyumba za makazi ya Majaji Dodoma, na hivyo kuiwezesha Mahakama kuhamia Dodoma. Miradi mingine iliyoendelea ni pamoja na miradi tisa (9) ya ujenzi wa vituo jumuishi vya utoaji haki; ujenzi wa majengo ya mahakama za wilaya 12; ujenzi wa majengo ya mahakama za mwanzo 72; na ujenzi wa nyumba ya jaji mkuu, ukarabati wa jengo la zamani la mahakama kuu Dodoma.

(iii) **Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa mwaka 2024:** Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na: uhakiki wa maeneo ya utawala yaliyojumuisha kata 3,956, vijiji 12,333, mitaa 4,269 na vitongoji 64,274; uandaaji wa nyaraka, uhamasishaji na utoaji wa elimu ya mpiga kura; ununuzi na usambazaji wa vifaa; ufuatiliaji na uratibu wa upigaji kura; uandikishaji wa wapiga kura; uteuzi wa wagombea na kampeni. Jumla ya shilingi bilioni 267.07 zilitumika.

(iv) **Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba za Viongozi na Watumishi**: Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI iliendelea na ujenzi na ukarabati wa nyumba 78 za viongozi ngazi ya mikoa na wilaya ambapo nyumba 40 zilikamilika na nyumba 38 zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Aidha, Serikali imeendelea na

ujenzi wa nyumba 231 kwa ajili ya wakurugenzi na wakuu wa idara katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo kati ya hizo nyumba 46 zilikamilika na nyumba 185 zipo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji. Jumla ya shilingi bilioni 25.58 zilitumika.

Serikali pia kupitia Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) iliendelea na utekelezaji wa awamu ya pili ya ujenzi wa nyumba 150 za watumishi eneo la Nzuguni – Dodoma ambao umefikia asilimia 27; ujenzi wa nyumba za watumishi wa umma katika eneo la Magomeni Kota Awamu ya Pili "*Block* B na C umekamilika" na *Block* D umefikia asilimia 15; na ujenzi wa nyumba za watumishi wa umma za Temeke Kota jijini Dar es Salaam umefikia asilimia 33. Kwa upande wa nyumba za viongozi, Serikali imekamilisha ukarabati wa nyumba saba (7) za viongozi jijini Dodoma na nyumba tatu (3) za viongozi katika mkoa wa Dar es Salaam. Jumla ya shilingi bilioni 8.76 zilitumika.

(v) **Ujenzi wa Majengo ya Utawala katika Mamlaka za Serikali za Mitaa:** Serikali imeendelea na ujenzi wa majengo 76 ya utawala ya Halmashauri ambapo majengo ya utawala 14 katika Halmashauri za Moshi Manispaa, Tunduma Mji, Mbinga Mji, Tanganyika, Mbulu, Rorya, Chunya, Mbeya Vijijini, Ulanga, Mtwara Vijijini, Madaba, Singida Vijijini, Uyui na Bumbuli yalikamilika na yanatoa huduma. Majengo 62 yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ikiwemo ukamilishaji, ujenzi wa kuta, kuezeka, nguzo na hatua ya msingi. Jumla ya shilingi bilioni 53.29 zilitumika.

(vi) **Ujenzi wa Ofisi za Watendaji Kata na Vijiji:** Serikali imeendelea na ujenzi wa: ofisi za kata 146 ambapo ofisi 95 zilikamilika na 51 zinaendelea; ofisi za vijiji 61 ambapo ofisi 27 zilikamilika na ofisi 34 zinaendelea; na ofisi za mitaa 97 ambapo ofisi 33 zilikamilika na ofisi 64 zinaendelea. Jumla ya shilingi bilioni 5.89 zilitumika.

o) **Sekta ya Ardhi**

63. Katika mwaka 2024/25, utekelezaji wa shughuli na miradi uliidhinishiwa shilingi bilioni 186.6 ambapo shilingi bilioni 164.6 zilitolewa, sawa na asilimia 88.2. Shughuli na miradi ya kipaumbele iliyotekelezwa ni pamoja na:

(i) Kuhuishwa kwa Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995 (Toleo la Mwaka 2023).

(ii) **Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha (KKK)**: Viwanja 14,948 vilipimwa katika Jiji la Arusha, Manispaa za Ubungo na Moshi, Halmashauri za Wilaya za Njombe, Ludewa, Makete, Korogwe, Magu, Mbarali, Ruangwa, Misenyi, na Kwimba. Jumla ya shilingi bilioni 4.06 zilitumika.

(iii) **Mradi wa Kuboresha Usalama wa Milki nchini (LTIP):** Hati 421,686 zilisajiliwa ambapo 366,436 zilitolewa vijijini na 55,250 kwa maeneo ya mijini; Alama za Kieletroniki za Upimaji (*Continous Reference Station* – CORS) 22 zilisimikwa katika Mikoa 22 kwa ajili ya kurahisisha kazi za upimaji na kupunguza gharama. Jumla ya shilingi bilioni 32.25 zilitumika.

(iv) **Mradi wa Ujenzi wa Kanzi Data za Ardhi Kitaifa (National Land Data Infrastructure Project):** Mshauri elekezi amepatikana ambaye anashirikiana na wataalam wa ndani kukamilisha usanifu wa mradi, kuandaa viwango vya makadirio ya gharama za mradi pamoja na kuandaa zabuni za ununuzi wa ndege maalum ya kupiga picha za anga na zabuni ya mkandarasi wa kutekeleza mradi. Hatua hii itawezesha kukamilisha kazi ya ununuzi wa vifaa na kumpata Mkandarasi wa uwekaji wa Vituo vya Kielektroniki vya Upimaji na uandaaji wa Ramani za Msingi. Jumla ya shilingi bilioni 5.77 zilitumika.

(v) **Mradi wa Kupima Mipaka ya Kimataifa:** Jumla ya kilometa 268 za mpaka ziliimarishwa na kufanya jumla ya kilomita zilizoimarishwa kufikia 458 kati ya kilomita 758 za nchi kavu katika mpaka kati ya Tanzania na Kenya kwa kuweka alama, vipimo na kuandaa ramani. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa uimarishaji mipaka imefanya ukaguzi wa mpaka wa Tanzania na Kenya, Tanzania na Zambia, Tanzania na Burundi na Tanzania na Msumbiji. Jumla ya shilingi bilioni 1.52 zilitumika.

(vi) **Mradi wa Uendelezaji wa Mji wa Samia Afcon:** Serikali ilisanifu Samia Afcon City uliopo jijini Arusha wenye ukubwa wa ekari 4,555 ambapo jumla ya viwanja 3,300 vimepangwa. Katika Mradi huo jumla ya viwanja 469 vimepimwa kwenye eneo lenye ukubwa wa ekari 209 kwa awamu ya kwanza. Utekelezaji wa mradi huu utawezesha kuwa na mji wa kisasa kwenye eneo linalojengwa uwanja wa mpira wa miguu uliopo Jijini Arusha ambao utatumika katika mashindano ya mpira wa miguu kwa Mataifa ya Afrika (AFCON) mwaka 2027.

(vii) **Uandaaji wa Mipango ya matumizi ya Ardhi Katika Vijiji:** Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi iliandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji 557 sawa na asilimia 198.3 ya lengo la vijiji 280 kwa mwaka. Hivyo, idadi ya vijiji vyenye mipango ya matumizi ya ardhi vimeongezeka kutoka vijiji 4,124 Juni 2024 hadi vijiji 4,681 Juni 2025, sawa na ongezeko la asilimia 13.5. Jumla ya shilingi bilioni 9.68 zilitumika.

Ili kuongeza kasi ya Kupanga Kupima na Kumilikisha ardhi, Serikali imekamilisha na kuanza kutumia mfumo wa Kielektroniki wa E- Ardhi kwa ajili ya utoaji huduma ambapo mikoa ya Arusha, Dodoma, Mbeya, Tanga na Mwanza na Halmashauri zote 41 za Mikoa hiyo zinatumia mfumo huu na Halmashauri nyingine saba (7) za Manispaa za Shinyanga, Kahama na Mtwara Mikindani;

Kigoma Ujiji, Chalinze, Songea na Nzega Mji. Kufuatia matumizi ya mfumo huu, wananchi wanapata huduma zifuatazo; mipangomiji, upimaji, uthamini, umikilishaji na usajili wa hati na nyaraka za kisheria. Kupitia utoaji wa huduma mbalimbali za ardhi, Serikali ilikusanya shilingi bilioni 156.5 sawa na asilimia 62.6 ya lengo la shilingi bilioni 250.

p) Sekta ya Utalii

64. Katika mwaka 2024/25, Sekta ya Utalii iliidhinishiwa shilingi bilioni 708.89 ambapo shilingi bilioni 623.17 zilitolewa, sawa na asilimia 87.9. Katika kipindi hicho, Serikali kwa kushirikiana na wadau imebaini vivutio vipya vya utalii 337. Katika kuboresha sekta ya utalii idadi ya watalii wa nje na ndani iliongezeka hadi kufikia 2,193,322 mwaka 2024/25 kutoka 1,994,242 mwaka 2023/24. Aidha, mapato yameongezeka kutoka dola za Marekani bilioni 3.3 kwa mwaka 2023 hadi dola za Marekani bilioni 3.9 kwa mwaka 2024. Vilevile, idadi ya watalii wa ndani iliongezeka kutoka 1,084,737 mwaka 2023 hadi 1,976,009 mwaka 2024 na kuongeza mapato hadi shilingi bilioni 1,027 mwaka 2024 ikilinganishwa na lengo la shilingi bilioni 968.75, sawa na asilimia 105.91.

q) Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi – PPP

65. Katika mwaka 2024/25, Serikali iliendelea kutekeleza Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Sura 103 ambapo katika kipindi hicho Kituo cha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi *(PPP Centre)* kiliwezeshwa kuanza utekelezaji wa majukumu yake kwa kuidhinishiwa bajeti ya shillingi bilioni 18.46 ambapo shilingi bilioni 11.11 zilitolewa, sawa na asilimia 60.2.

Miradi nane (8) ya maendeleo ilifanyiwa uchambuzi na kuidhinishwa na Serikali kwa ajili ya utekelezaji kupitia utaratibu wa PPP ambapo miradi mitatu (3) yenye mtaji wa shilingi bilioni 718.23 imeanza utekelezaji ikiwemo: mradi wa huduma ya usafiri wa mabasi katika Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) Awamu ya Kwanza na ya Pili pamoja na Mradi wa Ujenzi na Uendeshaji wa Jengo la Biashara la DDC Kariakoo. Miradi mitano (5) inaendelea na hatua za ununuzi wa wabia kutoka sekta binafsi ikiwemo: Mradi wa Barabara ya haraka (*Expressway)* Kibaha - Chalinze – TANROAD; Mradi wa Hotel ya nyota 4 na Jengo la Biashara - JNIA - TAA; Mradi wa Vituo vya Ukaguzi wa Lazima wa vyombo vya Moto - TPFCS; na Mradi wa Mabweni ya wanafunzi - Chuo cha Biashara (CBE). Aidha, katika kipindi hicho Mamlaka za Serikali za Mitaa ziliibua miradi mbalimbali ya maendeleo inayofaa kutekelezwa kwa utaratibu wa PPP na kazi ya upembuzi yakinifu wa miradi hiyo inaendelea ikiwemo Awamu ya 3 na 4 ya Mradi wa DART, mradi wa Barabara ya haraka (*Expressway)* Chalinze - Morogoro na mradi wa Barabara ya Igawa -Tunduma. Vilevile, Serikali iliendelea kutoa mafunzo kuhusu dhana ya PPP na Sheria ya PPP pamoja na kuhamisha wadau

kutumia fursa zilizopo kwenye Sheria hiyo ikiwa ni njia mbadala ya kugharamia miradi ya maendeleo ambapo wadau 3,177 walipata mafunzo.

r) Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi

66. Serikali ilitekeleza shughuli za uhifadhi na usimamizi endelevu wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na:

(i) **Hifadhi ya Bioanuai:** Katika kuimarisha hifadhi ya Bioanuai, Serikali ilihamasisha upandaji na utunzaji wa miti katika Halmashauri za Wilaya ambapo jumla ya miti 224,795,501 ilipandwa. Aidha, ili kuhakikisha upotevu wa misitu na bioanuai unadhibitiwa, Serikali ilisimamia utekelezaji wa katazo la matumizi ya kuni na mkaa kwa taasisi zinazolisha watu zaidi ya 100 kwa siku ambapo jumla ya taasisi 921 zilianza kutumia nishati safi ya kupikia.

(ii) **Udhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira:** Serikali imeendelea kuratibu udhibiti wa uchafuzi wa mazingira ambapo jumla ya viwanda 44 vya urejelezaji wa taka aina za plastiki, chuma chakavu, mafuta machafu, tairi chakavu, taka za kielektroniki na taka ozo katika Mkoa wa Dar es Salaam vimejengwa vyenye uwezo wa kuchakata tani 12,926 za taka kwa mwaka. Aidha, kaguzi za mazingira katika miradi 11,514 zilifanyika ikiwemo viwanda, migodi, mabomba ya mafuta, mitambo ya gesi na mafuta pamoja na nishati ya umeme. Vilevile, vibali 275 vya kusafirisha ndani na nje ya nchi, kuhifadhi na kukusanya taka hatarishi zikiwemo taka za kielektroniki vilitolewa na tani 1,107.68 za taka ziliteketezwa.

(iii) **Mabadiliko ya Tabianchi:** Katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, Serikali ilifanya marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 ili kujumuisha masuala ya mabadiliko ya tabianchi. Mabadiliko haya yamewezesha kuanzishwa kisheria Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni (National Carbon Monitoring Centre - NCMC) kilichopo mkoani Morogoro chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais ili kuimarisha uratibu wa masuala ya kaboni nchini. Aidha, Serikali imeendelea kushirikiana na nchi wanachama wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabia nchi ambapo kupitia ushiriki katika Mkutano wa 29 (COP29) Tanzania iliweza kukusanya takriban kiasi cha dola za Marekani milioni 512 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Mabadiliko ya Tabia nchi. Vilevile, jumla ya miradi 78 ya biashara ya kaboni imesajiliwa na kiasi cha shilingi bilioni 48 zilipatikana.

(iv) **Uratibu na Tathmini ya Mazingira:** Serikali ilianzisha Mfumo Jumuishi wa taarifa za Mazingira nchini (Integrated Environmental Management System - IEMIS) na kutoa vyeti 1,609 vya tathmini ya athari kwa mazingira.

2.4 Fursa zilizojitokeza katika utekelezaji wa bajeti

67. Katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/25 fursa zilizojitokeza ni pamoja na:

(i) Ongezeko la mahitaji ya ujenzi wa miundombinu na huduma zinazoweza kugharamiwa kwa kutumia njia mbadala;

(ii) Ongezeko la mahitaji ya usambazaji wa nishati ya gesi asilia na umeme kwa ajili ya viwanda, vyombo vya moto, maeneo ya biashara na majumbani;

(iii) Uwepo wa Sera na Sheria zinazoweka mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji katika maeneo mbalimbali ikiwemo kilimo, maji, ardhi, mifugo, uvuvi, madini, viwanda, nishati safi, biashara ya kaboni na usafirishaji;

(iv) Uwepo wa uhitaji wa huduma za usafirishaji wa abiria na mizigo kwa haraka baina ya vituo vya usafirishaji (SGR, ndege na bandari) na maeneo mbalimbali yakiwemo kongani za viwanda na maeneo ya biashara;

(v) Upatikanaji wa teknolojia na miundombinu ya kisasa katika soko inayoweza kutumika katika kuboresha utoaji wa huduma katika sekta mbalimbali;

(vi) Uwepo wa teknolojia ya malipo bila fedha taslimu inayorahisisha huduma na ukusanyaji wa mapato;

(vii) Kuwepo kwa fursa za uwekezaji katika viwanda ili kupunguza uagizaji wa bidhaa nje ya nchi na kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni;

(viii) Uwepo wa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi ambazo zinachochea mahitaji ya tiba utalii nchini;

(ix) Kuongezeka kwa soko la ndani kutokana na ukuaji wa kipato na idadi ya watu;

(x) Uwepo wa fursa za biashara kupitia masoko ya kikanda ikiwemo EAC, SADC na AfCFTA;

(xi) Kuongezeka kwa soko la nje hususan Afrika na Asia la mazao ya chakula, mifugo na uvuvi kutokana na ukuaji wa idadi ya watu;

(xii) Maendeleo ya miundombinu ya kimkakati (bandari, reli, barabara, umeme na TEHAMA) yanayowezesha uwekezaji na shughuli za uzalishaji;

(xiii) Uwepo wa fursa ya uhifadhi wa mazingira na biashara ya kaboni kupitia ununuzi wa viwango vya kaboni kwa ajili ya kudhibiti uharibifu wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;

(xiv) Uwepo wa fursa za uwekezaji katika rasilimali za uchumi wa buluu zikiwemo madini, uvuvi, maji, nishati, kilimo, utalii, usafiri na usafirishaji;

(xv) Uwepo wa sekta isiyo rasmi ambayo ina nafasi ya kuongeza wigo wa kodi;

(xvi) Uwepo wa fursa katika taasisi na mashirika ya umma kuzalisha na kuchangia mapato ya Serikali;

(xvii) Uwepo wa biashara ya milki (real-estate) inayochangia ongozeko la Pato la Taifa; na

(xviii) Uwepo wa amani, umoja na utulivu nchini.

2.5 Hatua za kuchukua ili Kutumia Fursa Zilizopo

68. Ili kuweza kunufaika na fursa mbalimbali zilizopo nchini, ni vema masuala yafuatayo yakatekelezwa:

(i) Kuandaa na kutekeleza mikakati ya kutafuta vyanzo mbadala vya fedha kwa ajili ya ugharamiaji wa miradi na ulipaji wa madeni ili kupunguza utegemezi kwa Serikali katika utekelezaji wa miradi;

(ii) Kuwekeza katika miundombinu ya usambazaji wa nishati ya gesi asilia na umeme kwa ajili ya viwanda, vyombo vya moto, maeneo ya biashara na majumbani;

(iii) Kuelimisha na kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika sekta mbalimbali za uzalishaji na utoaji wa huduma zikiwemo viwanda, elimu, madini, kilimo, mifugo, uvuvi, maji, usafiri na usafirishaji;

(iv) Kujenga, kukarabati na kuunganisha miundombinu ya usafirishaji na maeneo ya kiuchumi ili kuwezesha uzalishaji na usafirishaji wa haraka wa bidhaa na huduma;

(v) Kuwekeza katika tafiti na maendeleo, sayansi na teknolojia ili kuendeleza miundombinu, utoaji wa huduma na uzalishaji katika maeneo ya vipaumbele ikiwemo ujuzi wa TEHAMA kwa vijana;

(vi) Kuwekeza katika viwanda kwa kushirikiana na sekta binafsi ili kuongeza uzalishaji na kupunguza uagizaji wa bidhaa muhimu kutoka nje ya nchi ikiwemo viwanda vya dawa na vifaa tiba;

(vii) Kuingiza huduma za afya bobezi katika maboresho ya miundombinu ya hospitali za rufaa na kitaifa na kushirikiana na wataalamu wa kimataifa kwa ajili ya kuongeza ujuzi ili kuvutia utalii wa tiba nchini;

(viii) Kuhamasisha na kuimarisha usimamizi wa matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika utoaji wa huduma ikiwemo mifumo ya stakabadhi za ghala, biashara ya kaboni, malipo na ukusanyaji wa mapato ili kuongeza tija na kudhibiti upotevu wa mapato;

(ix) Kutekeleza miradi ya uhifadhi wa mazingira, mabadiliko ya tabianchi na biashara ya kaboni ili kunufaika na fursa hizo;

(x) Kuboresha na kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi, kutoa elimu, kuhamasisha pamoja na kuweka na kutekeleza mikakati ya kurasimisha sekta isiyo rasmi;

(xi) Kuongeza uwekezaji katika miundombinu wezeshi ya uvuvi wa bahari kuu ikiwemo ununuzi wa meli za uvuvi;

(xii) Kuongeza matumizi ya magari yanayotumia nishati ya gesi na umeme, yakiwemo ya Serikali ili kupunguza matumizi ya mafuta na uchafuzi wa mazingira;

(xiii) Kuimarisha Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha ardhi kwa kushirikiana na sekta binafsi;

(xiv) Kuwekeza katika sekta ya milki kwa kutambua vipande vya ardhi na majengo kwa kushirikiana na sekta binafsi;

(xv) Kufanya marekebisho ya Sheria Na. 5 ya Mwaka 2019 ya usambazaji maji na usafi wa mazingira ili kuvutia sekta binafsi katika eneo la usambazaji maji na usafi wa mazingira; na

(xvi) Kuimarisha usimamizi kwa mashirika ya umma kufanya biashara ili kuongeza uchangiaji wa mapato kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na kupunguza utegemezi kwa Serikali.

Kiambatisho Na. 1C

3 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAELEKEZO YA MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2025/26

3.1 Utangulizi

69. Sehemu hii inaelezea mapitio ya utekelezaji wa maelekezo yaliyotolewa katika Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2025/26 kwa kuzingatia tathmini na uchambuzi wa bajeti za mafungu ya kisekta kwa mwaka 2025/26 na maoni ya wadau yaliyotolewa katika vikao mbalimbali kuhusu maandalizi na utekelezaji wa bajeti ya Serikali.

3.2 Sura ya Bajeti ya Mwaka 2025/26

70. Kufuatia vipaumbele vya Serikali na maboresho mbalimbali ya kisera na mifumo ya ukusanyaji mapato yaliyofanyika, Sura ya bajeti ya Serikali ilibadilika kutoka mapendekezo ya shilingi bilioni 55,061.6 hadi shilingi bilioni 56,490.2, sawa na ongezeko la asilimia 2.6. Ongezeko hilo lilitokana na maboresho ya maoteo ya mapato ya ndani, misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. **Jedwali Na.3.1** linaonesha mapendekezo ya Sura ya Bajeti pamoja na Bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka 2025/26:

Jedwali Na.3.1: Mapendekezo ya Sura ya Bajeti pamoja na Bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka 2025/26

			Shilingi Bilioni	
Mapato	**2025/26 Mwongozo**	**2025/26 Bajeti Iliyoidhinishwa**	**Ongozeko/ Upungufu**	**Ufanisi (%)**
	A	**B**	**B - A**	
Mapato ya Ndani - Serikali Kuu	**37,402.7**	**38,785.6**	**1,382.9**	**3.7**
(i) Mapato ya Kodi na yasiyo ya Kodi (TRA)	31,426.1	34,103.9	2,677.8	8.5
(ii) Mapato yasiyo ya Kodi	5,976.6	4,681.7	-1,294.8	-21.7
Mapato ya Halmashauri	**1,559.8**	**1,680.5**	**120.7**	**7.7**
Misaada na Mikopo nafuu kutoka Washirika wa Maendeleo	**6,691.9**	**7,116.9**	**425.0**	**6.4**
(i) Misaada na Mikopo nafuu - GBS	1,741.0	1,741.0	0.0	0.0
(ii) Misaada na Mikopo nafuu ya Miradi	4,761.2	5,186.2	425.0	8.9
(iii) Misaada na Mikopo nafuu ya Kisekta	189.7	189.7	0.0	0.0
Mikopo ya Ndani na Nje	**9,407.2**	**8,907.2**	**-500.0**	**-5.3**
(i) Mikopo ya Nje	3,129.0	2,629.0	-500.0	-16.0
(ii) Mikopo ya Ndani	2,952.6	2,952.6	0.0	0.0
(iii) Mikopo ya Ndani - Rollover	3,325.6	3,325.5	0.0	0.0
JUMLA YA MAPATO YOTE (A+B+C+D+E)	**55,061.6**	**56,490.2**	**1,428.6**	**2.6**
Matumizi				
Matumizi ya Kawaida	**38,602.2**	**38,996.5**	**394.3**	**1.0**
(i) Mfuko Mkuu wa Serikali	**17,340.3**	**16,637.5**	**-702.8**	-4.1
- Malipo ya Riba Ndani	3,697.3	3,697.3	0.0	0.0
- Malipo ya Mtaji Ndani (Rollover)	3,325.6	3,325.6	0.0	0.0
- Malipo ya Mtaji Nje	4,389.7	4,389.7	0.0	0.0
- Malipo ya Riba Nje	2,796.4	2,796.4	0.0	0.0
- Michango ya Serikali kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii	2,428.5	2,428.5	0.0	0.0
- Matumizi Mengine ya Mfuko Mkuu	702.8	0.0	-702.8	-100.0
(ii) Mishahara	**13,454.2**	**13,174.2**	**-280.0**	**-2.1**
(iii) Matumizi Mengineyo (OC)	**6,365.6**	**7,757.1**	**1,391.5**	**21.9**
- Malipo ya Madeni yaliyohakikiwa	200.0	200.0	0.0	0.0
- Matumizi ya Halmashauri (own source)	937.3	1,067.1	129.7	13.8
- Matumizi mengineyo	5,228.3	6,490.1	1,261.8	24.1
(iv) Ruzuku ya Maendeleo	**1,442.0**	**1,427.7**	**-14.4**	-1.0
- Bodi ya Mikopo	931.1	916.7	-14.4	-1.5
- Elimumsingi bila Ada	511.0	511.0	0.0	0.0
			0.0	
Matumizi ya Maendeleo	**16,459.4**	**17,493.7**	**1,034.3**	**6.3**
(i) Fedha za Ndani	**11,508.5**	**12,117.8**	**609.3**	**5.3**
o/w Malipo ya Madeni yaliyohakikiwa	800.0	500.0	-300.0	-37.5
o/w Ugharamiaji wa SGR	1,800.0	1,511.0	-289.0	-16.1
o/w Ugharamiaji wa Miradi wa Umeme wa Julius Nyerere	500.0	350.0	-150.0	-30.0
o/w Matumizi ya Halmashari (own source)	622.5	613.4	-9.0	-1.4
o/w Miradi mingine	7,786.1	9,143.4	1,357.3	17.4
(ii) Fedha za Nje	**4,950.9**	**5,375.9**	**425.0**	8.6
JUMLA YA MATUMIZI YOTE (F+G)	**55,061.6**	**56,490.2**	**1,428.6**	2.6
NAKISI YA BAJETI (asilimia ya Pato la Taifa)	**3%**	**3%**		

Chanzo: Wizara ya Fedha

3.3 Utekelezaji wa Maelekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2025/26

71. Mafungu yameendelea kutekeleza na kuzingatia maelekezo katika hatua zote za maandalizi na utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2025/26. Uchambuzi uliofanyika unaonesha baadhi ya maelekezo yaliyotekelezwa ambayo ni pamoja na:

a) Maandalizi ya Mpango na Bajeti

72. Maafisa Masuuli wameendelea kuzingatia malengo na shabaha za Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26, Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2025/26, mpango mkakati wa taasisi na maagizo mengine yaliyotolewa na Serikali. Aidha, Maafisa Masuuli walizingatia ratiba ya uandaaji na uwasilishwaji wa bajeti pamoja na matumizi sahihi ya vizio vya vipimo na namba za mageresho ya kibajeti (GFS Codes 2014) wakati wa uandaaji na uwasilishaji wa bajeti.

b) Maelekezo ya Kuimarisha Ukusanyaji wa Mapato

73. Mafungu yameendelea kusimamia maelekezo kuhusu matumizi ya mashine za EFD kwa kutoa na kudai risiti za kielektroniki kwa malipo yote yanayofanywa kwa wazabuni na wakandarasi na pia kutoingia mikataba na kandarasi na wazabuni wasiotumia mashine hizo. Pia, Mafungu yameendelea kuratibu maboresho na uunganifu wa mifumo na uanzishwaji wa madirisha ya pamoja ya kielektroniki ya utoaji wa huduma na ukusanyaji wa mapato kwa taasisi zinazotoa huduma kwa pamoja na kuwezesha utoaji wa namba jumuishi kwa lengo la kurahisisha ulipaji kodi, ada na tozo za Serikali kwa wateja na hivyo kuongeza uhiari wa ulipaji wake. Pamoja na uzingatiwaji huu wa maelekezo, Serikali inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuhakikisha mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji wa mapato inaendelea kuunganishwa na kutumika ipasavyo.

c) Bajeti za Mishahara na Matumizi Mengineyo

74. Maafisa Masuuli wameendelea kuzingatia maelekezo ya kutenga bajeti kwa ajili ya mishahara na uendeshaji wa shughuli mbalimbali za Serikali. Aidha, masuala yaliyozingatiwa ni pamoja na: bajeti ya mishahara ya watumishi waliopo na ajira mpya; kubadilisha kada/kazi; upandishaji vyeo; uteuzi; uhamisho wa watumishi; uendelezaji wa rasilimali watu; na matumizi ya Mfumo Jumuishi wa Usimamizi wa Taarifa za Rasilimaliwatu na Mishahara (e-Watumishi).

d) Maelekezo Mahsusi kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa

75. Halmashauri za Serikali za Mitaa zimeendelea kutekeleza maelekezo mbalimbali kwa mwaka 2025/26 kwa ajili ya kuimarisha huduma na utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo yao. Shilingi bilioni 16.67 zimetengwa

kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi za kata, vijiji na mitaa, Shilingi bilioni 21.83 zimetengwa kwa ajili ya ukamilishaji wa miradi viporo iliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi na shilingi bilioni 14.14 kwa ajili ya kulipa madeni ya wazabuni. Aidha, Shilingi bilioni 123.42 zimetengwa kwa ajili ya mikopo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, Shilingi bilioni 150.75 zimetengwa kwa ajili ya miradi ya kimkakati ikiwemo ujenzi wa vitega uchumi, viwanda, machinjio, minada na hospitali mpya. Halmashauri pia zimeendelea kuzingatia matumizi bora ya ardhi kwa kupanga na kujenga majengo ya ghorofa katika miradi mipya ya majengo ya utawala, elimu, masoko na afya.

76. Halmashauri zimepanga kuwekeza katika miradi ya maendeleo ikiwemo upimaji na urasimishaji wa ardhi kwa kutenga Shilingi bilioni 15, kulipa fidia kwa maeneo yaliyotwaliwa kwa kutenga Shilingi bilioni 22.79 na utekelezaji wa mipango ya hifadhi ya mazingira kwa kutenga Shilingi bilioni 1.02. Aidha, bajeti imetengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya ustawi wa jamii, kuunganisha mifumo ya TEHAMA katika vituo vya huduma, usimamizi wa mikopo kwa vikundi na utekelezaji wa mipango ya wajibu wa kampuni kwa jamii (CSR). Vilevile, Shilingi bilioni 631.13 zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwa kuzingatia madaraja ya uchangiaji wa mapato ya ndani, ikilenga kuongeza ufanisi na utoaji wa huduma kwa wananchi.

e) Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

77. Maafisa Masuuli wameendelea kutekeleza Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo (DCF) ulioboreshwa na Mpango Kazi wake ikiwemo: kufuatilia mikataba ya uwili, kikanda na kimataifa; kuwasilisha kwa wakati makadirio ya michango ya uanachama; na kuhamasisha matumizi ya diplomasia ya uchumi.

f) Ujenzi wa Miundombinu na Ofisi za Wizara na Taasisi za Umma Katika Mji wa Serikali Jijini Dodoma

78. Maafisa Masuuli wamezingatia mahitaji ya kukamilisha ujenzi wa miundombinu na ofisi za Wizara na Taasisi katika Mji wa Serikali – Dodoma ambapo hadi kufikia Septemba, 2025 wastani wa ukamilishaji wa majengo ya awamu ya pili umefikia asilimia 92.9.

g) Uchumi wa Kidigitali

79. Shilingi bilioni 4.90 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa vifaa vya mfumo jumuishi wa kisekta wa kubadilishana taarifa baina ya sekta za umma na binafsi nchini. Jumla ya mifumo 898 imeunganishwa kupitia miundombinu 14 ya kitaifa na kisekta ambayo kati ya mifumo hiyo, 514 ni ya Serikali na 384 ni ya sekta binafsi ambayo imewezesha miamala 1,051 kufanyika kwa wakati mmoja. Mifumo hii imeunganishwa na mfumo wa utambuzi wa watu (**Jamii Namba**).

h) Masuala ya Watu Wenye Ulemavu

80. Maafisa Masuuli wameendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu wezeshi katika vituo na taasisi zinazotoa huduma kwa watu wenye ulemavu. Aidha, wameendelea kutekeleza Mwongozo wa Utekelezaji, Ujumuishwaji na Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu Tanzania wa mwaka 2022 ambapo Shilingi bilioni 1 zimetengwa kwa ajili ya Mfuko wa Taifa wa Watu Wenye Ulemavu ili kutekeleza afua zinazolenga kuwawezesha watu wenye ulemavu kiuchumi, kijamii na kielimu. Vilevile, mfumo wa PD-MIS na Albino/PD-MIS *Mobile App* imeunganishwa na mifumo mingine ya kitaifa ili kurahisisha ukusanyaji, ufuatiliaji na uchambuzi wa taarifa na hivyo kuimarisha utoaji wa huduma kwa Watu Wenye Ulemavu.

i) Uandaaji wa Bajeti yenye Mlengo wa Kijinsia

81. Maafisa Masuuli wameendelea na utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto Awamu ya Pili (MTAKUWWA II – 2024/25 – 2028/29) ambapo pamoja na mambo mengine Mawaziri 16 wa Wizara za Kisekta wametia saini matamko ya utayari wa ushirikiano katika utekelezaji wa Mpango. Pia, mafunzo yamefanyika kwa maafisa dawati wa jinsia na maafisa bajeti kutoka katika Wizara, Idara za Serikali na Taasisi ili kuwajengea uwezo katika kupanga na kutekeleza bajeti zenye mlengo wa kijinsia.

j) Masuala ya Muungano

82. Maafisa Masuuli wameendelea kuzingatia na kutekeleza maelekezo kuhusu masuala ya Muungano ili kuendelea kuulinda, kuudumisha na kuimarisha Muungano kwa maendeleo ya nchi. Maelekezo yaliyozingatiwa ni pamoja na kutenga bajeti kwa ajili ya kuwezesha shughuli za ushirikiano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambapo programu na miradi mbalimbali imeendelea kutekelezwa katika pande mbili za Muungano kwa lengo la kuboresha ustawi wa kiuchumi na kijamii kwa wananchi. Aidha, hoja za Muungano zimeendelea kufanyiwa kazi ili kudumisha umoja, mshikamano, amani na utulivu wa Taifa.

k) Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi

83. Maafisa Masuuli wameendelea kutekeleza masuala yanayohusu uhifadhi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi kwa kusimamia Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022- 2032) na Mwongozo wa Biashara ya Kaboni wa Mwaka 2022.

l) Afua za Lishe

84. Maafisa Masuuli wameendelea kuzingatia utekelezaji wa Mpango wa Pili Jumuishi wa Taifa wa Utekelezaji wa Masuala ya Lishe (NMNAP – II) wa Mwaka 2021/22 – 2025/26 kwa kutenga bajeti kupitia *objective Y* kwa ajili ya kutoa elimu kwa jamii juu ya matumizi sahihi ya chakula yanayoendana na

lishe, kuongeza upatikanaji wa huduma za lishe bora ngazi ya jamii na vituo vya kutolea huduma za jamii, kuimarisha ushirikishaji wa sekta mbalimbali na sekta binafsi katika masuala ya lishe.

m) VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza

85. Maafisa Masuuli wameendelea kutenga bajeti kupitia *Objective A* kwa ajili ya kutekeleza matakwa ya Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa VVU na UKIMWI, SURA 431, Sera ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI ya Mwaka 2001 na Mkakati wa Tano wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI Tanzania 2021/22 - 2025/26 (NMSF-V), Mwongozo na Waraka Na. 2 wa Utumishi wa Umma wa Mwaka 2014 kuhusu kudhibiti VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa Mahali pa Kazi katika Utumishi wa Umma na kutekeleza afua za kudhibiti magonjwa ya afya ya akili kwa watumishi wa umma.

n) Mapambano Dhidi ya Rushwa

86. Maafisa Masuuli wameendelea kutenga bajeti ya utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Nne 2023 - 2030 sanjari na usimamizi wa utekelezaji wake. Mkakati unatekelezwa kwa mujibu wa Waraka Mkuu wa Utumishi wa Umma Na. 1 wa Mwaka 2024. Lengo Kuu la Awamu ya Nne ya Mkakati ni Kuwa na Jamii iliyostawi na yenye Mifumo Madhubuti ya kukuza uadilifu na isiyovumilia rushwa.

o) Mapambano Dhidi ya Dawa za kulevya

87. Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya kwa kuweka uwajibikaji wa wadau katika udhibiti wa dawa za kulevya; kuimarisha tafiti kuhusu dawa za kulevya; kuimarisha doria na operesheni za mara kwa mara; na kufanya kaguzi katika vituo vya forodha, vyombo vya usafiri, kampuni za usafirishaji vifurushi na kwenye kampuni zinazojihusisha na biashara za kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya. Aidha, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali Serikali inaendelea kuimarisha huduma za tiba kwa waraibu wa dawa za kulevya pamoja na kutoa elimu kwa umma kuhusu dawa za kulevya nchini.

p) Masuala ya Haki Jinai

88. Maafisa Masuuli wa Wizara na Taasisi zinazohusika katika mnyororo wa Haki Jinai wameendelea kutekeleza mipango na mikakati ya kuimarisha haki jinai nchini kwa kuwajengea uwezo watumishi kupitia mafunzo ya muda mrefu na mfupi ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa weledi na ufanisi. Miundo ya kiutumishi ya baadhi ya taasisi zinazohusika na utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai imeendelea kufanyiwa marejeo kwa lengo la kuongeza uwajibikaji na ufanisi katika taasisi hizo. Aidha, maboresho haya yanahusisha kuunda na kuimarisha mifumo ya TEHAMA ili kurahisisha utendaji kazi na kuwezesha kubadilishana taarifa baina ya taasisi za Haki Jinai.

q) Uandaaji na Uwasilishaji wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti

89. Maafisa Masuuli wanaendelea kutekeleza matakwa ya Kifungu cha 55 cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Kanuni zake kwa kuandaa na kuwasilisha Wizara ya Fedha na Tume ya Mipango taarifa za utekelezaji wa bajeti kila robo mwaka ndani ya siku 30 baada ya kukamilika kwa robo ya mwaka na taarifa za mwaka kabla ya tarehe 15 Oktoba. Aidha, nakala za taarifa hizi kutoka Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa huwasilishwa Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI; Taasisi na Mashirika ya Umma huwasilishwa Ofisi ya Msajili wa Hazina na nakala kwa Wizara mama. Hata hivyo, kuna umuhimu wa kufanya *harmonization* ya miundo ya taarifa zinazohitajika na wadau mbalimbali Serikalini.

r) Maelekezo kuhusu Maandalizi ya Uchaguzi Mkuu

90. Maandalizi stahiki yamefanyika kwa wote wanaohusika na masuala ya uchaguzi mkuu na utekelezaji unaendelea kwa kuzingatia sheria na kadri ya maelekezo mahsusi ya Serikali na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi.

91. Pamoja na uzingatiwaji wa maelekezo yaliyobainishwa katika mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Mwaka 2025/26, utekelezaji wa maelekezo mengine unaendelea katika kipindi kilichobaki cha mwaka wa fedha 2025/26. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa maelekezo hayo yanatekelezwa ipasavyo**.**

3.4 Mwenendo wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2025/26

92. Bajeti ya Serikali iliyoidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mwaka 2025/26 ni shilingi bilioni 56,490.3. Bajeti inagharamiwa na mapato ya ndani shilingi bilioni 40,466.1 na misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo shilioni bilioni 1,069.9. Aidha, nakisi ya bajeti inagharamiwa na mikopo ya ndani shilingi bilioni 6,278.2 na mikopo ya nje shilingi bilioni 8,676.1.

93. Katika kipindi cha julai hadi Novemba 2025, Serikali ilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 22,881.0 kutoka vyanzo vya ndani na nje sawa na asilimia 98.6 ya lengo la kipindi hicho. Matumizi ya Serikali yalikuwa shilingi bilioni 22,937.6, sawa na asilimia 98.8. Matumizi ya shilingi bilioni 56.5 yaliyozidi mapato yaligharamiwa na mkopo wa muda mfupi kutoka Benki Kuu.

3.4.1 Mapato

94. Katika kipindi cha Julai hadi Novemba 2025, mapato yalifikia shilingi bilioni 15,901.6, sawa na asilimia 98.2 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 16,193.6 katika kipindi hicho. Kati ya mapato hayo: mapato ya kodi yalikuwa shilingi bilioni 13,105.5; mapato mengine (mapato yasiyo ya kodi) yalikuwa shilingi bilioni 2,429.1; na misaada ilifikia shilingi bilioni 367.0.

3.4.2 Matumizi

95. Katika kipindi cha Julai hadi Novemba 2025, jumla ya matumizi ya Serikali bila kujumuisha malipo ya mtaji wa deni ilikuwa shilingi bilioni 20,831.1, sawa na asilimia 98.9 ya lengo la shilingi bilioni 21,068.6. Aidha, mchanganuo wa matumizi umeainishwa katika **Jedwali Na 3.2**.

Jedwali Na. 3.2: Matumizi ya Fedha za Serikali, Julai – Novemba 2025

Matumizi	Makadirio	Halisi	Ufanisi
	Shilingi Bilioni		
Mishahara na stahiki za watumishi	3,702.5	3,832.1	103.5%
Gharama za bidhaa na huduma	2,717.8	3,375.7	124.2%
Malipo ya riba	2,613.9	2,202.1	84.2%
Ruzuku kwenye taasisi za uwekezaji	56.7	54.2	95.6%
Ruzuku na michango	9,503.0	9,309.5	98.0%
Mafao na misaada ya kijamii	249.4	192.3	77.1%
Gharama nyingine	851.6	567.8	66.7%
Uwekezaji katika mali zisizo za kifedha	1,373.8	1,297.5	94.5%
Jumla Kuu	**21,068.6**	**20,831.1**	**98.9%**

3.4.3 Kugharamia Nakisi

96. Katika kipindi cha Julai hadi Novemba 2025, Serikali ilipokea mikopo kutoka nje na ndani jumla ya shilingi bilioni 6,979.4, sawa na asilimia 99.4 ya lengo la kipindi hicho. Aidha, malipo ya mitaji yalikuwa shilingi bilioni 876.0 kwa mikopo ya ndani na shilingi bilioni 1,230.4 kwa mikopo ya nje. Hivyo, mikopo halisi kwa ajili ya ugharamiaji wa nakisi ni shilingi bilioni 4,873.0.

Kiambatisho Na. 1D

MUUNDO WA MTEF 2026/27 - 2028/29

Maelezo ya Kisera kwa Ufupi

(i) Maelezo ya Waziri/Mkuu wa Mkoa/Meya au Mwenyekiti wa Halmashauri/Mwenyekiti wa Bodi/Baraza

(ii) Maelezo ya Afisa Masuuli.

Sura ya 1: Uchambuzi wa Hali Iliyopo

1.1 Uchambuzi wa Wadau

1.2 Uchambuzi wa Uwezo, Udhaifu, Fursa na Changamoto

1.3 Masuala Muhimu ikijumuisha mawasilisho ya usimamizi wa vihatarishi

Sura ya 2: Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti

2.1 Mapitio ya Utekelezaji - 2024/25

2.1.1 Muhtasari wa Fedha zilizovuka mwaka 2023/24 kwa kila programu na maelezo ya matumizi 2024/25

2.1.2 Makadirio ya Mapato kwa Mwaka yakilinganishwa na Mapato Halisi

2.1.3 Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka yakilinganishwa na Matumizi Halisi

2.1.4 Muhtasari wa Malengo yaliyopangwa yakilinganishwa na Malengo yaliyofikiwa

2.2 Mapitio ya Utekelezaji kwa Nusu Mwaka - 2025/26

2.2.1 Muhtasari wa Fedha zilizovuka mwaka 2024/25 kwa kila programu na maelezo ya matumizi 2025/26

2.2.2 Makadirio ya Mapato kwa Mwaka yakilinganishwa na Mapato Halisi

2.2.3 Makadirio ya Matumizi ya Mwaka yakilinganishwa na Matumizi Halisi

2.2.4 Muhtasari wa Malengo kwenye MTEF yakilinganishwa na Mafanikio yaliyopatikana

2.3 Changamoto zilizojitokeza 2024/25 na Mikakati ya kukabiliana na changamoto

Sura ya 3: Makadirio ya MTEF (2026/27 - 2028/29)

3.1 Muhtasari wa Makadirio ya Bajeti ya Mwaka na Miaka Miwili inayofuata (Fomu Na.1)

3.2 Malengo Makuu, Shabaha na Shughuli zitakazofanyika (Fomu Na. 3A)

3.3 Makadirio ya Matumizi ya Mengineyo kwa Mwaka na Miaka Miwili inayofuata (Fomu Na. 3B)

3.4 Muhtasari wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida (Fomu Na. 3C)

3.5 Makadirio na Maoteo ya Mapato (Fomu Na.4)

3.6 Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo kwa Mwaka na Miaka Miwili inayofuata (Fomu Na.6)

3.7 Muhtasari wa Matumizi ya Miradi ya Maendeleo (Fomu Na. 6.1)

3.8 Mfumo wa Matokeo wa Kitaasisi (Fomu Na.7)

3.9 Muhtasari wa Makadirio ya Mishahara kwa kila Fungu (Fomu Na. 8A)

3.10 Muhtasari wa Makadirio ya Mishahara kwa Kifungu (Fomu Na. 8B)

3.11 Kipengele Na.I – Muhtasari wa Wafanyakazi Walio kwenye Orodha ya Malipo ya Mishahara (Fomu Na. 8C)

3.12 Kipengele Na.II - Muhtasari wa Watumishi Wenye Kibali Wanaotarajiwa Kuajiriwa Katika Mwaka husika (Fomu Na. 8D)

3.13 Kipengele Na.III - Muhtasari wa Wafanyakazi Wanaotarajiwa Kuajiriwa (Fomu Na. 8E)

3.14 Orodha ya Wafanyakazi Wanaotarajiwa Kustaafu (Fomu Na. 8F)

3.15 Jedwali la Mishahara kulingana na Ikama (Fomu Na. 9)

3.16 Fomu ya Taarifa za Miradi (Fomu Na. 10A)

3.17 Muhtasari wa Makadirio ya Bajeti ya Miradi kwa mwaka unaofuata kwa Fungu (Fomu Na. 10C)

Kiambatisho Na. 1E

RANDAMA YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/27

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

JINA LA FUNGU ....

FUNGU NA ....

RANDAMA YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2026/27

Imetayarishwa na;

Anuani ya Fungu

Machi, 2026

YALIYOMO

VIFUPISHO

SURA YA KWANZA

1. UTANGULIZI

- 1.1. Dira
- 1.2. Dhima
- 1.3. Majukumu ya Fungu

SURA YA PILI

2. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA FUNGU YA MWAKA 2025/26

- 2.1. Taarifa ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati…
- 2.2. Tathmini ya Utekelezaji Bajeti hadi Februari 2026
  - 2.2.1. Taarifa ya Fedha Zilizovuka Mwaka 2024/25 (**Jedwali Na. 1**)
  - 2.2.2. Mapato/Maduhuli (**Jedwali Na. 2**)
  - 2.2.3. Matumizi ya Kawaida
  - 2.2.4. Miradi ya Maendeleo
- 2.3. Mafanikio ya Utekelezaji wa Bajeti
- 2.4. Changamoto (kama zipo) ambazo ni muhimu Kamati ya Bunge ikazifahamu na Mikakati ya Kuboresha Utekelezaji wa Bajeti

SURA YA TATU

3. MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2026/27

- 3.1. Vipaumbele vya Mpango na Bajeti
- 3.2. Makadirio ya Mapato
- 3.3. Makadirio ya Matumizi ya kawaida
  - 3.3.1. Kazi zitakazotekelezwa (kifungu kwa kifungu) (**Jedwali Na. 3**)
- 3.4. Makadirio ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo
  - 3.4.1. Miradi Itakayotekelezwa (**Jedwali Na. 4**)
- 3.5. Muhtasari wa Maombi ya Fedha kwa Mwaka 2025/26 (**Jedwali Na.5**)

  Muhtasari uoneshe maombi ya fedha kwa Fungu husika na mchanganuo wake

Jedwali Na. 1: Taarifa ya Fedha Zilizovuka Mwaka 2024/25

Geresho la Mradi	Jina la Mradi	Shughuli zilizoombewa Kibali	Fedha zilizovuka Mwaka 2024/25		
			Fedha zilizobaki Kufikia Juni, 2025	Fedha zilizotumika hadi Feb 2026	Kazi zilizotekelezwa
5401	Ujenzi wa...		68,213,114	45,490,000	Fedha zimetumika kukamilisha shughuli za kuweka tiles, kupaka rangi, kuweka milango na madirisha,

Jedwali Na. 2: **Tathmini ya Ukusanyaji Mapato ya Ndani / Maduhuli**

Mapato Yaliyoidhinishwa	Makusanyo Halisi	Ufanisi (Asilimia)	Sababu za Ufanisi

Jedwali Na. 3: Mchanganuo wa Fedha za Matumizi ya Kawaida Mwaka …

Geresho la Kifungu: Mfano 1001

Jina la Kifungu: Mfano Utawala na Rasilimali Watu

NA.	KASMA	MAELEZO YA KASMA	KIASI KILICHOTENGWA		MAELEZO YA MATUMIZI
			2025/26	2026/27	
1.	21111	Mishahara ya watumishi	500,000,000	600,000,000	Kitengo kinaomba kuidhinishiwa **shilingi 600,000,000** kwa ajili ya kulipa mishahara ya watumishi 30 walio katika masharti ya kudumu na malipo ya uzeeni. Kasma hii imeongezeka kwa

NA.	KASMA	MAELEZO YA KASMA	KIASI KILICHOTENGWA		MAELEZO YA MATUMIZI
			2025/26	2026/27	
					shilingi 100,000,000 kutokana ongezeko la watumishi watatu (3) katika kitengo.

Jedwali Na. 4: Mchanganuo wa Fedha za Matumizi ya Maendeleo Mwaka …

Geresho la Kifungu: Mfano 1001

Jina la Kifungu: Mfano Utawala na Rasilimali Watu

Geresho la Mradi	Jina la Mradi	Shughuli zilizopangwa kutekelezwa	Gharama za Mradi	
			Fedha za ndani	Fedha za nje
4321:	Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi (Primary Education Development Programme)	Kuimarisha Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) Awamu ya Pili – GPE LANES II	-	2,000,000

Jedwali Na. 5: Muhtasari wa Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka….

Maelezo			Bajeti 2026/27
1	Matumizi ya Kawaida	Mishahara	
		Matumizi Mengineyo	
	Jumla Ndogo		
2	Matumizi ya Maendeleo	Ndani	
		Nje	
	Jumla Ndogo		
Jumla Kuu			

Kiambatisho Na. 1F

MUUNDO WA TAARIFA YA KAMATI YA BAJETI

Ukurasa wa juu
Yaliyomo
Vifupisho vya maneno
Utangulizi
Sehemu hii itahusisha maelezo mafupi juu ya wajibu na majukumu ya Kamati katika usimamizi wa bajeti; orodha ya wajumbe na kumbukumbu za barua za uteuzi kwa mujibu wa sheria ya bajeti na orodha ya agenda zilizojadiliwa

1.0 Uendeshaji wa vikao
(Sehemu hii itahusisha ratiba na utaratibu wa uendeshaji wa vikao)

2.0 Mapitio ya Muhtasari wa kikao cha kamati kilichopita.
(Elezea kwa ufupi maazimio ya kikao kilichopita).

3.0 Ukusanyaji wa mapato na mgawanyo wa rasilimali:
- 3.1 Mwenendo wa ukusanyaji wa mapato;
- 3.2 Mgawanyo wa rasilimali kulingana na vipaumbele vya bajeti kama ilivyoainishwa kwenye mpango kazi (Bajeti ya matumizi ya kawaida na maendeleo);
- 3.3 Utaratibu wa ugawaji wa rasilimali kila mwezi kulingana na vipaumbele vya bajeti; na
- 3.4 Mgawanyo wa rasilimali fedha katika Idara na Vitengo.

4.0 Taarifa ya kazi zilizotekelezwa nje ya mpango na bajeti.

5.0 Taarifa ya mkakati wa kudhibiti uzalishaji wa madeni.

6.0 Mafanikio, Changamoto na Mapendekezo.

7.0 Hitimisho.

Kiambatisho Na. 1G

Gender Budget Statement Format

Table 1
Name of the Institution (Ministry/Region/District):____

<table>
<tr><td colspan="7">Program (Name of a Programme and Total Budget allocation):</td></tr>
<tr><td colspan="7">Project (Name of the project and Total Budget allocation):</td></tr>
<tr><td colspan="7">Priority Area [Gender and Women Development policy (2023)]</td></tr>
<tr><td>Gender Situational Analysis (Clearly state the existing gender problem in the selected S/P backed by sex disaggregated data where applicable).
• What is gender problem here?
• What is the root cause of the problem?
• What are the evidence? (sex disaggregated data), source?
• Is there any policy available?
• Is there any specific gender interventions needed?</td><td>Output (Is it the output gender responsive or its general)</td><td>Planned Activities to reduce the gender gap (does the activities aimed at closing the gender identified)</td><td>Output Indicator (dis aggregated by sex where applicable)</td><td>Baseline (2024/25)</td><td>Target 2026/27 (dis aggregated by sex where applicable)</td><td>Budget FY 2026/27</td></tr>
<tr><td>Total GBS Budget</td><td></td><td></td><td></td><td></td><td></td><td></td></tr>
</table>

Table 2
GBS Reporting format

REPORT ON THE IMPLEMENTATION OF GENDER BUDGET STATEMENT FY 2026/27							
Reporting Ministry/Region/District:							
Fiscal Year:2026/2027							
Program Name:							
Project Name:							
Priority Area							
Gender Situational Analysis:							
Output	**Planned Activities**	**Planned Targets**	**Achievements against planned activities, targets and indicators**	**Briefly describe immediate impact that were achieved through the planned interventions**	**Total executed budget Vs approved Budget FY 2026/27 and reasons for variance**		**Execution rate %**
					Approved budget	**Total executed budget**	